DRAFT PROGRAMME (Working Document)

WEDNESDAY, SEPTEMBER 6, 2017, Zanzibar, United Republic of Tanzania

<table>
<tr><td>8.00 am - 9.00 am</td><td colspan="2">Registration</td><td>Meeting Room</td><td>EAKC Secretariat</td></tr>
<tr><td>9.00 am - 10.00 am</td><td colspan="3">Welcome Remarks & Opening Ceremonies
1. EAC Anthem
2. Executive Secretary, East African Kiswahili Commission
3. Secretary General, East African Community
4. Chairman, EAC Council of Ministers
5. Guest of Honour</td><td>Session Chair
Rapporteur</td></tr>
<tr><td>10.00 am - 10.30 am</td><td colspan="4">Health Break</td></tr>
<tr><td rowspan="2">10.30 am - 11.30 am</td><td colspan="4">Plenary Session – Meeting Room</td></tr>
<tr><td colspan="3">Keynote Address 1 - Prof. Alamin Mazrui</td><td>Session Chair Prof. Mlinzi Mulokozi
Rapporteur</td></tr>
<tr><td rowspan="2">11.30 am - 1.00 pm</td><td colspan="4">Parallel Sessions</td></tr>
<tr><td>Meeting Room
Kiswahili and Regional Integration

Session Chair
Rapporteur

Presenters
1. Jactone Onyango & Ireri Mbaabu
2. James O. Ontieri
1. Kabange M. Ernest
2. Kasombo T. Michael
3. Levis D. Niyonkuru
4. Mwenda Mbatia
5. Nancy K. Ayodi
6. Patrice Ntawigira
7. Prisca Jerono
8. Aidah Mutenyo
9. Anthoney Owino Oloo
10. Daniel Ochieng Orwenjo
11. Muthahinga Moses & Kulava Y. S.</td><td>Conference Hall 1
Kiswahili and Development

Session Chair
Rapporteur

Presenters
1. Clara Momanyi
2. Cyprien Niyomugabo
3. Denis Bukuru & Lothaire Niyonkuru
4. Fulgence Nintunze
5. Fidelite Niyokwizigira
6. George Mrikaria
7. Hadija Jilala
8. Isaac I. Odeo
9. Kimani Njogu
10. Mwanakombo Mohamed
11. Peter Mose
12. Tirizeye J. Claude
13. Sangai Mohochi</td><td>Conference Hall 2
Kiswahili and Education (I)

Session Chair
Rapporteur

Presenters
1. Ahmad Y. Sovu
2. Alex Umbima Kevogo & Nelly Kitonga
3. Ally S. Khalfan
4. Aneth Kasebele
5. Andele F. Henry & Oduori T. Wamubi
6. Benson Oduor Ojwang
7. Daulat Abdalla Said & Salma Omar Hamad
8. Dismas Sibweche
9. Dorothée Nshimimana
10. Leonard Chacha & Anjejo Mark</td><td>Rooftop Place
Kiswahili, Trade and Business

Session Chair
Rapporteur

Presenters
1. Elizabeth G. Mahenge
2. Emmanuel Ndayisaba
3. Hanah C. Mwaliwa
4. Lubuuka Yunusu
5. Miriam Mwita
6. Pacifique Malonga
7. Phibian Muthama
8. Privat Nibaruta
9. Rachel Maina
10. Sophie Okwena
11. Timothy K. M'Ngaruthi</td></tr>
</table>

<table>
<tr><td>1.00 pm - 2.00 pm</td><td colspan="4">Lunch Break</td></tr>
<tr><td>2.00 pm - 3.00 pm</td><td colspan="4">Plenary Session – Meeting Room</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="4">Goodwill Messages I

Session Chair Rapporteur
1. H.E Ali Hassan Mwinyi
2. EAC Secretariat
3. East African Legislative Assembly
4. East African Court of Justice
5. Lake Victoria Fisheries Organization
6. Civil Aviation Safety and Security Oversight Authority
7. Inter-University Council for East Africa
8. Lake Victoria Basin Commission
9. East African Health Research Commission
10. East African Science and Technology Commission
11. East African Business Council</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="4">Parallel Sessions</td></tr>
<tr><td></td><td>Kiswahili and Education (II)

Session Chair
Rapporteur

Presenters
1. Genie C. Irankunda
2. Gervas A. Kawonga
3. Jactone Onyango & Ireri Mbaabu
4. Jane A. Oduor
5. John Habwe
6. Lothaire Niyonkuro
7. Mbwarali Kame
8. Mussa M. Hans
9. Mwanahija A. Juma & Amour S. Said
10. Mwenda Mukuthuria, James Ontieri & Stanley Adika</td><td>Kiswahili and Democratization

Session Chair
Rapporteur

Presenters
1. Abdulrahim H. Taib & Maimuna A. Makallo
2. Aldin K. Mutembei
3. Catherine Ndungo
4. Chande Omar
5. Deborah N. Amukowa
6. Fokas Nchimbi
7. James M. Mwita
8. Masereka L. Kahaika
9. Nathan O. Ogechi</td><td>Kiswahili, Media and Public Spaces

Session Chair
Rapporteur

Presenters
1. Anne Munuku
2. Ayub Mukhwana
3. Basilio Gichobi Mungania
4. Elias Majambere
5. Ellen Otieno, Inyani Simala & John Habwe.
6. Eric Niyongabo
7. Esther Chomba & Patrick Muhoni
8. Hamad Khamis & Zainab A. Idd
9. Hamisi Babusa
10. Hezekiel Gikambi
11. James M. Mwita</td><td>Kiswahili Literature and Integration (I)

Session Chair
Rapporteur

Presenters
1. Abdulrahim H. Taib & Maimuna A. Makallo
2. Ahmad Kipacha
3. Arnold B.G.Msigwa
4. Carren Nyandiba
5. Daulat A. Said
6. Jacob Mwita
7. Joachim Kisanji
8. Joseph N. Maitaria
9. Judith Mwavali
10. Magdaline Wafula</td></tr>
<tr><td>4.30 pm - 5.00 pm</td><td colspan="4">Health Break</td></tr>
<tr><td>6.00 pm - 8.00 pm</td><td colspan="4">Official Launch of the EAKC Strategic Plan (2017 – 2022) & Conference Dinner</td></tr>
</table>

THURSDAY, SEPTEMBER 7, 2017

8.30 am – 9.30 am	**Plenary Session – Meeting Room**			
	Goodwill Messages (II) **Session Chair**		**Rapporteur**	
	1. DAAD 2. Council for the Development of Social Science Research in Africa (CODESRIA) 3. Republic of Burundi 4. Republic of Kenya		5. Republic of Rwanda 6. Republic of South Sudan 7. Republic of Tanzania 8. Republic of Uganda)	
9.30 am – 10.30 am	**Key Note Address 2**: Prof. F.E.M.K. Senkoro		**Session Chair:** Prof. Clara Momanyi **Rapporteur**	
10.30 am – 11.00 am	**Health Break**			
11.00 am – 1.00 pm	**Kiswahili, Media and Public Spaces** **Session Chair** **Rapporteur** **Presenters** 1. Ken Walibora 2. Marcel K. M. Ubi 3. Monday A. Amazima 4. Nancy J. Ngowa & Deo Ngonyani 5. Niyokindi Valere 6. Pamela A. Oloo 7. Riziki Jacob 8. Shani Omari 9. Toboso M. Bernard & Mosol Kandagor 10. Wilson Okaka & Irene J. Nagasha 11. Yasin S. Musa	**Kiswahili Literature and Integration (II)** **Session Chair** **Rapporteur** **Presenters** 1. Masoud N. Mohamed 2. Mlinzi Mulokozi 3. Omar S. Mohamed 4. Pamela M. Ngugi 5. Rayya Timammy 6. Salma O. Hamad 7. Suleiman Haji & Yassin S. Mussa 8. Titus Kaui 9. Wallace Mlaga 10. Willy Migodela 11. Zaharia M. Alawy 12. Ziada Haji Ali	**Kiswahili, Literacy and Health** **Session Chair** **Rapporteur** **Presenters** 1. Anna M. Kishe 2. Gertrude Joseph 3. Miriam Osore 4. Patience Mbonabuca 5. Sheila Wandera-Simwa	**Kiswahili, Education and Change (III)** **Session Chair** **Rapporteur** **Presenters** 1. Nasra Habibu Ally 2. Nkinde Mwangoka 3. Richard M. Wafula 4. Rocha Chimera 5. Sarah N. M. Ngesu 6. Seleman Sewangi 7. Silas O. Owala 8. Sirin Demirci 9. Tatien Masharabu 10. Zuhura A. Moh'd 11. Ondara K. Reuben 12. Susan C. Choge
1.00 pm – 2.00 pm	**Health Break**			
2.00 pm – 3.00 pm	**Final Remarks & Closing Ceremonies**			

FRIDAY, 8TH SEPTEMBER, 2017: EXCURSION

ABSTRACTS

Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Taarab: Uchanganuzi wa Kifeministi

Abdulrahim Hussein Taib
Chuo Kikuu cha Egerton
na
Maimuna Ahmed Makallo
Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar
B-p: husseintalibali@gmail.com

Ufeministi ni mtazamo ambao imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi-pingu ambazo zimejengeka kwenye msimamo na itikadi ya kiume. Wanawake ni viumbe wanaopitia maudhi mengi na unyanyasaji katika jamii. Wamenyanyaswa na wamejaa machungu kwenye mioyo yao. Jukwaa la nyimbo linawapa fursa ya kuonyesha uchungu na matatizo mengi walionao. Lakini cha kushangaza ni kwamba, nyimbo kama za taarab ambazo nyingi huimbwa na wanawake zilikuwa na zimaendelea kuimbwa zenye kubeba taswira hasi dhidi ya mwanamke. Ni kutokana hali hiyo makala hii inaazimia kutumia Nadharia ya Ufemenisti kama kurunzi ya kumulikia ufaafu na usiofaafu wa wa taswira unaojitokeza katika nyimbo za Taarab.

Nafasi ya Dini katika Amani

Abdulrahim Hussein Taib
Chuo Kikuu cha Egerton
Na
Maimuna Ahmed Makallo
Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar
husseintalibali@gmail.com

Imani ndiyo kitu cha kwanza kinachohitajika kwa mwanadamu kabla kupatikana amani. Hapa imani inakuwa ni ngazi ya kufikia hiyo amani. Imedhihirika ulimwenguni kote kwamba amani iliyokuwepo au hata ile iliyopo inatishiwa kutoweka katika jamii zetu. Na hali hii tunaweza kusema huenda ikawa imesababishwa na kukosekana imani. Tunapozungumzia suala la kuleta amani, hatunabudi kufahamu kwamba amani sio kitu ambacho kitazungumzwa kwenye jukwaa; au makongamano au madukani kwenda kuinunua kwa thamani yoyote ile. La, bali amani ni suala ililojumisha jumla yaa mambo yanayozunguka maisha ya mwanadamu. Hivyo makala hii ina azimia kudadisi kubainisha na kupendekeza njia mwafaka ambazo lao zitazingatiwa huenda likatoa moja ya suluhisho ya kutatua tatizo la kukosekana kwa amani.

“Tone la Maji”: Metonomia za Usawiri wa Uongozi Bora za Shaaban Robert

Ahmad Kipacha
B-p: Ahmadi.kipacha@nm.aist.ac.tz/ahkipacha@gmail.com
Makala yanasawiri namna tamathali ya metonomia inavyotumika katika riwaya za *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1968) za Shaaban Robert (19091-1962) kuweka bayana dhamira ya uongozi bora wa jamii kwa kunasibisha vikoa vya aina tatu vya kimetonomia: vya kimaumbile ya kijiografia, vitendea kazi na viungo vya mwili wa mwanadamu na misingi mbalimbali ya uongozi bora. “Tone la maji” ni taswira ya viongozi kuwa ni waleta mvua ya maafa au mvua ya manufaa. “Mpini” katika shoka ni taswira ya viongozi kuwa wachanjaji kuni na anawawajibisha washikilie kisehemu hicho cha shoka ili “kufungua milango” ya ustawi. “Ulimi wa nasaha” kulenga kauli za viongozi kuepuka kutema “mate ya sumu” mbele ya “macho ya watu” katika huu “uso wa ardhi” kwani wanawajibika kuwa ni “mkono wa uokovu” wa kuleta manufaa “bega kwa vega” na wananchi haswa kwa kuzingatia kuwa kilimo ni “uti wa mgongo” wa maendeleo ya jamii. Kwa kutumia Modeli za Lakoff & Johnson (1980) na Kovecses Zoltan (2010) za KISABABISHI kuwa TOKEO na KIJISEHEMU kuwakilisha KIZIMA tunafafanua ni kwa kiasi gani nyenzo ya kimetonomia imefanikiwa kuibua misingi ya uongozi bora kwa jamii yake. Ni lipi tunaloweza kujifunza kutoka kwa nguli Shaaban Robert ili kuwafunda vijana na umma kwa ujumla juu ya maadili ya viongozi wa jamii zetu hususan wanapopewa dhamana ya uongozi kupitia umetonomia? Mchango wa makala haya ni kuuchanganua mchango wa riwaya hizo teule katika masuala ya kisiasa na uongozi wa jamii kwa lenzi ya kimetonomia kujalizia kazi za awali za uhakiki wa Kifasihi za Mbuguni (1978) Leslie (2010) Wafula (2014) na Massawe (2014) zilizotangulia.

Changamoto za Uingizaji wa sera ya Lugha katika sera za Elimu na Utamaduni: Haja ya kuwa na sera mahususi ya lugha Tanzania

Ahmad Y. Sovu
sovu82@gmail.com
Makala haya yanajadili changamoto mbalimbali zinazohuisiana na sera ya lugha, ambayo kwa kadri ya ufahamu wetu hadi sasa hatuna sera mahususi ya lugha katika nchi ya Tanzania, badala yake masuala ya lugha yameingizwa katika sera ya Utamaduni na sera ya elimu. Sera ya lugha ni jumla ya mawazo, matamko, sheria, kanuni na taratibu zenye kufafanua utekelezaji wa mabadiliko ya matumizi ya lugha Mekacha, (2000) Msanjila, (2009). Aidha, makala yanafafanua kuhusu dhana, aina ya sera za lugha na kuonesha mifano ya sera ya lugha kama ilivyoingizwa katika sera ya utamaduni na elimu. Data katika makala haya kwa kiasi kikubwa zimekusanywa kutoka maktaba na kwa wadau mbalimbali wa lugha. Changamoto zilizojadiliwa ni pamoja na; kutokuanishwa kwa mpango wa utekelezaji wa sera, sera ya lugha kushughulikia suala la elimu tu, kutokupewa nafasi ya lugha nyingine za jamii n.k. Kwa mintarafu ya changamoto hizo, makala haya yanabainisha sababu za changamoto hizi na kubainisha faida za kuhusu haja ya kuwa na sera madhubuti na mahususi ya lugha nchinia Tanzania ili ipambanue nafasi ya kila lugha (Kiswahili, lugha za kigeni na lugha za jamii) katika masuala ya kiuchumi, kuhifadhi utamaduni, mawasiliano na teknolojia n.k. Kwa ujumla, makala haya yanatoa mchango kwa watunga sera, serikali na wananchi wa Tanzania na wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwani kadri lugha zinapopewa nafasi

ya kutumiwa inayostahili basi bila shaka kasi ya maendeleo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zitapiga hatua katika nyanja anuwai

Kiswahili,Utandawazi na Ushirikiano wa Maendeleo.

Aidah Mutenyo
Chuo Kikuu cha Kyambogo-Uganda

aidahmutenyo@gmail.com

Erastus Miricho na wengine wamefasili Lugha kama mfumo wa sauti nasibu zenye kubeba maana na ambazo zimekubaliwa na jamii ya watu fulani zitumike katika mawasiliano. Naye Kimani Njogu na wenzake,wamefasili lugha kama mfumo wa sauti nasibu wenye mpangilio,unaoleta maana maalum na kuwezesha mawasiliano.Sauti za lugha hutamkwa kwa mdomo,na huweza kudhihirishwa kwa ishara ya maandishi. Kiswahili ni lugha ya kibantu iliyo na manufaa mengi ya kipekee. Uchunguzi huonyesha kuwa Kiswahili kimekuwa kikitumika Afrika zaidi ya miaka elfu moja iliyopita. Kumaanisha Kiswahili kama chombo cha mawasiliano kina mchangu mkubwa sana katika utandawazi na ushirikiano wa maendeleo. Makala haya yatajadili jinsi matumizi ya Kiswahili,utandawazi na ushirikiano wa maendeleo utakavyofanikisha malengo endelevu ya maendeleo katika mazingira yanayobadilika.

Demokrasia, Kiswahili na Maendeleo ya Wananchi wa Afrika Mashariki

Aldin K. Mutembei
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
mutembei@yahoo.com

Lugha ni miongoni mwa mihimili muhimu sana katika demokrasia. Katika nchi zote ambazo zinajieleza kuwa kiwango chao cha demokrasia kipo juu, lugha imetiliwa maanani na kuendelezwa ili wananchi katika nchi hizo waweze sio tu kujua maana ya maendeleo, bali wajiletee wenyewe maendeleo wayatakayo. Yawe ni maendeleo ya kijamii, kisiasa au kiuchumi. Kwa maneno mengine, ni kupitia katika lugha ambapo wananchi wameshiriki bila kulazimishwa katika kuijenga demokrasia nchini mwao. Kwa hakika mawazo ya dhana ya demokrasia kutokea Uyunani ya kale yaliangalia kwa jicho la kipekee dhima ya lugha katika jamii. Makala hii, inalenga kuangalia suala la lugha ya Kiswahili katika kuiimarisha demokrasia katika nchi za Afrika Mashariki. Makala itatumia mkabala wa kihistoria ili kujadili kuhusu uelewa wa wananchi na namna uelewa huo unavyofungamana na kujiletea wenyewe maendeleo. Tukitumia nadharia ya uhalisia, tunataka kuzitathmini jamii za Afrika mashariki na kuangalia nafasi ya lugha katika kujenga demokrasia na kuimarisha maendeleo.

Juhudi zisizo rasmi za kuimarisha hali ya kujua kusoma na kuandika katika Kiswahili nchini Kenya

Alex Umbima Kevogo
Chuo Kikuu Kishiriki cha Garissa
na
Nelly Kitonga
Chuo Kikuu Kishiriki cha Garissa
umbima2000@gmail.com/nellykitonga@yahoo.com

Kuanzia miaka ya 1960, hali ya kujua kusoma na kuandika ilikuwa muhimu kwa mataifa masikini duniani kuanza kujiinua na kujitegemea kiuchumi (Lankshear na Knobel, 2006). Hii ni kwa sababu hali ya kujua kusoma, kuandika na kuhesabu humwezesha mwananchi yeyote yule kushiriki kiuamilifu kwenye mijadala, uamuzi na shughuli za kitaifa ambazo huchangia maendeleo ya taifa lake. Tangu kujinyakulia uhuru, mataifa ya Afrika Mashariki yameimarisha juhudi za kuinua viwango vya kujua kusoma na kuandika. Juhudi hizo huendeshwa katika miktadha ya kitaasisi na isiyo ya kitaasisi. Aidha, mashirika ya kiserikali na yale yasiyo ya kiserikali yamehusika kwa njia moja au nyingine kuimarisha hali ya kujua kusoma na kuandika. Juhudi hizo za kuinua hali ya kujua kusoma na kuandika zimekuwa na athari ya kuendeleza matumizi ya lugha za Kiafrika na hata za kigeni. Lengo la makala ni kuchunguza juhudi zinazofanywa na wakala wa kiserikali na wale wasio wa kiserikali kuinua hali ya kujua kusoma na kuandika katika miktadha isiyo rasmi nchini Kenya. Baadhi ya mbinu zinazotumiwa na wakala hao ni kukariri matini zilizoandikwa na uchunguzi shiriki (Nabea, 2009). Makala yananuiwa kutoa kwanga kuhusu juhudi zisizo za kitaasisi zinazofanywa na wakala wa kuinua viwango vya kujua kusoma na kuandika nchini Kenya.

Umuhimu wa kuzingatia utamaduni katika Nadharia za uundaji wa Istilahi

Ally S. Khalfan
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)
ally.khalfan@suza.ac.tz/alialbatawy@yahoo.com

Mnamo karne za 18 na 19 wanazuoni walishangazwa sana kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa istilahi na tofauti zilizokuwepo kati ya istilahi na dhana zinazowakilishwa na istilahi hizo. Hali hii ilisababisha kuanza kuibuka kwa nadharia zilizoongoza uundaji wa istilahi zilizoasisiwa na mwanaistilahi wa Kiaustria Eugene Wüster, ambaye awali alikuwa na raghba ya kuunda utaratibu maalumu wa ukusanyaji na usanifishaji wa istilahi. Nadharia Asilia ya Istilahi - NAI (*General Theory of Terminology*) (tafsiri ni yangu) ya Wüster ilifungua milango ya nadharia nyengine kadhaa katika uwanja huu wa kitaaluma, zikiwemo Nadharia ya Istilahi ya Isimu Jamii (Gaudin: 1993), Nadharia ya Istilahi ya Jamii na Akili (Termmeman: 2000) na Nadharia ya Istilahi ya Mielekeo Anuai au Nadharia ya Istilahi ya Milango (Cabré: 2003). Hata hivyo, nadharia zote hizi zinatilia mkazo zaidi usahihi wa uhusiano kati ya istilahi na dhana inayowakilisha istilahi husika pamoja na ukubalifu wa istilahi husika kwa watumiaji. Katika kufikia vigezo hivyo, nadharia zinasisitiza umuhimu wa vipengele vya lugha na maana kama misingi ya kukubalika kwa istilahi. Makala hii inajaribu kuonesha kubwa suala la utamaduni wa jamii lina nafasi kubwa katika kukubalika kwa istilahi, na hivyo kuna haja ya kuongeza kipengele cha utamaduni katika Nadharia ya Istilahi.

Ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Tanzania.

Aneth Kasebele
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa.
akasebele@yahoo.com

Katika nchi ya Tanzania, Kiswahili kinatumika kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi. Pia, Kiswahili kinafundishwa kama somo la lazima katika shule za sekondari kwa kidato cha kwanza mpaka cha nne. Vilevile, Kiswahili kinafundishwa kama somo la hiari katika shule za sekondari kwa kidato cha tano mpaka cha sita na vyuo vikuu. Makala haya, yana lengo la kufafanua ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vya elimu ya juu nchini. Ili kufanikisha lengo

hilo, tutaangalia mafanikio na changamoto zinazoukabili ufundishaji huo na mwisho tutatoa mapendekezo.

Kiswashili na mabadiliko ya kielimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

Andele F. Henry
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Oduori T. Wamubi
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

andelehenry@yahoo.com na timwamubi@gmail.com

Kazi inadhihirisha namna ambavyo Kiswahili kinaweza kutumiwa kuleta mabadiliko katika jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia katika mfumo wa elimu. Elimu ni nguzo muhimu ya maendeleo katika jamii. Hii inatokana na kauli ya Aggarwal (1985) kwamba elimu ni utamaduni ambao kila kizazi hukipokeza kizazi kinachofuatia ili kukiwezesha kudumisha au hata kuimarisha mafanikio yaliyopatikana. Hili ni dhihirisho kuwa elimu ni maisha yote anayopitia mtu kwa kutegemea urazini. Kwa hivyo, elimu ni maisha na maisha ni elimu ambayo ni sehemu ya utamaduni au hali ya maisha ya jamii fulani. Elimu hii huchangia katika kuleta mabadiliko ya nyanja mbalimbali za maisha ya binadamu. Lugha ni wenzo mkuu katika kufanikisha elimu ambayo hufungamana na utamaduni na maendeleo yanayotokana na mabadiliko chanya katika jamii. Mabadiliko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yanaweza kushehenezwa katika mfumo sawa wa elimu kwa nchi husika ambazo kwa sasa zina mifumo ya elimu iliyo tofauti. Lugha ya Kiswahili inaweza kuwa wenzo muhimu wa kusawazisha mifumo hii. Jinsi ilivyo sasa, kila nchi ina mfumo wa elimu wenye sera tofauti za matumizi ya lugha. Nchi kama vile Kenya na Uganda hutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia na pia kama somo katika mtalaa wao wa elimu. Kiswahili nacho, hufunzwa tu kama somo. Hali hii inatinga pakubwa matumizi ya Kiswahili katika kufanikisha mabadiliko yanayotarajiwa. Kazi hii inapendekeza kuwa lugha ya Kiswahili itumiwe kwenye mfumo wa elimu kama wenzo wa kuleta mabadiliko muhimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Athari za ujinga wa Kusoma na Kuandika katika Maendeleo ya Afya ya Jamii – Tanzania

Anna M. Kishe

amkishe@yahoo.com

Ujinga si istlahi ngeni katika lugha ya Kiswahili. Katika kamusi ya Kiswahili sanifu ya TUKI (2004) ujinga ni hali yakutokujua kitu fulani, upumbavu, pia ubozi". Kumbe "ujinga" ina maana pana na inaweza ikasababishwa na mambo mengi. Mathalani unaweza kuwa mjinga au mpumbavu wa kutokujua kutumia simu ya mkononi hususan matumizi ya whatsAAp. Unaweza kuwa mjinga wa kutokuelewa umuhimu wa kunywa maji yaliyochemshwa au kwenda kumuona daktari mara unaposikia dalili za malaria. Lakini ujinga tunaokusudia kuuelezea hapa ni ule ujinga wa kutokujua kusoma na kuandika. Kujua kusoma na kuandika ni suala linalopewa uzito kama silaha ya kuleta maendeleo ya nchi; kiafya, kiuchmi kisiasa na kiutamaduni. Hili linajidhihirisha

wazi kaika mitaala ya Elimu ya kufundisha Elimu ya watu wazima. Hivyo basi, kujua kusoma na kuandika ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo ya afya. Kwa upande mwingine, kutokujua kusoma na kuandika kuna matokeo hasi. Lengo la makala haya ni kujadili athari za ujinga zinazotokana na kutokujua kusoma na kuandika katika maendeleoya afya ya jamii hususani Tanzania. Makala inakusudia kuonyesha vikwazo vinavyosababisha kuwepo na ufahamu mdogo wa kusoma na kuandika hasa katika masuala yanayohusu afya. Hatimaye tutajadili njia mbalimbali katika kukabiliana na tatizo hili. Makala itaongozwa na vipengele vifuatavyo katika kujadili mada hii: Nini dhima ya lugha katika jamii. Kwa nini ni muhimu kujua kusoma na kuandika? Athari za kutokua kuasoma na kuandika katika mapambano ya afya. Ni nini utatuzi wa changamoto hizi?

Matumizi ya lugha katika vichekesho meme (memes and gafes) kwenye mitandao ya kijamii Nchini Kenya

Anne Munuku
Chuo Kikuu cha Mount Kenya
amunuku@yahoo/com/amunuku@mku.ac.ke

Teknolojia ya habari na mawasiliano imeathiri sekta nyingi hapa nchini Kenya na kwingineko duniani. Kuingia kwa mitandao ya kijamii kuanzia mwaka wa 2005 na kuendelea kumechangia pakubwa katika kupanua nafasi ya demokrasia ambapo raia wa kawaida hupata nafasi ya kujieleza, kukosoa, kutoa maoni na hata kuungana na wengine katika ujenzi wa jamii meme. Katika kufanya hivi watu hutumia lugha tofauti. Nchini Kenya kuna matumizi ya lugha za Kiswahili na Kiingereza pamoja na lugha msimu ya Sheng'katika mitandao ya kijamii. Mawasiliano haya yanahusu maswala rasmi kama yanavyowasilishwa katika stesheni za kitaifa ambazo huwaslisha taarifa za habari kwenye mitandao kama Facebook na Twitter. Wananchi hutoa maoni yao katika mitandao hii na wakati mwingine hutumia vichekesho (memes na gafes) kujadili maswala mazito yanayotukia katika jamii. Makala hii ni ya kiutafiti na inanuia kueleza vichekesho hivi ambavyo hutumika katika mitandao ya Facebook na Whatsapp kwa kuangalia jinsi lugha inavyotumika hasa kimuundo, mtagusano wa lugha mbili au zaidi, maswala yanayomulikwa katika meme hizi na wahusika katika diskosi hii. Kwa jumla makala hii itazungumzia sifa za meme hizo kama diskosi katika mitandao ya kijamii iliyoteuliwa. Diskosi katika matini hii ni jumbe katika Whatsapp ambazo huchukua muundo wa vichekesho na ambazo hujulikana kama "memes" na "gafes" kwa lugha ya Kiingereza. Madhumuni ya utafiti yalikuwa: 1) Kukusanya jumbe za meme katika mtandao wa Facebook na Whatsapp; 2) Kubainisha sifa za jumbe hizo kimuundo na kimtindo; 3) Kuchunguza lugha zinazotumiwa na jinsi zinavyochanganywa kuunda ujumbe huo. Sampuli ya maksudi ilizingatiwa. Data ilikusanywa kupitia kwa makundi ya Whatsapp anayoshiriki mtafiti na katika kurasa za Facebook za Citizen TV na NTV pamoja na ukurasa wa mchekesheji mashuhuri Churchill. Nadharia ya uchanganuzi hakikifu wa diskosi kwa mujibu wa Fairclough (1998) ulitumika ili kuchanganua maswala ya jamii yanayochangia meme hizi na miundo ya matini katika meme ambayo huchukuliwa kama usemi kwa jumla. Kulingana na nadharia hii usemi huwa na majukumu matatu; kujenga uhusiano, kupitisha mawazo na kujitambulisha. Katika kuchanganua usemi huu matini (text) huchunguzwa pamoja na jinsi matini hiyo inavyopokelewa na kutumia (discursive practice) na hatimaye jinsi jamii pana invyohusishwa na usemi huo. Yote hayo hutokea katika tukio la mawasiliano. Aidha makala inanuia kuongeza maarifa katika usomi wa diskosi na kufungua mjadala kuhusu utanzu mpya unaokua haraka katika mitandao ya kijamii.

Social Media and technological violence against women in Kenya

Anne Munuku
Jomo Kenyatta University of Agriculture and Technology, Kenya.
amunuku@yahoo/com/amunuku@mku.ac.ke

Violence against women has been studied for decades since the invention of feminist thoughts and theories in the early 20th century. The relationship between humans based on gender is a question that continues to interest sociologists, ethnologists, educationists, linguists and generally all communication experts and scholars. A lot of research on gender relations exists. However the role of new technology on the propagation of discrimination against women or men is just beginning to be explored. The new term, TECHVAW (Technological Violence against Women) is a new concept that needs to be investigated. This paper builds on the body of research that already exists by examining gender relations in media, specifically new media in Kenya. The main objective of the paper is to show how women in Kenya are depicted in social media. The argument of the paper is that technological violence against women in Kenya is rife regardless of their economic status. To understand this issue, the language used against these women on social media is examined. The research is based on comments from the members of the general public on the social media walls of main television stations, specifically, Citizen TV, NTV and KTN, after a news item covering women. The news can be on achievements, tragic events, life issues and other debates where women are involved. Violence faced by women in online platforms can be investigated using different approaches of feminism including liberal capitalist feminism, cultural feminism, African feminism, commercial feminism and existential feminism. Due to the fact that this paper is based on an African society that mostly relies on socio-cultural norms for social interactions, African feminism is used to explain the phenomenon. The discussion of the paper is based on selected news items concerning ordinary women and celebrities whose stories were featured in those stations at different times. The news items were purposively selected since not all news concern women. To determine if the comments made by the general public are depicting violence against women, the form of language used is examined in terms of lexical choice and grammatical structure as well as the language chosen, that is Kiswahili, Sheng' or English, whenever a violent statement comes up. The number of positive, negative, neutral and conflicted comments is shown on table. The data is then presented in percentages to show the extent to which violence is being propagated in online discourse in Kenya's mainstream media.

Swahilihub kama Jukwaa la Utandawazishwaji wa Kiswahili

Anthoney Owino Oloo
Chuo Kikuu cha Kibabii
aowino@kibu.ac.ke / owinoanto@yahoo.co.uk

Lugha ya Kiswahili, ambayo ndiyo inayoongoza kwa ukubwa na umaarufu miongoni mwa lugha kuu za asili za Afrika imezidi kushuhudia mwamko mpya. Kadri inavyozidi kukubalika na kuashiria dalili za kutumiwa na watu wengi zaidi karibu duniani kote, ndivyo inavyozidi kukumbatia na kutumika kwenye majukwaa mbalimbali ya kiutandawazi. Miongoni mwa majukwaa hayo ni swahilihub ambayo ni mradi mahususi wa kukikuza, kukiendeleza na kukiimarisha Kiswahili. Tafsiri ya Swahili Hub ni Kitovu cha Kiswahili. Ni tovuti inayohifadhi,

kukuza na kuendeleza taaluma ya Kiswahili mtandaoni. Ni jukwaa mojawapo ya majukwaa yanayohimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili kitaaluma mtandaoni. Kiswahili pia kinatumika vilivyo katika tovuti kwa kupeana, kupeleka na kutafutia taarifa. Tovuti za Kiswahili zimezagaa duniani kote, nyingi zikiwa Marekani na Ulaya, lakini hata Afrika zimeanza kusimikwa. Kuna tovuti zenye kozi za kufundisha Kiswahili, kwa kusoma na kusikia kupitia kompyuta na zipo zenye kamusi za Kiswahili, makala au maelezo ya kitaaluma kuhusu Kiswahili. Zipo injini za upekuzi (search engines) zenye kutumia Kiswahili (mfano Google). Juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanywa katika kukienzi Kiswahili katika nyanja za sayansi na teknolojia. Miongoni mwa juhudi hizo ni kutekelezwa kwa Mradi wa Swahili Language Manager (SALAMA) kwa ushirikiano wa Taasisi za Taaluma za Kiswahili (TATAKI) na Chuo Kikuu cha Helsinki unaokusanya maneno na matini ya lugha ya Kiswahili ili kuunda kopora (kusanyo la data za lugha), na kisha kuyachanganua kiisimu, kuyapatia tafsiri ya Kiingereza, na kuyahifadhi katika kanzi kwa ajili ya watumiaji. Makala hii inalenga kubainisha nafasi ya kipekee ya tovuti ya swahilihub katika kuimarisha juhudi mbalimbali za kuitumia lugha ya Kiswahili kwenye mawanda ya kiutandawazi.

Kukakamaa[1] kwa Wajifunzaji wa Lugha ya Pili nchini Tanzania: Mifano kutoka kwa Wajifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Jamii ya Wakinga

Arnold B.G.Msigwa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
agawasike@gmail.om

Wajifunzaji lugha ya Pili hukabiliwa na changamoto mbalimbali katika kumudu lugha ya Kiswahili. Chanzo cha changamoto hizo zinaelekea kutokuwa na namna moja ya kuzieleza. Makala haya kwa hiyo, yanalenga kufafanua chanzo cha kukakamaa kwa Wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamiilugha teule nchini Tanzania. Kwa kuwa jamii mbalimbali za Kitanzania ziishizo vijijini mazingira yake yanaelekea kufanana, mifano kutoka kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga itatumika. Swali linaloibuliwa na makala haya ni, Je, kukakamaa kunakowapata Wajifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga kunasababishwa na nini?

Vyombo vya Habari na Taaluma ya Kiswahili Kenya: Mchango wa Gazeti la *Taifa Leo*.

Ayub Mukhwana
Chuo Kikuu cha Nairobi
ayubumukhwana@yahoo.com

Vyombo vya habari vinayo historia ndefu ya ukuzaji na uimarishaji wa sio tu lugha ya Kiswahili, bali lugha zote zilizowahi kuandikwa au kutumiwa katika vyombo vya habari view vya machapisho au vya elektroni. Makala hii inamulika namna vyombo vya habari vinakuza taaluma vya Kiswahili. Makala hii inayo malengo ya kubaini ufaafu wa vyombo vya habari katika kukuza taaluma ya Kiswahili kama vifaavyo kuigika na vingine Kenya na kuonyesha changamoto ambazo zinaweza kuhasiri ukuzaji wa taalauma ya Kiswahili kutokana na vyombo vya habari. Makala hii itajikita katika gazeti la Kiswahili Kenya ambalo ni Taifa Leo na tasnifu ya makala hii ni kuwa gazeti la Taifa Leo lafaa kufanya zaidi ya linavyofanya ili kuwa chombo cha habari kinachokuza

Ni dosari sugu ambazo hazibadiliki licha ya mjifunzaji kufunzwa vema na waalimu, kuwa na muda wa kufanya mazoezi juu ya jambo alilojifunza na kuendelea kupata ingizo kutoka kwa walimu au jamii inayomzunguka.

vyema taaluma ya Kiswahili. Data kwa ajili ya makala hii imepatikana kupitia kwa usomaji wa magazeti na maandishi mengineyo mbali na kuitathmini hali halisi ya gazeti la Taifa Leo Kenya. Hata hivyo, mengi katika mambo yatakayosemwa kuhusu gazeti la Taifa Leo Kenya yanaweza vilevile kutumikizwa kwa magazeti yaandikwayo kwa lugha za kiasili katika eneo hili la Afrika Mashariki.

Vyombo vya Habari na mchakato wa kueneza au/na kudumaza matumizi ya Kiswahili Afrika mashariki

Basilio Gichobi Mungania
Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya
gmungania@uonbi.ac.ke

Jamii za Afrika hazina historia ndefu ya vyombo vya habari. Hapo awali sisi Wafrika tulikuwa tukitegemea sana mawasiliano ya ana kwa ana. Tangu vyombo vya kisasa vilipoletwa hapa kwetu, vimekuwa vikitegemewa na wananchi wengi sana sio tu kwa taarifa za habari peke yake bali pia kwa matumizi yafaayo ya lugha. Cho chote kinachowafikia wasikilizaji au watazamaji kupitia vyombo hivi huchukuliwa kuwa ni ukweli mtupu. Wasikilizaji wengi huamini chochote kile kinachowafikia kupitia vyombo vya habari. Wasikilizaji wengi huwa wanavitegemea vyombo hivi katika kujifunza sarufi na matumizi bora ya lugha ya Kiswahili. Imani ya wasikilizaji au/na watazamaji wengi ni kuwa washiriki katika vyombo hivi huwa wanatumia sarufi inayofaa. Wasikilizaji na watazamaji wengi hujaribu iwezekanavyo kuiga matumizi ya lugha inayotumiwa katika vyombo hivi vya habari. Hata hivyo, kunayo matumizi mengi yasiyofaa ambayo yanatumiwa na watangazaji pamoja na watu wengineo wanaochangia mijadala katika vyombo hivi kila uchao. Madhumuni ya karatasi hii ni kuchanganua mchango wa vyombo vya habari ama katika kuendeleza au/na kudumaza maendeleo na matumizi ya Kiswahili kama chombo cha mawasilianao katika Afrika Mashariki. Kadhalika itajaribu kupendekeza mbinu zinazoweza kutumiwa ili kuhakikisha kuwa matumizi ya lugha katika vyombo hivi yanazingatia sarufi faafu ya Kiswahili.

Migrant Speech Communities as Catalysts for Promoting Kiswahili in the Luo Region of Kenya

Benson Oduor Ojwang
Maseno University
kojwa@yahoo.com

The acceptance of Kiswahili as a medium of everyday communication has been lacklustre among the Luo of Kenya. This has partly been attributed to historical factors such as mistrust of the enterprising Swahili traders who brought goods to the hinterland and were perceived to manipulate the language to fleece their undiscerning upcountry clients. Such experiences and encounters led to perceptions of Kiswahili as the language of the oppressor hence strong attitudes developed that eventually militated against the acceptance of Kiswahili. Moreover, the Luo are particularly perceived as having acquired a sub-standard variety of Kiswahili due to their sheer lack of interest. In contrast, the Luo propensity to identify more with English and gain proficiency in the foreign language as a marker of sophistication was stronger. This attitude is no longer tenable since Kiswahili has since been promoted in status serving both as a national language and a co-official

language with English besides being a compulsory examinable subject in school. There is therefore need to enhance acceptability of Kiswahili among the Luo. One strategy of achieving this is to recognize the catalyzing role of migrant communities such as the Luo who relocated to Tanzania in the early 60's mainly as traders and farmers and who continue to maintain links with their Kenyan kin despite their assimilation into the Tanzanian system. In the Luo region, there are also pockets of Swahili, Arabic, Asian and Nubi immigrants settled in the interior. The primary language of contact of these settlers with the Luo is Kiswahili. This paper examines the sociolinguistic factors that determine the acquisition and trends of use of Kiswahili among Kenyan Luo in the face of increased cross-border movement among EAC citizens. It is concluded that social and political integration of the East African Luo with other EAC members can be facilitated by the diffusion of Kiswahili both within and across the nations.

Fasihi Kidijitali (?): Mfano wa 'Sipendi Ujinga'

Carren Nyandiba
Chuo Kikuu cha Rongo.
carrynyandiba@gmail.com

Fasili mbalimbali zimetolewa kuhusu dhana ya fasihi. Baadhi ya fasili zimetolewa na (Njogu na Chimera, 1999; Wamitilla, 2008; Wanjala, 2011). Wote hawa wanaafiki kwamba fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa namna maalum inayoathiri, na kupitisha ujumbe unaomhusu binadamu. Uteuzi wa lugha katika fasihi hufanywa kwa ufundi wa hali ya juu, na kwa sababu hiyo lugha ya fasihi huwa na upekee fulani ikilinganishwa kazi nyinginezo zisizokuwa za kifasihi. Fasihi huweza kuwasilishwa kupitia maandishi au matamshi pamoja na matendo kwa kuchukua maumbo kama riwaya, hadithi fupi, nyimbo, mashairi, tamthilia na kadhalika. Fasihi hubadilika kadri jamii inavyobadilika. Mabadiliko katika jamii huathiri maudhui, aina na hata uwasilishaji wa fasihi. Miongoni mwa mabadiliko ya jamii yaliyoathiri fasihi ni jamii kuimarika kidijitali. Katika jamii ya sasa, mawasiliano mengi yanafanywa kwa njia ya kidijitali ambapo kuna matumizi ya tarakilishi, na simu kama zana kuu za kuwezeha mawasiliano hayo. Jamii imeshuhudia uibukaji wa mitandao mbalimbali ya kimawasiliano ya kijamii kama vile *facebook, whatsup, twitter, Instagram,* jumbe fupi za simu na kadhalika. Fasihi nayo haijasazwa nyuma kwani sasa kuna maandishi yanayoweza kuchukuliwa kama ya kifasihi yanayobuniwa na kusambazwa kidijitali. Makala hii inachunguza aina hiyo ya maandishi inayosambazwa katika mitandao ya kijamii ya *facebook* na *whatsup* inayotambulika kwa jina 'sipendi ujinga.' Lengo la makala hii ni kuchunguza sifa za kifasihi katika maandishi haya na iwapo maandishi hayo yanaweza kuchukuliwa kama kipera cha fasihi au la.

Nafasi ya Kiswahili katika Siasa na Demokrasia Nchini Kenya

Catherine Ndungo
Chuo Kikuu cha Kenyatta
catemndungo@gmail.com

Tangu kuidhinishwa kwa katiba ya Kenya ya mwaka 2010, kumekuwa na juhudi kambambe za kuelimisha umma juu ya haki zao kwa muujibu wa katiba hasa katika muktadha wa siasa na

demokrasia. Baadhi ya wadau katika mchakato huu ni mashirika ya kimataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali , madhehebu ya kidini na watu binafsi ambao wamejitwika mzigo wa kuhakikisha kuwa umma umemakinika hasa katika nyanja za siasa na demokrasia. Hata hivyo baadhi ya wadau kama Chombo cha Ukaguzi wa Mchakato wa Uchaguzi, shirika la Wapenzi wa Esta na Debora na Asasi ya Elimu ya Demokrasia wamedai kuwa, juhudi za kuelimisha umma juu ya siasa na demokrasia hazijafanikiwa. Kuna sababu kadha ambazo zimehusishwa na hali hii zikiwemo kukithiri kwa ufisadi hasa wakati wa kupiga kura, wapiga kura wengi kutokuwa na elimu ,ukabila na katika orodha hii ninaongeza uteuzi wa lugha ya kuendesha elimu juu ya siasa na demokrasia .Shughuli nyingi kuhusu siasa na demokrasia kama vile vijitabu, mabango na mijadala katika vyombo vya habari vya umma kama magazeti,runinga na redio zimeendeshwa kwa lugha ya kiingereza ambayo ni ya kigeni kwa Wakenya wengi. Hapajakuwa na juhudi za kuendesha shughuli hizi kwa lugha ya mwananchi wa kawaida wa Kenya ambayo ni Kiswahili. Mandela amedai kuwa iwapo unanuia kufikia roho ya mtu huna budi kutumia lugha yake. Makala haya yanalenga kuchunguza hali hiyo kwa kutoa rai kuwa iwapo mwananchi anayelengwa na juhudi hizo hatafikiwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha ya walio wengi, juhudi hizo zitaambulia patupu na Malengo ya Maendeleo Endelevu yatasalia kuwa ndoto.

Demokrasia, Kiswahili na Maendeleo ya Wananchi wa Afrika Mashariki

Chande Omar
chande_omar@yahoo.com

Watangazaji wengi vijana wanaofanyakazi katika vyombo vya habari hutumia Kiswahili kisicho rasmi. Jambo hili hupelekea malalamiko mengi kutoka kwa wanajamii wenye umri mkubwa. Halkadhalka vyombo vinavyo simamia matumizi ya lugha huvinyooshea vidole vyombo vya habari kwa matumizi mabaya ya lugha.Pia shutuma ni nyingi kwa vyombo vya habari hutoka kwa viongozi wa serikali na wanasiasa. Vyombo vya habari vinaonekanwa vinapindukia mipaka katika matumizi ya lugha. Jambo lisiloangaliwa ni jinsi ya mabadiliko yanayotakea katika jamii, kwamba watumiaji wengi wa lugha hii ni vijana na watoto wenye umri chini ya miaka 35. Vijana hawa wamekua kwa namna nyengine na mazingira tofauti na wale wanaotoa shutuma za matumizi mabaya ya lugha. Hivi sasa lugha ni ya kasi (fast language), ya uwazi (openeness) na huzingatia teknolojia ya chombo cha mawasiiano. Vijana wanaokua katika wakati huu huathiriwa na mambo hayo kiasi kwamba utumiaji wao wa lugha huwa tofauti na wazee wao. Vijana wanaoajiriwa katika vyombo vya habari hulazimika kutumia lugha katika ufahamu wao kulingana na mwenenendo wa utamaduni wa wakati. Lugha yao ni ya mchanganyiko kutokana na utandawazi na elimu wanayopata shuleni na katika vyuo wanavyosoma. Hali hii imebadiisha sana utumiaji wa lugha katika vyombo vya habari. Maneno mengi ya kigeni yanaingia katika vyombo vya habari kama ni athari ya utandawazi. Neno linalotumika Marekani hii leo, leo hii hii linadakwa na watangazaji wa vipindi vya radio na Tv, watumiaji mitandao ya jamii na pia waandishi wa magazeti. Kwavile nadharia za mawasiliano zinaonesha kuwa utamaduni hutoka katika nchi zenye maendeleo makubwa ya mawasiiano kwenda katika nchi zilizochini kimaendeleo vijana wetu hutawaliwa na utamaduni wa nje, hivyo matumizi ya maneno ya kigeni kutoka magharibi huzidi katika lugha ya Kiswahili. Kwa kuzingatia hali hizi Kiswahili hakiwezi kubaki kuwa kile cha zamani, lazima

kitakwenda na wakati na mabadiliko ya vijana wanaotumia lugha hiyo. Hali hii inajadiliwa kwa kina katika makala hii.

Kiswahili kama Rasilmali Muhimu ya Kuboresha Uchumi wa Afrika Mashariki

Clara Momanyi
Chuo Kikuu cha Kikatoliki Afrika Mashariki

clamona@yahoo.com

Kwa miongo mingi sasa, Kiswahili kimekuwa kikijadiliwa katika kumbi za kitaaluma, kielimu na hata katika makongamano ya kitaifa na kimataifa barani Afrika na kwingineko. Kwamba Kiswahili sasa ni lugha ya kimataifa ni ukweli usiopingika. Wenyeji wa Afrika Mashariki wana mchango mkubwa katika kukitandawazisha Kiswahili ulimwenguni. Kwa wengi, Kiswahili kimeweza kuwapa posho ya kujikimu na mtaji wa kujiendeleza kibinafsi. Hata hivyo, ipo haja sasa ya kujadili umuhimu wa lugha hii katika uchumi wa nchi za Afrika Mashariki. Historia imetufunza kwamba maendeleo mapana ya lugha inayotumiwa na wengi na juhudi za wenyeji wake kuisafi na kuisafirisha kwingineko ni mchakato aali wa kuikuza ili ichukue sura ya kimataifa. Aidha, ni mchakato wa kufaidi nchi yao pia kiuchumi. Kule kuisafirisha na kujenga taasisi ulimwenguni za kuweza kuifunza huku ikichukua nafasi kubwa katika mawanda ya elimu ni mbinu adhimu ya kuiwezesha nchi yao kuitumia kama kitega uchumi cha kuimarisha pato la nchi. Mifano ya makuzi ya lugha kama hizi ulimwenguni ni mingi. Je, ni mbinu zipi ambazo nchi za Afrika Mashariki zinaweza kuzindua ili kuboresha uchumi wao kwa kutumia Kiswahili? Ni mikakati ipi ambayo asasi za serikali na taasisi za elimu zinaweza kuimarisha ili kubaini ukweli kwamba Kiswahili ni dafina inayoweza kutumiwa kuimarisha hali za maisha ya jamii zao? Makala haya yanapigia darubini njia mbalimbali zinazoweza kutumiwa ili kubainisha Kiswahili kama rasilmali inayoweza kutumiwa na nchi za Afrika Mashariki kuboresha hali zao za kiuchumi.

Kiswahili Nchini Rwanda: Ufunguo wa Maendeleo Endelevu Katika Afrika ya Mashariki

Cyprien Niyomugabo
Chuo Kikuu cha Rwanda-Koleji ya Elimu (UR-CE)
niyomugabocyprien@gmail.mail.com

Kijiografia na kihistoria, Rwanda ni nchi ambayo, ipende isipende, haina budi kuhusiana na lugha ya Kiswahili. Jamii hii inapakana na nchi zinazokitumia sana Kiswahili. Kwa upande wa historia, ukoloni wa Kijerumani tangu mwaka wa 1892 hadi 1914, ulikiwezesha Kiswahili kuingia kiurahisi Rwanda, nchi ambayo wakati huo iliwekwa katika "Afrika Mashariki ya Wajerumani", ukanda uliokuwa na Kiswahili kama Lugha rasmi.Wakati mwingine, watu wengi hujiuliza swali la kutaka kujua nani aliyekuwa wa kwanza kuleta Kiswahili nchini Rwanda. Mtawala wa Kijerumani, mfanyabiashara wa Kiarabu, dini ya Kislamu na wamisionari wa Kizungu, nani ameleta au ametumia kwanza Kiswahili nchini Rwanda? Inaaminika kwamba, Kiswahili kama lugha rasmi iliingizwa Rwanda na utawala wa Kijerumani mwishoni mwa karne ya 19. Ndiyo sababu Kiswahili Rwanda kimepitia mihula mitatu muhimu: Kiswahili kama lugha tawala (1900-1929). Katika muhula huu ambao ni kipindi cha utawala wa Mjerumani kinachukuliwa kama muhula wa staha wa Kiswahili. Maadam, Mjerumani alikiteua Kiswahili kuwa lugha rasmi dhidi ya Kidachi na Kinyarwanda. Muhula uliofuatia ni kipindi cha Kiswahili usingizini (1929-1979). Mnamo mwaka

wa 1929, Wabelgiji walipiga marufuku matumizi ya Kiswahili kwa nia ya kufuta mabaki na athari za utawala wa Wajerumani na Kifaransa kikachukuwa nafasi ya Kiswahili, "lugha laanifu". Hali hii ya kutopatia thamani na hadhi Kiswahili iliendelea hadi 1979. Mhula wa tatu ni kuanzia mwaka 1979 hadi sasa ambao unatazamwa kama mhula wa mwamko mpya wa Kiswahili**.** Tarehe 24 Machi 1979, serikali za Rwanda na Tanzania zilitilia saini mkataba wa ushirikiano katika nyanja za elimu na utamaduni.Tanzania ikaitpatia Rwanda walimu na wataalamu wengine wa Kiswahili. Hiki ni kipindi cha urasimu mpya wa Kiswahili ambao kipeo chake kikawa tareahe 17 Oktoba 2017, wakati ambapo Rwanda imeiteua lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi pamoja na Kinyarwanda, Kiingereza na Kifaransa. Kwa hiyo makala hii inalengea kueleza maendeleo ya Kiswahili na mchango wake katika kufungulia Rwanda milango ya ushirikiano na nchi za Afrika ya Mashariki na ulimwengu mzima, Rwanda ikichukuwa Kiswahili kama mfungamano wa kikanda na maendeleo endelevu katika nyanja zote.

Ufunguo: Ufunguo wa maendeleo, Lugha ya Kiswahili, Rwanda, Afrika Mashariki, lugha rasmi, Mfungamano wa kikanda.

The Globalization of Kiswahili and the False Promise of English

Daniel Ochieng Orwenjo
The Technical University of Kenya
orwenjo@daad-alumni.de

There is no doubt that Kiswahili has gained ground as a language of choice by millions of people in East Africa and its neighbours. It has been transported to different parts of Africa and the West due to migration, both voluntary and as a consequence of ethnic wars, including the fight against colonialism and apartheid. Refugees from neighbouring countries learn Kiswahili during their short stay in Kenya or Tanzania and keep the language when they finally immigrate to England, the United States, or other western countries. This paper argues that the globalization of Kiswahili and the expansion of its domains of use beyond its traditional original role as a lingua franca is hinged on the false promise of English that East African states had upon attaining independence. Grounding its arguments on the notions of linguistic human rights and linguistic pluralism, the paper advocates for a radical shift in the language in education policy in East Africa and for an inclusion of other Kenyan languages including sheng as one of the languages of instruction and communication within Kenyan school classrooms.

Key Words: Multilingualism, Linguistic Human Rights, Linguistic Pluralism, Language in Education Policy

Tafauti ya Maana ya maneno kwa mujibu wa Utamaduni: Fasili za vidahizo katika *Kamusi la Kiswahili Fasaha* na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 3*

Daulat Abdalla Said
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanziabar,
na
Salma Omar Hamad
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

tsaidab@yahoo.com

Utamaduni wa jamii hutafautiana kutokana na mila, desturi, lugha, itikadi, imani, maadili pamoja na masuala yote ya mazoea ya jamii inayohusika na utamaduni huo. Tafauti za kiutamaduni zinaweza kuwepo baina ya nchi moja na nyengine, au baina ya kundi moja la watu na kundi jengine ndani ya nchi moja, hasa nchi inapokuwa kubwa, yenye watu wa makabila mengi kama ilivyo Tanzania. Aidha, kanuni za utungaji wa kamusi zinaeleza kuwa maana ya neno hutokana na maana ya kisemantiki pamoja na maana ya kiutamaduni. Makala hii ina lengo la kueleza tafauti ya maana ya maneno baina ya Tanzania bara na Zanzibar. Utafiti umechunguza tafauti hizo za maana kwa kutumia fasili za vidahizo katika *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (KKF) na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS). Kwa kutumia vidahizo vilivyofanana ambavyo vina maana tafauti zilizosababishwa na tafauti za kiutamaduni baina ya maeneo hayo, imebainika kwamba maana ya kidahizo ni njia moja inayoweza kuonesha tafauti ya utamaduni baina ya eneo moja na jengine linalozungumza lugha moja na ambalo linatafautiana katika baadhi ya vipengele vya kiutamaduni. Matarajio yetu ni kuwa makala hii itasaidia sana katika taaluma ya Semantiki na Leksikografia hasa katika uundaji wa majopo ya kutunga makamusi ya Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano kwa wazungumzaji wa Kiswahili wa maeneo tafauti.

Usasabaadaye katika hadithi fupi ya "Mazishi Yangu" iliyoandikwa na Ken Walibora katika mkusanyo wa *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine*

Daulat Abdalla Said
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanziabar

tsaidab@yahoo.com

"Ubunifu ni kuona yale ambayo hayapo na kuyafinyanga mpaka yawe kama yapo, kuyafanya yahisiwe, yasikike, na muhimu zaidi yaonekane. Uhalisia wa kibunifu unakuwa umechukua sura ya uhalisia halisi kiasi kwamba wasomaji watasema haya yalitukia au yalimtukia mwandishi." Ken Walibora anaithibisha kauli yake hii katika hadithi ya "Mazishi Yangu". Uisomapo hadithi hii unaweza kudai kuwa ni hadithi ya kitawasifu. Kinyume chake ni kuwa "Mazishi Yangu" ni hadithi fupi ya usasa ambayo ina sifa ya fasihi ya kimajaribio. "Mazishi Yangu" inaweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia mbalimbali za kisasa kama nadharia ya upokezi wa msomaji, udenguzi, muingiliano wa matini, ukoloni baadaye, umuundo, umuundoleo na usasabaadaye. Makala hii inakusudia kuchambua hadithi ya "Mazishi Yangu" kwa kutumia nadharia ya usasabaadaye katika kipengele cha lugha. Kwa kuwa Lugha ndio roho na mwili wa fasihi. Hivyo basi, usasabaadaye katika kazi za fasihi huundwa kutokana na lugha na pia lugha huaongozwa na usasabaadaye. Baadhi ya vipendele vya lugha ya usasabaadaye vitakavyochambuliwa katika makala hii ni uchanganyaji wa tanzu, muingiliano matini, uhalisiamazingaombwe, mchezo wa maneno na uvunjaji wa kanuni na kaida za uandishi. Kwa jumla makala hii itakuza au kuendeleza uhakiki wa utanzu huu wa hadithi fupi, ambao kwa kwa upeo wa uelewa wa mwandishi bado haijachambuliwa katika Kiswahili hususani kwa kutumia nadharia za kisasa za uhakiki.

Athari za lugha ya Kiswahili katika siasa nchini Kenya

Deborah Nanyama Amukowa
Chuo Kikuu cha Maseno

dnanyama@yahoo.com

Juhudi nyingi za kujenga taifa lenye maendeleo na kubuni nafasi za kazi haziwezi kufua dafu bila kushirikisha lugha. Uchangamano wa kiisimu nchini Kenya sambamba na hadhi iliyotokana na tangazo la kikatiba (2010) kwamba kiswahili ni lugha ya taifa na lugha ya kwanza rasmi, ni ishara ya uwezo uliotunikiwa lugha hii. Hali hii bila shaka itachangia pakubwa katika maendeleo ya nchi. Uwekaji sera ambayo itahakikisha maendeleo na uwezeshaji lugha katika kutimiza majukumu yake ya utambulisho wa kitaifa, kimatifa na utoaji huduma ni muhimu. Kutokana na upana wa kimatumizi katika nyanja mbalimbali Kiswahili kimefikia upeo wa kuwa na athari kubwa katika uwanja wa kisiasa nchini Kenya.

Historia fupi ya Kiswahili Nchini Burundi na Changamoto za kukiendeleza katika sekta mbalimbali za Maendeleo ya Kitaifa

Denis Bukuru
na
Lothaire Niyonkuru
Chuo Kikuu cha Burundi
dbukuru@gmail.com

Kiswahili ni mojawapo katika lugha nne muhimu zinazotumiwa nchini burundi, pamoja na Kirundi, Kifaransa, na Kiingereza. Kiswahili kiliingia Burundi kutoka pwani mwa Afrika Maashariki, mwishoni mwa karne ya 19, ikiletwa na wahubiri wa dini ya kiislamu pamoja na Wazanzibari waliokuwa wakifanya biashara ya watumwa. Kiswahili kilitia nanga sehemu za kandokando ya Ziwa Tanganyika na haswa katika mji wa Rumonge. Utawala wa kikoloni ulipoingia, Kiswahili kilitumika kama lugha ya mawasiliano baina ya watawala wa kizungu na wenyeji wa kirundi. Sera hiyo ilitumiwa na utawala wa kijerumani (1896-1916) na kibelgiji (1916-1962). Na kadri miji ilivyoendelea kukuwa Kiswahili kilitumika kama lugha ya mawasiliaano au *lingua franca* katika vituo visivyofuata mila na desturi za wenyeji. Baada ya uhuru, Kiswahili kilipigwa marufuku katika nyanja rasmi za serikali, na kilitumika katika nyanja zisizo rasmi kama biashara, na mawasiliano kati ya Warundi na wageni. Pamoja na hayo, kiswahili kilianza kufundishwa Chuo Kikuu cha Burundi miaka ya 1980. Baada ya Mkataba wa Amani wa Arusha (2000) kuwaruhusu wakimbizi wa kirundi kurudi nchini mwao, Kiswahili kilipata umuhimu zaidi, haswa baada ya Burundi kuingia Jumuia ya Afrika Mashariki na Kiswahili kuteuliwa kama lugha ya mawasiliayano katika nchi wanachama wa Jumuia hiyo. Hatimaye Kiswahili kilipewa nafasi katika Rasimu ya Sera ya Lugha nchini Burundi (2010).

Mchango wa Wamishonari Wakatoliki katika Kuendeleza Elimu ya Kiswahili Magharibi mwa Kenya baina ya 1931-1963.

Dismas Sibweche
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro
Sibwechedismas"yahoo.com

Licha ya Wamishonari Wakatoliki kutumia Kiswahili katika shughuli zao za kielimu na kidini na pia licha ya kujishughulisha na elimu katika viwango mbalimbali, juhudi zao za kukitumia na kukiendeleza Kiswahili hazijafanyiwa uchunguzi wa kina. Hali hii si ya kuridhisha hasa

ikizingatiwa kuwa ni kutokana na shughuli hizo mbalimbali ambapo msingi wa baadaye wa Kiswahili ulijengwa. Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu utafanywa kwa lengo la kutathmini mchango wa Wamishonari Wakatoliki katika maendeleo ya elimu ya Kiswahili katika eneo la Magharibi mwa Kenya baina ya 1930 – 1963. Utafiti uataongozwa kwa madhumuni yafuatayo: kuchunguza mchango wa Wamishonari Wakatoliki katika maendeleo ya elimu ya Kiswahili, kujadili hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Wamishonari Wakatoliki kuendeleza elimu ya Kiswahili na mwisho, kujadili changamoto zilizowakabili wamishonari hao katika kuendeleza elimu ya Kiswahili katika eneo la Magharibi mwa Kenya. Utafiti utaongozwa na nadharia ya Bosch D (1991) kuhusu Mabadiliko ya Dhana ya Thiolojia ya Misheni. Hitimisho la utafiti litakuwa kuwa Wakenya walichangamkia kujifunza na kutumia lugha za kienyeji kikiwemo Kiswahili siyo kwa minajili ya kutaka wapate hadhi kijamii na kiuchumi bali kwa sababu za umoja. Kwa upande mwingie Wakenya wajifunza Kiingereza kwa mapendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Matumizi ya Istilahi za Kiswahili katika Elimu. (sayansi-Isimu, biolojia na kemia)

Dorothée Nshimimana
Chuo Kikuu cha Burundi
nshimadot"yahoo.com

Makala hii itajadili matumizi ya istilahi za Kiswahili katika utundishaji wa masomo ya sayansi kama vile Isimu, Biolojia, Kemia na Fizikia. Makala itagawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao utafafanua baadhi ya maneno yaliyotumiwa katika mada hii. Pili, itazungumzia juu ya utumiaji wa istilahi za Kiswahili katika ufundishaji wa baadhi ya masomo ya sayansi. Tatu, itaelezea changamoto zilizopo katika utumiaji wa istilahi za Kiswahili katika kufundisha masomo ya sayansi kama vile Isimu, Biolojia, Kemia. Sehemu ya nne, itazungumzia juu ya dhima ya matumizi ya istilahi za Kiswahili katika masomo ya sayansi. Mwisho, kutatolewa hitimisho la mjadala ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya namna ya kuimarisha uundaji istilahi za kisayansi na matumizi yake kwa ajili ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kiswahili na Vyombo vya Habari kwa Umma

Elias Majambere
Chuo kikuu cha Ziwa Tanganyika (ULT)- Burundi

majambereelia@gmail.com

Kiswahili ni Lugha mojawapo ambayo zinatumiwa katika jumuia ya Afrika mashariki,kitaifa na kimataifa.kina umuhimu mkubwa kwa kuwa kinasaidia kwa kupasha habari mbali mbali kwa uma.jamii ya afrika mashariki inayo zungumza kiswahili inakitumia kwenye serikali,kampuni,viwandani,ofisini hata mashambani,bila kusahau kutumia lugha hiyo kwa kutangaza biashara yawo kwa kupitiya ruha hiyo.na ruha yaq kiswahili imekuwa suruhisho kwenye jamii kutokana na kwamba afrika mashariki wengi wawo ni ruha yawo mama.ndio maana vyombo vya habari vinakazi ya kutoa habari kwa uma na Kiswahili kimekuwa kifaa cha kutumika katika habari kwa kuwa kinatumiwa kutoa habari kwa uma. Kutokana manufaa ya

Kiswahili, jamii ya jumuiya yetu inapaswa kukipenda, kukikuza, kukipa nafasi yake kwa kukitumia kama ilivyo kukisambaza ki taifa na kimataifa pia duniani kote.Ili mpango huo iuamarike serikali, mashirika mbalimbali na taasisi mbalimbali vinachukua nafasi ya kwanza katika kuhimiza uiamara huo.

Kiswahili, Biashara na Kazi: Utaanzaje Kujiajiri na Utawezaje Kujikwamua Kiuchumi?

Elizabeth Godwin Mahenge
University of Dar es Salaam – Institute of Kiswahili Studies
lizmahenge@gmail.com

Kiswahili ni mtaji wa kufanyia biashara na vilevile ni kazi. Wapo watu mbalimbali wamejiajiri au wameajiriwa kupitia Kiswahili. Je, utaanzaje kujiajiri? Utawezaje kujikwamua kiuchumi? Makala haya yatachokoza mjadala na kujaribu kujibu maswali haya.

Ufasiri wa Habari za Kiswahili kwa Lugha-Ishara kwenye Televisheni ya KTN.

Ellen Otieno, Simala Inyani & John Habwe.
ellenotieno@gmail.com

Mada hii ilichaguliwa kwa sababu Lugha-Ishara (LI) na fasiri ni mbinu mahsusi za mawasiliano miongoni mwa watu wa jumuiya ya 'viziwi'. Wafasiri wa lugha ya wachache (k.m LI) hulazimika kufasiri taarifa nyingi kinadharia kutoka lugha zilizoimarika zaidi kiakademia (yaani, lugha za maongezi) hadi kwa LI. Mfasiri hufasiri kwa sababu anatarajia kuwa taarifa zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili zitawasilishwa na kueleweka na watu wenye matatizo ya kusikia. Tulichochewa na kuelewa kwetu kwamba mbinu ya ufasiri ni ya kimsingi katika ufahamu wa maana ya habari za Kiswahili zinazofasiriwa kwa LI kwenye televisheni (TV). Katika harakati za kufasiri habari za Kiswahili kwa kutumia LI wafasiri na watu wenye matatizo ya kusikia hukumbana na changamoto mbalimbali ambazo zitajadiliwa kwa undani katika makala haya. Huu ndio mkabala unaomhusisha msemaji/mfasiri pamoja na ishara zake, muktadha na msemewa/mfasiriwa ili kuchanganua maana. Tunaamini kuwa mfasiri ndiye hushughulikia dhana ya maana katika ukamilifu wake, ambapo vipengele vyote vinavyochangia upatikanaji wa maana huegemezwa. Dhana ya ufasiri wa habari za Kiswahili kwa kutumia LI kwenye TV haijatiliwa maanani sana na wataalamu wa fasiri nchini Kenya. Kwa sababu hii, uchanganuzi huu ulidhamiria kuibua hamu ya kiusomi ya kushughulikia ufasiri wa habari za Kiswahili kwa LI kwenye TV kama kipashio muhimu cha kimawasiliano kinachofaulisha mawasiliano kati ya watu wanaosikia na wasiosikia. Isitoshe, fasiri za habari za Kiswahili zinailenga LI kwenye televisheni ambayo haijashughulikiwa kwa undani kutokana na hadhi ya chini utanzu huu umepewa. Katika kuinua hadhi hii, tunaamini uchunguzi huu utachangia kuwahamasisha wataalamu kuumakinikia. Kwa kuongezea, stesheni ya TV tunayoishughulikia haijawahi kuhakikiwa kwa mujibu wa utenda kazi wa mfasiri kwenye televisheni. Matundura (2007) anadahili kuwa vyombo vya habari huweza kuwaathiri watu pakubwa, matumizi ya istilahi tofauti kuelezea dhana ileile na picha ndogo ya mfasiri kwenye skrini wakati mwingine huweza kuwakang'anya watazamaji (viziwi) wa habari hizo. Pana haja ya vyombo vya habari kuwaajiri wataalamu waliosomea taaluma ya fasiri na kurukebisha ukubwa wa picha ya mfasiri, la sivyo mawasiliano yatapotoshwa hasa tukichukulia

kwamba vyombo vya habari vina ushawishi mkubwa kwa umma ya watu wenye matatizo ya kusikia.

Kiswahili, Biashara na Kazi

Emmanuel Ndayisaba
Chuo kikuu cha Mwanga(Light University)
Emma.sneayndayi@gmail.com

Makala yangu inahusu umuhimu wa Lugha ya Kiswahili katika swala zima la Biashara na kazi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ikumbukwe kuwa lugha hii yenye asili ya Kibantu ilianza Pwani ya Afrika Mashariki na sasa imeenea katika nchi zote za maziwa makuu na duniani kote.Kiswahili kina umuhimu sana katika biashara hapa Afrika Mashariki maana ni Lugha ambayo ni rahisi sana kuongea na kuelewana kati ya mteja na muuzaji. Utamu wa Lugha hii unakuja pale ambapo maneno mengi yanafanana na maneno ya lugha za kibantu. Sambamba na hayo kiswahili pia ni Lugha ya Kimataifa kama zilivyo Lugha zingine kama vile kingereza, kifaransa na zinginezo, na ndio maana Jumuiaya ya Afrika Mashariki kwa kutambua umuhimu huo imepitisha mswaada wa kukifanya Kiswahili kuwa Lugha rasmi ya kikanda. Kumbe kupitia juhudi hizi na zinginezo zinazofanywa na wadau mbalimbali wa Kiswahili, zitawafanya wana jumuiya ya Afrika Mashariki kubobea katika lugha hii na hatimaye kupata urahisi wa kukitumia Kiswahili katika shughuli za maendeleo. Kwa mtazamo unaoonekana wazi ni kwamba Kiswahili kimekuja kuleta mabadiliko ya Biashara na kazi.

Kiswahili, Vyombo vya Habari na Mawasiliano kwa umma

Eric Niyongabo
Chuo Kikuu cha Burundi
ericngabo10@gmail.com

Katika jumuiya ya Afrika Mashariki, ni dhahiri kwamba yapo mabadiliko kadha wa kadha katika nyanja mbalimbali mathalani kiuchumi, kijamii, kielimu… Hiyo inatokana na uwepo na kazi ya vyombo vya habari na mawasiliano kwa umma. Vyombo hivyo ni muhimu sana katika kuelimisha jamii kwa namna moja au nyingine. Vyombo hivyo ni pamoja na : runinga, idhaa za redio, magazeti. Makala haya yana lengo la kudhihirisha kuwa lugha yetu Kiswahili inasaidia pakubwa katika kujenga jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia vyombo vya habari na mawasiliano kwa umma. Aidha, makala haya yatadhihirisha umuhimu na manufaa ya kiswahili hasa hasa katika vipindi mbalimbali vya idhaa za redio, runinga lakini pia katika machapisho ya badhii ya magazeti. Ijulikane kuwa vipindi hivyo vinathibitisha uwepo wa mabadiliko mazuri mathalani katika michezo ya kuigiza inayoonya jamii… au kwa njia ya ukuzaji wa elimu mathalani katika vipindi vya Kiswahili ambavyo vinapitishwa ili kusahihisha makosa madogo madogo ya kifonetiki na kimofolojia. Makala haya yatachambua kwa kina swala hilo. Kwa upande mwingine Wahenga walisema “hakuna msafara wa mamba usiokuwa na kenge” Kusema kwamba makala haya yatadhihirisha hali tofauti ya mabadiliko yasiyo mazuri katika baadhi ya nchi za Afrika mashariki ambazo hazijapiga hatua ndefu katika utumiaji wa Kiswahili katika vyombo vya habari na mawasiliano kwa umma, mfano thabiti ni upatikanaji za magazeti zinazochapishwa kwa kiswahili kwa nadra sana. Sehemu nyingine itazungumzia mabadiliko ya waandishi wa habari wanaochapisha magazeti yenye habari zenye elimu haba au za kupotosha, kubomoa jamii zetu

hasa kwa upande wa vijana na wanajamii wote kwa ujumla mathalani kuacha mila na desturi zetu na kugeukia mila na desturi za Magharibi hali ambayo inaonekana kuwa na msaada usiyofaa. Hatimaye zipo nchi ambazo baadhi ya raia wake wana fikra « potovu » wasemapo kuwa utumiaji wa Kiswahili katika vyombo vya habari na mawasiliano haufai na kusema bora Kiingereza, kifaransa… Makala haya yataonyesha hasara wazipatazo watu tuliowazungumzia hapo juu lakini pia makala haya yatatoa dira na mwelekeo kwa watu hao na kwa wanajumuiya wote kwa ujumla ili kukuza na kuelimisha umma.

Kiswahili, Vyombo vya Habari na Mawasiliano kwa Umma

Esther Chomba na Patrick Muhoni
South Eastern Kenya University
echomba@seku.ac.ke

Vyombo vya habari ni asasi muhimu sana katika kukuza na kueneza lugha yoyote ile, hasa katika enzi hii ya utandawazi. Vyombo hivi ni kama vile idhaa za redio, televisheni na magazeti. Katika mataifa yetu kuna vyombo vingi vya habari vinavyotoa huduma anuwai kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya wateja wao. Katika karne hii ya 21, vyombo vya habari vimelazimika kuhakikisha kuwa wateja wao wananufaika kutokana na huduma mbalimbali ambazo hutolewa kila kukicha. Huduma hizo hujumuisha kuwajuza, kuwafundisha, kuwaburudisha na hata kuelimisha wanajamii kwa namna moja au nyingine. Makala hii itatathmini jinsi vyombo vya habari vitasaidia katika kuleta manadiliko katika jumuiya ya Afrika mashariki kupitia lugha ya Kiswahili kwa kuboresha mawasiliano kwa umma. Vyombo vya habari huru na vyenye nguvu ni kichocheo katika mapambano dhidi ya umaskini na ujinga katika nchi yoyote ile zikiwemo nchi za Afrika Mashariki. Katika wakati huu, kuna ushahidi wa kutosha kuwa Afrika haihitaji kitu kingine chochote kile bora zaidi ya mfumo wa vyombo vya habari wa kidemokrasia zaidi kwa ajili ya maendeleo na ukuaji wa kiuchumi.Sekta ya habari ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi – hususan nchi maskini kama zilivyo nchi za Afrika Mashariki. Vyombo vya habari hufichua vitendo vinavyokwamiza maendeleo ya nchi kama vile ufisadi, rushwa katika utawala, matumizi mabaya ya madaraka, huduma duni kwa wananchi na ubadhirifu wa mali za umma. Inakisiwa kuwa takriban zaidi ya watu milioni mia moja wanaizungumza lugha ya Kiswahili katika eneo hili la Afrika Mashariki. Kutokana na idadi hii ni wazi kuwa Kiswahili kinaweza kutumiwa pakubwa katika kuleta maendeleo sio tu Barani Afrika bali pia ulimwenguni kote.

Ukuu wa ufanisi wa Kiswahili katika ujenzi wa Demokrasia Afrika Mashariki

Fokas Nchimbi
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa

fokasnchimbi@gmail.com

Makala hii inajaribu kueleza ukuu wa ufanisi wa lugha ya Kiswahili kama chombo shirikishi na zalifu zaidi kwa maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na mustakabali wake. Inaonesha uakisi wa ukuu wa ufanisi wa lugha ya Kiswahili kwa kuangazia matumizi na mchango wake katika ujenzi wa demokrasia katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ujenzi wa demokrasia, ambao katika makala hii, umechukuliwa- kama katika mataifa mengine yote duniani-

kuwa ni mchakato jumuishi na endelevu, hauwezi kufanikiwa katika hatua zozote pasi na matumizi ya makusudi ya lugha yenye ufaafu na ufanisi stahiki katika eneo hili la Afrika ya Mashariki, yaani lugha ya Kiswahili. Ujenzi wa demokrasia ni mchakato usio na ukomo ambao unaruhusu kuwepo kwa mfumo wa kitaasisi ambapo jamii za kirai zinaweza kupata fursa pana ya uwakilishi na ushiriki wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja. Katika makala hii tunadai kuwa ujenzi wa demokrasia na ushiriki wa Wanaafrika Mashariki katika michakato ya kisiasa unaweza kufikiwa kwa kiwango kikubwa, zalishi na endelevu ikiwa kutakuwapo na hatua za makusudi za kujenga mazingira wezeshi ya matumizi ya Kiswahili katika shughuli zote za kisiasa na hususan katika juhudi za pamoja za udemokrasishaji. Hakuna lugha katika Jumuiya ya Wanaafrika Mashariki inayoweza kuwaunganisha na kuchapuza maendeleo yetu kama Kiswahili. Ukuu wa ufanisi wa lugha ya Kiswahili katika ujenzi wa demokrasia katika Afrika Mashariki unatokana na kukua, kuenea, kujulikana kwake kwa Wanaafrika Mashariki wengi na kuhusiana kwake na lugha nyingi za watu wa makabila karibu yote katika Eneo la Maziwa Makuu. Kwa hiyo, watu wengi wa Afrika Mashariki wanaweza kushiriki kwa ufanisi na kunufaika zaidi na ujenzi wa demokrasia katika jumuiya yao.

Kuleta Mabadiliko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kiswahili

Fulgence Nintunze
Chakukibu.kisw@gmail.com

Mada hii inahusu namna Jumuiya ya Afrika Mashariki inavyoweza kukua na kubadilika kupitia utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Maendeleo hivyo kupitia lugha ya kiswahili elimuni na hasa nchini Burundi, tunajaribu kutathmini athari za mabadiliko haya ya mitaala ya Kiswahili nchini burundi katika viwango vyote na jinsi gani inavyoweza kusaidia katika maendeleo endelevu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuna mabadiliko mengi yametokea katika elimu. Mabadiliko hayo hasa yamejikita katika mitaala mbalimbali kwa jumla na katika mitaala ya Kiswahili kibayana. Kwa hivyo, patokeapo mabadiliko yoyote ya kimitaala katika elimu vivyo hivyo panatokea mabadiliko ama chanya au hasi. Kwa hiyo maada hii inajaribu kutafuta utatuzi wa changamoto mbalimbali zitokeapo.

Mada hii inajaribu kutathmini jinsi mabadiliko kuhusiana na elimu yanaweza kushawishi maendeleo endelevu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia lugha ya Kiswahili. Pia na jinsi inavyoweza kuathiri wadau katika Kiswahili mchakato wa maendeleo hasa katika elimu, katika jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla na hasa nchini Burundi. Kisha kuona jinsi Kiswahili kinaweza kuwa lugha ya uwazi na maendeleo endelevu kwa watu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuijadili maada ya « Kiswahili, Elimu na Mabadiliko » ikisiri hii inajaribu pia kutoa picha ya Afrika Mashariki ya leo na kesho kimaendeleo endelevu kupitia lugha ya Kiswahili.

Kiswahili, Ufungamano wa Kikanda na Maendeleo

Fidélité Niyokwizigira
Chuo kikuu cha Ziwa Tanganyika (ULT)

Kiswahili ni lugha ya kibantu kwa sababu maneno yake mengi yanatokana lugha mama za jamii kubwa za Kiafrika ambazo hujulikana kama " bantu" Kiswahili ni lugha rasmi katika nchi za Tanzania na Kenya, pia ni lugha ya pili au tatu kwa Burundi, Uganda na Rwanda.Hata hivyo nchi kama Zambia, Congo, Burundi na Rwanda zimekuwa na muamko mkubwa wa kiswahili. Kiswahili ni lugha mojawapo inayosaidia kuimarisha umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

ambapo kimekuwa ni chombo kikubwa na cha msingi wa maendeleo ya mila na desturi za wana Afrika Mashariki ndani na nje ya Afrika.Tukishikamana na kudumisha undugu kupitia chombo hiki kinachotuunganisha na kutupia mbali tofauti zetu , bila shaka tunaweza kuteketeza matatizo yote na kila chochote kinachotukosesha usawa na kujenga uhusiano bora na wakudumu. Hakuna tunachoweza kufikilia bila usalama na utulivu, hivyo kukusanyika pamoja kwa lengo moja ni kitu muhimu, hapo kutakuweko ; kudumisha amani na usalama, kuimarisha mahusiano ya Kimataifa, kufungua mipaka katika nchi za eneo hilo la Afrika Mashariki. Mfungamano huu unaleta pia maendeleo kwa kufanya Afrika iongeze mashindano ya Kiuchumi , kufanya mikakati na misingi mbalimbali ya kuendeleza uchumi , kujenga ajira kwa vijana na ukuaji wa miji kwa haraka, miundombinu bora hata punguzo katika kubadirishana biashara ndani ya Afrika Mashariki.

Kiswahili, Elimu na Mabadiliko

Génie Claudia Irankunda
Chuo kikuu cha Maziwa makuu (UG L)- Burundi

Lugha ya Kiswahili ni kiungo muhimu sana katika maendeleo ya nchi za Afrika Mashariki hasa katika uchumi, elimu siasa, utamaduni na biashara.Hivi sasa kuna muamuko wa Kiswahili katika za Afrika Mashariki, katika elimu na mabadiliko ya nchi hizo . Mwamko ambao sasa umo zaidi miongoni mwa vijana wa sekondari na wale wa vyuoni kwa mfano ; Chama cha wanafunzi wa Kiswahili vyuo vikuu vya Afrika Mashariki(CHAWAKAMA),kinawakutanisha wanafunzi katika kuendeleza mijadala kuhusu kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki. Fasihi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki inamchango mkubwa katika swala zima la mabadiliko ya ukanda huu. Swala hili pia linaakisi mabadiliko katika jamii hususan katika elimu, uchumi na siasa. Kimekuwepo na hamu ya watu wengi zaidi kutaka kusoma kiswahili, hali hii imesababababisha kuwepo kwa shule nyingi za Serikali na vyuo vingi ambao wanasoma Kiswahili hata pale ambapo hakuna walimu au vifaa na miundo mbinu ya kutosha. Elimu ya Kiswahili itasababisha mabadiliko katika nchi za Afrika Mashariki kupata fursa za kufanya mambo mengi tofauti ambayo anajenga maisha ikwemo biashara, elimu, afya, sanaa siasa na uchumi. Kupitia lugha ya Kiswahili inaonekana kuwa lugha hiyo inaleta mabadiliko mengi katika nchi za Afrika Mashariki zaidi ya asilimia 80 ikiwemo kuwezesha wadau kujipatia ajira katika sekta mbalimbali, kukuza vipaji na kuuza au kununua kupitia elimu hiyo ya kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki.

Nafasi ya Kiswahili na Uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

George Mrikaria

Lugha ni chombo cha mawasiliano katika jamii. Nchi waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekuwa na historia ya muda mrefu wa ushirikiano kiutamaduni, kijamii na kiuchumi.

Ushirikiano huu ulifikia kuwa na Kamati moja ya kusimamia lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki wakati zikiwa makoloni ya Mwingereza na hata baada ya kupata uhuru Kamati hii iliendelea kusimamia masuala ya uendelezaji wa lugha ya Kiswahili. Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipovunjika mwaka 1977 kukawa hakuna ushirikiano baina ya nchi zilizokuwa wanachama wa jumuiya hiyo na suala la lugha likabaki kuwa la kila nchi kuendesha kwa namna yake. Kufika mwaka 1999 nchi hizi ziliona kuna umuhimu wa kurudiana na kuamua kufufua Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya Jumuiya hii kufufuliwa nchi nyingine tatu ziliomba na kukubaliwa kujiunga na Jumuiya hiyo ambazo ni Rwanda, Burundi na Sudani Kusini. Kwa sasa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaundwa na nchi sita. Makala haya yanakusudia kujadili kuenea kwa Kiswahili na nafasi na mchango wake katika kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kusoma na Kuandika kutaikuza na kuidumisha Sekta ya Afya

Gertrude Joseph
Gettyj2004@yahoo.co.uk

Lugha ndiyo msingi wa kujifunza kwani bila lugha huwezi kuelewa wala kuwasiliana na wanadamu wenzako. Kiswahili ndiyo lugha inayotumiwa na jamii ya Waswahili. Hivyo basi kusoma na kuandika Kiswahili, ndiyo roho ya utambuzi wa hazina iliyojificha katika maandishi anayokutana nayo mgonjwa au mtu anayemhudumia mgonjwa. Umuhimu wa kujua kusoma na kuandika haupingiki katika jamii yoyote iwayo. Kujua kusoma na kuandika ndiko kunakotupatia maarifa yote yanayomzunguka mwanadamu. Hali inaweza kuwa tete ikitokea kwa bahati mbaya mmojwapo kati ya mgonjwa au anayemhudumia mgonjwa akashindwa kufuatilia kwa makini maelezo na maelekezo yote yanayotolewa na wahudumu wa afya kuhusu dawa na matibabu ya mgonjwa. Endapo makosa yatafanyika, basi kuna hatari ya mgonjwa kupata athari mbaya kutokana na kutokufuata vizuri maelekezo yaliyotolewa. Athari hizi zinaweza kusababisha matokeo mabaya kama vile kupata mzio, ulemavu au hata kifo.Suala la kujua kusoma na kuandika halina budi kutiliwa mkazo katika jamii ili kujiepusha na madhara ambayo yanaweza kutokea.

Mafanikio ya matumizi ya Kiswahili kufundishia Elimu ya Juu: Mtazamo Mpya

Gervas A. Kawonga
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa
(Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)
kawongag@yahoo.com

Tafiti zilizopo hadi sasa kuhusu nafasi ya Kiswahili kwenye elimu zinaakisi mawazo ya kimapokeo kwamba lugha ya Kiingereza pekee ndiyo inayotumika kufundishia elimu ya juu. Ushahidi wa sera ya lugha nchini Tanzania unaakisi hali hiyo. Wakati kukiwa na uelewa huo wa kimapokeo, elimu ya juu inaanzia shahada ya kwanza. Katika ngazi hiyo ya elimu wanafunzi wanajifunza isimu na fasihi kama maarifa ya kimajumui kwa Kiswahili. Kwa kuzingatia mtazamo huo Kiswahili kinabadili nafasi yake kutoka kufundishwa kama somo na kuwa lugha ya kufundishia. Katika ngazi ya shahada ya umahiri na uzamivu wahitimu wa shahada hizo kwa Kiswahili wanalazimika kufanya utafiti kama mchakato wa kisayansi ili kuibua maarifa mapya katika Nyanja ama za isimu na fasihi au masuala mtambuka ikiwa ni pamoja na lugha katika elimu. Huu ni mtazamo mpya unaolenga kuonesha nafasi halisi ya lugha ya Kiswahili katika elimu. Ni mtazamo unaolenga kuifahamisha jamii nafasi ya Kiswahili katika elimu ya juu na uwezo wake

katika kumudu dhana mbalimbali za kifalsafa kuhusiana na masula ya lugha, fasihi, isimu na elimu. Makala haya yanakusudia kuchunguza kiwango ambacho Kiswahili kimefanikiwa kutumika kama lugha ya kufundishia elimu ya juu katika taaluma za Kiswahili. Katika kufanya hivyo masuala ya urari wa istilahi utachunguzwa kama eneo muhimu la lugha ya kitaaluma. Hatua madhubuti za kuchukua kwa ajili ya kuboresha zaidi hasa kwa wakati huu ambapo sio tu katika Tanzania Kiswahili kimetangazwa kisera kutumika katika ngazi zote za elimu, bali pia kinachukua sura ya utangamano ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vyuo vingi vya Afrika Mashariki vinafundisha taaluma za Kiswahili kwa Kiswahili. Wito wa makala haya ni kuanzisha na au kuimarisha kitengo cha istilahi ili kuwa na msawazo wa matumizi yenye nidhamu katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha na kama lugha ya kufundishia isimu na fasihi katika elimu ya juu.

Tafsiri Nyenzo ya Kiswahili kuelekea Utangamani na Maendeleo Endelevu ya Afrika Mashariki

Hadija Jilala
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
dijaah@yahoo.com/hadija.jilala@out.ac.ac.tz

Maendeleo ya kijamii kiuchumi, kisiasa na kisayansi yametokana na juhudi za ugunduzi wa watu wa kale na kusambaa kupitia tafsiri. Ugunduzi na ustaarabu wa Wamisri ulioigwa na Wayunani hatimaye kuwa chimbuko la ustaarabu wa Ulaya katika karne ya 19 uliwafikia kupitia mbinu ya tafsiri. Maarifa na elimu ya ulimwengu yalihama na kuenea duniani kupitia tafsiri ambayo ilitumika kama daraja la kufanikisha mawasiliano na kuunganisha jamii lugha tofauti. Kwa hiyo, tafsiri ilisaidia kuhamisha utamaduni wa jamii moja kwenda jamii nyingine. Maendeleo ya Afrika Mashariki hayawezi kupatikana bila kuwa na lugha inayoziunganisha nchi hizo kwa sababu kihistoria nchi hizo zina usuli tofauti wa lugha. Kwa hiyo, Afrika Mashariki inahitaji lugha itakayoziunganisha nchi wanachama ili kurahisisha maelewano, mawasiliano na kuziunganisha nchi Wanachama kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Kwa minajili hiyo, ili kufikia utangamani na maendeleo endelevu ya Afrika Mashariki makala hii inaitazama tafsiri kuwa nyenzo ya lugha ya Kiswahili katika kufikia jukumu hilo. Swali la msingi ni namna gani tafsiri inaweza kutumika katika kufikia adhma hiyo? Je, tafsiri ina nafasi gani katika kufikia utangamani na maendeleo endelevu ya Afrika Mashariki? Je, tafsiri ina dhima gani katika kuwaunganisha wana Afrika Mashariki? Kwa hiyo, makala hii inahusu tafsiri nyenzo ya Kiswahili kuelekea utangamani na maendeleo endelevu ya Afrika Mashariki. Lengo la makala hii ni kuchunguza na kujadili ni kwa jinsi gani tafsiri inaweza kutumika kama nyenzo ya kufikia utangamani na maendeleo endelevu ya Afrika Mashariki. Makala hii inajadili kuwa, lugha ya Kiswahili inaweza kutumia tafsiri kama nyenzo ya kusaidia katika utangamani na maendeleo endelevu ya Afrika Mashariki.

Ukiushi wa Matumizi ya Kiswahili Sanifu katika Vyombo vya Habari

Hamad Khamis Juma & Zainab Ali Iddi
hamadkhjuma@gmail.com na zeinabiddi@yahoo.com

Makala hii inakusudia kuchunguza makosa ya ukiukaji wa matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu katika vyombo vya habari, sababu za makosa hayo na kuonesha jinsi yanavyoathiri maendeleo na ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Data ya makala hii kwa kiasi kikubwa imekusanywa maktabani kwa kupitia magazeti na rekodi za vipindi vya redio na runinga. Pia, kuna data iliyokusanywa uwandani

ambapo wazungumzaji wa Kiswahili sanifu wamesailiwa juu ya matumizi sahihi ya Kiswahili katika vyombo vya habari. Uchambuzi na uchanganuzi wa data umeongozwa na mkabala wa kinadharia wa *Uchanganuzi Kina Kilongo* ulioasisiwa na Fairclough (1994). Msingi mkuu wa nadharia hii ni kuonesha uhusiano uliopo kati ya matumizi ya lugha na miktadha mbalimbali ya mazungumzo. Hivyo basi, tumeitumia nadharia hii kuchanganua makosa ya ukiukaji wa matumizi sahihi kulingana na miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha. Katika uchunguzi huu tumebaini kuwa wanahabari hufanya makosa ya aina mbili; *kisarufi* na *kimantiki* ambapo hufanya makosa ya kisarufi kama vile, matumizi ya msamiati usio sanifu, kuiga miundo ya Kiingereza na kubadili na kuchanganya msimbo. Makosa ya kimantiki ambayo hufanywa na wanahabari ni pamoja na matumizi msamiati visivyo, kutozingatia muktadha wa mazungumzo, kutozingatia kanuni za lugha. Kwa mujibu wa uchunguzi wetu makosa hayo hutokana na sababu kadhaa kama vile, ukosefu wa ujuzi wa matumizi ya lugha, kasumba juu ya matumizi ya lugha, kupuuza matumizi sahihi ya maneno, na kadhalika. Kwa kuhitimisha tunaweza kusema kuwa makosa hayo kiasi kikubwa huathiri maendeleo na ukuaji wa lugha ya Kiswahili.

Baadhi ya Makosa ya Kisarufi na kimsamiati wayafanyayo Wanahabari nchini Kenya

Hamisi Babusa
Chuo Kikuu cha Kenyatta
hobabusa@gmail.com

Vyombo vya habari vinachangia pakubwa sana katika kuendeleza au kudidimiza Kiswahili ulimwenguni. Wanahabari huwa wana majukumu mawili makuu. Jukumu dhahiri ni kuwasilisha matukio jinsi yanavyotukia na jukumu la pili ambalo ni fiche ni la kuwa walimu wa lugha kwani watu wengi walio na umilisi tofauti wa lugha hujifunza lugha kutoka kwa wanahabari. Wanahabari basi wana jukumu la kuhakikisha kuwa wana umilisi wa kiwango cha juu cha lugha ya Kiswahili wanapotoa matangazo au kuandika habari zao. Katika makala haya, tutajadili baaadhi ya makosa ya kisarufi na kimsamiati wanayofanya wanahabari nchini Kenya.

Nafasi ya Kiswahili katika Biashara na Kazi Afrika Mashariki

Hanah Chaga Mwaliwa
Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi
hannah.mwaliwa@uonbi.ac.ke; **mwaliwach@yahoo.com**

Kiswahili ni lingua franka inayotumika miongoni mwa wazungumzaji wengi katika jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni lugha ambayo hutumika na watu wa tabaka na jamii tofautitofauti katika eneo la Afrika Mashariki. Kwa wengi, Kiswahili ni lugha ya pili kama si ya kwanza. Hii ni kwa sababu ya mazingira mwafaka ya lugha yaliopo katika eneo hili. Nchini Kenya kwa mfano, Kiswahili ni lugha rasmi na lugha ya taifa. Zaidi ya hayo, lugha hii hufunzwa kama somo la lazima, jambo ambalo pia limechangia kuenea na kukua kwa matumizi yake. Hali hii iaonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika shughuli za kibiashara na kikazi miongoni mwa wakazi wa eneo la Afrika Mashariki. Makala hii inaangazia nafasi na umuhimu wa matumizi ya Kiswahili katika kufanikisha shughuli za kibiashara na kazini miongoni mwa wazungumzaji wa Afrika Mashariki. Tutatumia muktadha wa nchi za Kenya, Tanzania na Uganda kuonyesha uwezo wa Kiswahili katika kufanikisha shughuli za biashara na kazi. Tunaazimia kujua sababu gani zinafanya wafanyibiashara kupendelea kutumia Kiswahili kuliko lugha zingine kwenye shughuli zao. Pia tunanuia kuonyesha mchango wa Kiswahili katika upanuzi na ufanisi wa shughuli za wafanyakazi

na wafanyabiashara katika eneo la Afrika Mashariki. Aidha, tutatalii mchango wa lugha hii katika kuendeleza na kufanikisha maendeleo ya jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mabadiliko Ya Kidiskosi Katika Magazeti Ya Kiswahili-Mtazamo Wa Nadharia Ya Isimu-Media

Hezekiel Gikambi Peter
Catholic University of East Africa
hezekielgikambi@gmail.com

Miongoni mwa mambo ambayo yamekuwa yakibadilika badilika katika tasnia ya utoaji habari katika magazeti na tovuti za habari kwa Kiswahili nchini Kenya, kama ilivyo kote ulimwenguni, ni jinsi ya kuziandaa na kuzisambaza matini za habari hizo, yaani teknolojia ya uzalisha na usambazaji. Huku mabadiliko haya yakiwa yameshughulikiwa kiusomi katika lugha za kimagharibi kama vile Kiingereza na Kijerumani, bado hatujapata tafiti nyingi zilizoegemea katika matini za Kiswahili na uzalishwaji wake. Makala hii haijifungi na mabadiliko hayo ya kiteknolojia ila itajaribu kuangalia jinsi mabadiliko mengine tofauti kabisa, ya kidiskosi, yamedhihirika katika matini za habari za Kiswahili baada ya miongo sita kutoka miaka ya 1960, 1970, 1980, 1990, 2000, na kutoka 2010 hadi wa sasa. Utafiti huu umechanganua matini kutoka kwa gazeti la Taifa Teo lililoanza kuchapishwa tangia 1958 kila siku hadi wa leo nchini Kenya na kuchanganua jinsi diskosi imekuwa ikibadilika badilika baada ya mwongo mmoja au iwapo hakika imekuwa ikibadilika. Data hii imekusanywa kutumia sampuli elekezi za habari za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kibiashara, kispoti na kielimu. Nakala za sampuli za magazeti zitabadilishwa kuwa matini kavu kwa kutumia programu za Ubuntu/Linux na kujenga kongoo za aina hizo. Sampuli za kongoo hizo zitachanganuliwa kupitia vichanganuzi kongoo vya **TextStat 1.51** na **AntConc3.4.3** ili kupata sifa za kilugha kama ujirani wa maneno (collocations) upatano (concordances) na mara ya utokeji wa maneno (frequency lists) zinazoweza kuelezea diskosi tawala katika kipindi fulani na kulinganisha na kipindi kifuatacho. Zaidi ya kongoo kutakuwa na data itakayotokana na mahojiano na wataalamu wateule waliowahi na hata wanaofanyia kazi chapisho linalochunguzwa. Uchanganuzi huu wa diskosi umeegemezwa katika misingi ya Nadharia ya kisasa ya Isimu-Media (***Media Linguistics Theory***) inayochukulia matini za vyombo vya habari kuwa ni zao na mchakato wa kijamii unaotumia lugha katika kueleza na kuakisi hali halisi ya jamii hiyo katika wakati fulani.

Kiswahili kama wenzo wa kuimarisha Maarifa ya Kisayansi kwa ajili ya kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Isaac Ipara Odeo
Chuo Kikuu cha Kibabii , Bungoma. Kenya
iodeo@kibu.ac.ke/iparaodeo@yahoo.com

Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zina changamoto nyingi kama ilivyobainika kwa kushindwa kwao kutekeleza baadhi ya malengo ya maendeleo ya milenia. Hata hivyo, mazingira ya sasa yanadhihirisha nafasi na uwezekano wa mafanikio. Licha ya ukweli kwamba nchi hizi zina utajiri wa maarifa jadi na pia zinafahamika kwa ubunifu wa hali ya juu, hakuna viashiria vya athari chanya ya ufanisi. Hii ni kwa sababu sayansi ya kisasa haiwafikii watu kwa kuwa imefumbatwa katika lugha ya kigeni wasioifahamu huku ubunifu na uvumbuzi wa watu vijijini ukishindwa kuhusishwa kwenye sayansi na teknolojia ya kisasa kwani unatekelezwa kwa

lugha zisizo za ‘kisayansi’. Kiswahili ina uwezo wa kubadilisha hali kwa kuwa ni lugha yenye hadhi na matumizi mapana ikilinganishwa na lugha nyingine za asili. Katika makala haya, tutajadili mikakati ya kukiwezesha Kiswahili kuimarisha nafasi yake kama wenzo wa kuweza kutatua changamoto za maendeleo zinazokabili Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha tutapendekeza mbinu za kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu kupitia Kiswahili.

Changamoto za ufundishaji wa kiswahili kama lugha ya pili kwa wageni nchini kenya

Jacktone O. Onyango
Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
tony60jacko@yahoo.com

Katiba ya Kenya (2010) imetambua Kiswahili kama lugha ya taifa na pia lugha rasmi. Majukumu haya mawili yameiwezesha lugha ya Kiswahili kutumiwa na watu wengi zaidi nchini Kenya kuliko lugha nyingine yoyote. Kwa hiyo wageni wanaozuru Kenya kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwingineko wanalazimika kujifunza Kiswahili ili kutangamana kikamilifu na wenyeji katika shughuli mbalimbali za maisha. Hata hivyo, ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wageni nchini Kenya hukumbwa na changamoto mbalimbali ambazo huwazuia baadhi ya wageni hao kuimudu kikamilifu lugha hii na hivyo basi kutoweza kutangamana vizuri na wenyeji. Kwa hiyo, lengo la makala hii ni kujadili changamoto zinazowakumba wageni wanaojifunza lugha hii pamoja na hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto hizo na hivyo basi kuchangia utangamano katika Afrika Mashariki.

Kutoka Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki hadi Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki: Kamisheni inajifunza nini?

Jacktone Onyango
na
Ireri Mbaabu
Chuo Kikuu cha Kenyatta.
tony60jacko@yahoo.com na irerimbaabu@yahoo.com

Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iliyosanifisha Kiswahili kuanzia mwaka 1930 hadi 1964 iliweka msingi imara wa ukuzaji na uenezaji wa lugha ya Kiswahili katika Afrika Mashariki na ulimwengu kwa jumla. Katika utekelezaji wa shughuli zake, Kamati hii ilifanikiwa kutimiza baadhi ya malengo yake lakini pia ilikumbwa na matatizo mbalimbali ambayo yalisababisha kuvunjika kwa Kamati hiyo. Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki inaweza kufanikiwa katika utekelezaji wa shughuli zake iwapo itajifunza mambo mbalimbali kutokana na mafanikio na matatizo yaliyoikumba Kamati. Hivyo basi, lengo la makala hii ni kujadili mambo muhimu ambayo Kamisheni inaweza kujifunza kutokana na shughuli za Kamati na hivyo basi kusaidia katika ukuzaji na uenezaji wa lugha hii.

Uhakiki wa Maudhui katika Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Jacob Mwita
Chuo Kikuu cha Rongo – Kenya
Jacobmwita12@gmail.com

Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umetiliwa maanani sana hasa katika shughuli rasmi za Jumuiya kama zilivyo nyimbo za mataifa mbalimbali. Wimbo huu huimbwa wakati wa ufunguzi rasmi wa vikao vya Jumuiya. Isitoshe, kwa mfano nchini Kenya, wimbo wa Jumuiya umeanza kuimbwa hata mashuleni kwenye gwaride wakati wa kupandisha bendera. Hatua hii ni muhimu katika kukuza na kudumisha umoja na uzalendo miongoni mwa wanajumuiya. Makala hii inahakiki maudhui makuu yanayobainishwa na wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuonyesha mchango wake katika kuleta mabadiliko yanayodhamiriwa na jumuiya hii. Ninatumia Uchanganuzi Matini kuhakiki maudhui katika beti zote na kiitikio.

Kiswahili katika Kampeni za kisiasa Nchini Kenya: Tathmini ya Matumizi ya Kiswahili miongoni mwa Wagombea Urais

James Marwa Mwita
Chuo Kikuu cha Rongo
Jamesmwita1984@yahoo.com

Kiswahili nchini Kenya ni lugha ya taifa na vilevile lugha rasmi. Lugha ya Kiswahili inatumika katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kama lugha ya taifa, Kiswahili hutumika kuwaunganisha wananchi wa makabila na tamaduni mbalimbali. Watu mbalimbali huelewana kwa urahisi kwa kutumia Kiswahili kuwasiliana. Wakoloni walilitambua hili na kukipinga Kiswahili kwa sababu kilikuwa kinawaleta pamoja wakenya na kuwawezesha kupigania uhuru wao, jambo ambalo wakoloni hawakulipendelea. Kwa hivyo matumizi ya Kiswahili katika siasa nchini Kenya yamekuwepo toka enzi za kikoloni. Baada ya uhuru, Rais wa kwanza wa Kenya, Mzee Jomo Kenyatta, alitambulika kwa matumizi yake ya Kiswahili alipokuwa akiwasiliana na wananchi. Mpaka wa leo, viongozi mbalimbali wa kisiasa nchini wanatumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana na kuwasilisha sera zao kwa wananchi. Katika makala hii, tunapania kutathmini jinsi wagombea mbalimbali wa kiti cha urais nchini Kenya mwaka 2017 wanaitumia lugha hii katika kuwasilisha sera zao kwa wananchi wakati wa kampeni. Wagombea watakaotathminiwa ni wale watakaokuwa wameteuliwa rasmi na vyama vyao vya kisiasa kupeperusha bendera za vyama hivyo. Tunapania kuchanganua matumizi ya Kiswahili ya wagombea hawa tangu wakati watakapoteuliwa rasmi na vyama vyao hadi wakati wa uchaguzi wa kitaifa utakaofanyika Agosti 8, 2017. Kichocheo cha utafiti huu ni ukweli kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na vilevile lugha rasmi nchini Kenya. Aidha Kiswahili ni lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo basi, rais akiwa ishara mojawapo ya umoja wa kitaifa, anafaa kuwa kielelezo cha kile kinachowaunganisha wananchi wote, yaani, lugha ya taifa.

Udhalilishaji wa Mwanamke katika Mitandao ya Kijamii: Tathmini ya Ukurasa wa *"Robert Mugabe Quotes"* katika mtandao wa *Facebook*.

James Marwa Mwita
Chuo Kikuu cha Rongo
Jamesmwita1984@yahoo.com

Mitandao ya kijamii imekua kutokana na maendeleo ya kiteknolojia. Kwa mwongo mmoja uliopita, mitandao mingi ya kijamii, pamoja na programu tumizi zinazoiwezesha mitandao hii kufanya kazi barabara imebuniwa. Mifano ya mitandao maarufu ya kijamii ni *Facebook, Twitter*,

WhatsApp, Instagram, WeChat n.k. Mitandao hii inasaidia sana katika usambazaji habari kwa urahisi, kwa gharama ya chini sana na kwa uwazi zaidi. Kutokana na huu urahisi na uwazi wa usambazaji habari, jamii zimepata kuendelea na kuimarika. Japo hii mitandao ina faida kemkem, kwa upande mwingine imechangia katika kuporomosha maadili katika jamii. Ni dhahiri kuwa mitandao hii imetumiwa kwa njia isiyo sawa na ndiyo maana nchi mbalimbali, zikiwemo zile za Afrika Mashariki, zimetunga sheria kuongoza matumizi yake. Miongoni mwa maswala ya kimaadili ambayo yanalengwa na hizi sheria katika mitandao ya kijamii ni pamoja ulaghai, ugaidi, ponografia, uchochezi, udhalilishaji wa kijinsia n.k. Katika makala hii, tunalenga kutafitia jinsi mitandao ya kijamii inachangia kuporomosha maadili hususani jinsi inavyotumika kumdhalilisha mwanamke na juhudi zake katika jamii. Kwa kuwa hii mitandao ni mipana zaidi, tutajikita katika *Facebook* hususani ukurasa wa "*Robert Mugabe Quotes"* kwa ajili ya data ya makala hii. Tutamia mbinu ya uchanganuzi matini ili kuyapambanua na kuyaeleza matokeo yetu. Aidha, makala hii itapendekeza njia za kupunguza udhalilishaji huu wa kijinsia.

Kiswahili kama kichocheo cha Maendeleo ya Kiuchumi katika nchi za Afrika Mashariki

James Omari Ontieri
Chuo Kikuu cha Maasai Mara
jontieri@gmail.com

Kiswahili ni lugha ya matumizi mapana katika ukanda wa Afrika Mashariki. Katika juhudi ya kujiendeleza kiuchumi, jamii mbalimbali zinahitaji lugha ya mawasiliano ambayo inaeleweka kwa wahusika kama njia kuu ya kuafikia maendeleo. Aidha, kunahitajika juhudi za kimakusudi miongoni mwa wananchi za kuimarisha viwango vyao katika matumizi ya Kiswahili ili kuitumia lugha hiyo katika kushirikisha mipango anuwai ya kimaendeleo katika nyanja za kiuchumi. Ni kutokana na hali hii ambapo makala hii inalenga kuonyesha mchango wa Kiswahili katika suala zima la maendeleo ya kiuchumi katika nchi za Afrika Mashariki. Data ya makala hii itakusanywa kupitia kwa upekuzi wa maandishi yanayohusu mchango wa lugha katika maendeleo ya jamii pamoja na yale yanayohusu hali halisi ya maendeleo ya kiuchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha wanaopanga sera za maendeleo ya kiuchumi katika nchi husika kwa kuonyesha namna lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumiwa katika kuinua hali ya maendeleo ya kiuchumi. Pia wahusika mbalimbali wanaoshiriki katika shughuli za kiuchumi watawekewa wazi umuhimu wa Kiswahili katika kuboresha juhudi zao za kujiimarisha kimapato.

Some Aspects of Kiswahili Phonology that lack Prominence in Phonology Books and in the classroom

Jane Akinyi Ngala Oduor
University of Nairobi
oduorjane@yahoo.com

Kiswahili just as any language of the world is unique. Its uniqueness as a language is seen in many areas of language study. In this paper the main concern is in its phonology, an area that deals with the systematic organization of its speech sounds. There are many aspects of Kiswahili phonology that are either left out or not handled conclusively in Kiswahili phonology text books. In Kiswahili

phonology classrooms, it is therefore possible that they are not given the prominence they deserve because lecturers also tend to rely on the text books available in the market when preparing lecture notes. The uniqueness of Kiswahili as a language should be brought out clearly in the teaching of its phonology. For this reason, this paper attempts to point out the areas of concern, showing how they should be handled in text books as well as in teaching. Some of the areas which are not handled adequately and yet they help to show the uniqueness of Kiswahili phonology are in the analysis of some sound segments, the analysis of long as compared to short vowels, the analysis of some of its syllables, phonetic versus phonemic transcription and, finally, the emerging dialects of Kiswahili as far as their pronunciation aspects are concerned. The ultimate aim of the paper is to contribute towards an in depth analysis of Kiswahili that will help to lift it up in terms of research, innovation and teaching to the level of analysis attained for the other big languages of the world.

Kufuwawa kwa Miiko na Mabadiliko ya Tabia Nchi: Mifano kutoka katika Jamii ya Wabungu

Joachim A N Kisanji, Yusta Mganga, Grace C Mkomwa na Said Omary Said
jachim_kisanji@yahoo.com

Miiko hujitokeza katika jamii mbalimbali ili kusaidia jamii hizo katika kukabiliana na changamoto za kimaumbile na kuhakikisha ustawi wa vizazi vyake dhidi ya mabadiliko ya mara kwa mara ya kimaumbile. Miiko ni jitihada za wanajamii kujitafutia njia au majawabu ya kukabiliana na tishio la kuangamia kwao. Jamii ya Wabungu imekuwa na miiko ambayo tunainasibisha na changamoto za utunzaji wa mazingira ya jamii yao. Tunamakinia miiko inayohusiana na ustawi wa ardhi na rutuba, vyanzo vya maji na utunzaji misitu na hali ya hewa. Tunajenga hoja kuwa kuna mlandano baina ya kujitokeza kwa uharibifu wa mazingira katika jamii ya Wabungu katika kipindi hiki, hususani suala la mmonyoko wa ardhi, kukauka kwa chemchemu na kuongezeka kwa joto na tishio la jangwa katika jamii hiyo na kufuwawa kwa miiko ya kisanaajadiya ya Kibungu. Matokeo ya hojaji kwa wanajamii wa Wakibungu juu ya aina mbalimbali ya miiko iliyokuweko kabla ya kipindi cha utandawazi katika miaka 80 na 90, inaonyesha ni kwa kiasi gani kupotea kwa miiko hiyo kumechangia katika uharibifu wa mazingira. Mchango wa Makala haya ni kubaini mchango wa sanaajaadiya katika kuchangiya mapambano dhidi ya utunzaji wa mazingira katika jamii za Kiafrika ambazo bado zinafuata na kuthamini mifumo ya nguvu za kijaala (miungu, mizimu na miiko).

Changamoto za Ufundishaji wa Kiswahili Afrika Mashariki: Suala la Uainishaji Nomino kuwili

John Habwe
Chuo Kikuu cha Nairobi
johnhabwe@gmail.com

Karatasi hii inachunguza suala la ufundishaji na uendelezaji wa Kiswahili Sanifu katika ukanda wa Afrika Mashariki. Inajikita kwenye suala la ufundishaji wa nomino kwa kuzingatia hoja kwamba kuna nomino zinazobadili ngeli zake kama sifa ya mabadiliko yake na kuna zile nomino ambazo huanishwa katika makundi mawili au hata zaidi.Karatasi hii inahoji kwamba waalimu na wataalamu wengi wamekuwa wamelifumbia macho suala hili na hivyo kusababisha mvutano

katika uanishaji wa nomino husika.Karatasi hii inadai kuwa kutozingatia kwa huu uainishaji kuwili vyuoni na katika vyombo vya utangazaji katika shule kunainyima lugha Sanifu ya Kiswahili nafasi ya kukua na kuwa na utajiri katika sarufi yake.

Methali za Kiswahili katika Uelezi na Uelekezi wa Demokrasia

Joseph Nyehita Maitaria
Chuo Kikuu cha Karatina
nyehitam@yahoo.com

Makala haya yanafafanua Methali za Kiswahili katika uelezaji na uelekezaji kuhusu suala la demokrasia katika matifa ya Afrika Mashariki. Methali hizi zinazotokana na jamii za Afrika Mashariki ambapo baadhi zimetafsiriwa na zimejumuishwa katika hazina iliopo. Hivyo, ni kitambulisho muhimu cha utamaduni wa wenyeji. Kabla ya maajilio ya wakoloni, kumekuwepo na kauli asilia za kitamaduni zilizoashiria demokrasia katika jamii ingawa kwa sura tofauti. Hapa Afrika Mashariki (kwa wakati wa sasa), utandawazi umezidi kutamalaki na umeathiri mielekeo ya watu kuhusu suala la demokrasia. Katika mawasiliano ya kijamii, methali za Kiswahili zimekuwa zikitumiwa kuwa nyenzo inayochochea usaili na tafakari kuhusu masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kimatumizi, unuwai wake umejikita katika tamathali za usemi ambapo hubainisha itikadi, falsafa ya watu kuhusu utamaduni wao. Isitoshe, methali hizo zinaweza kuwa vilelelezo vya kuelekezana, kuelimishana katika masuala ya siasa na uongozi katika jamii. Katika miaka ya 1960 (hasa baada ya uhuru) hadi wakati wa sasa, mataifa ya Afrika Mashariki yamekuwa yanajitahidi kuhusisha umma katika masuala ya uongozi. Hata hivyo, maono ya watu yamebadilika mno kuhusu masuala ya kisiasa kutokana na athari ya utandawazi ambapo wananchi wamekuwa wakisaili uhusika wao katika uongozi wa mataifa yao. Katika kiwango cha mtu binafsi na jamii, kumeshuhudiwa kutoridhishwa kuhusu suala la demokrasia. Umma wa vijijini umepewa nafasi finyu wa uhamasishwaji na uhusika katika masuala ya siasa na demokrasia; kwa sababu, hawafikiwi kwa lugha wanayoielewa. Swali hapa ni: mhimili ya demokrasia unaweza kuwasilishwa na kujadiliwa kwa namna inayoeleweka hasa kwa umma mpana katika mataifa ya Afrika Mashariki? Makala haya yanaangazia namna methali za Kiswahili zinavyoweza kuwa kurunzi ya kiharakati na kielekezaji cha jamii kuhusu masuala ya demokrasia. Aidha, makala haya yatazingatia taifa la Kenya kama mfano na itapendekezwa namna methali teule za Kiswahili zinavyoweza kutumiwa zaidi katika kukabiliana na kuepuka vizingiti vya mwafaka wa demokrasia kwa wakati wa sasa.

Wosia wa Shaaban Robert kwa Vijana wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka *Barua za Shaaban Robert*

Judith Kidigu Mwavali
Chuo Kikuu cha Kisii – Kisumu

Makala hii inarejelea *Barua za Shaaban Robert* na kueleza wosia wa mwandishi kwa ndugu yake mdogo Yusuf Ulenge. Ikichukulia mhusika Ulenge kuwa mwakilishi wa vijana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, makala inahoji kwamba Shaaban Robert anatoa mwongozo muhimu kuhusu elimu na maisha kwa ujumla. Makala inashikilia msimamo kwamba *Barua za Shaaban Robert* zina mafunzo muafaka kwa vijana ambao ndio msingi muhimu katika kujenga Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyo thabiti.

Kiswahili kama Lugha ya Maendeleo ya Afrika

Kabange Mukala Ernest
Chuo kikuu ca Lubumbashi/DRC
ernestkabange@gmail.com

Mabadiliko ya tabia nchi, yanaonekana kuwa jambo muhimu linaalo ongeza magumu juu ya umaskini kwenyi inchi za kiafrika. Tangu myaka mingi hivi, mataifa kadha ya kiafrika yanashiriki kwenyi kongamano za kidunia nzima ao za kiafrika, kufikiri juu ya kuona iwezikanayo ili watu wote waelewe kwa ginsi mabadiliko ya tabia nchi yanaangamiza kabisa na kudumu mpaka yaharibu maisha ya binaadamu. Kwenyi kongamano hizo, elimu zimetolewa na mipango imekamatwa kuusu kila mtu mahali anapoishi na kwa kila kaazi anapofanya, ajuwe ya kwamba anaweza, katika mabadiliko mazuri ya tabia yake, kuponyesha afrika na dunia nzima kwa asara hiyo. Lakini magumu ni kujuwa namna gani ujuzi huo na mipango hiyo zitafikia na kuwelewanika kwa watu wote kwani katika nchi za kiafrika, watu wengi ni wale ambao hawajuwi lugha za kigeni hizo wandishi wengi wanatumia, na wengi tena zaidi ni wale nao hawajuwi ata kusoma na kwandika. Nao Walimu watakaopeleleza na kuwafundisha kwa ajili ya jambo hilo, hawajuwi lugha mama za kila elfu za makabila jumuiya ya Afrika. Ni hapo matumizi ya kiswahili, yataweza kusaidia lengo ilo kwani kiswahili tangu zamani, kimesemewa, japo umbalimbali, na watu wengi kwenyi eneo kubwa la Afrika (Manessy, G., 1963) na kimeingia mpaka vijijini kikigeuka fazi nyingi kuwa lugha mama ya makabila tofauti (Kabange, M., 2014).

Maneno muhimu : tabia nchi, kongamano, mabadiliko, ujuzi, kupeleleza, lugha mama

Lubumbashi Swahili versus Swahili Sanifu: Linguistic Break and Regional Integration and Development

Kasombo Tshibanda Michaël
University of Lubumbashi/DRC
michelkasombo@gmail.com

Sociolinguistic and political factors can lead to a linguistic break into a sole language then make it split into different languages and prevent its speakers from socio-cultural and siocio-economical integration. Among these factors we can list the lack of permanent contact between speakers, the influence of neighboring languages, the lack of coherent linguistic policy, polycentric standardization, etc. Beyond a mere contrastive Swahili sketch centred concern, this paper intends to show that the Lubumbashi Swahili (LS) in particular and the Democratic Republic of the Congo Swahili in general slowly stands as a different language as opposed to the Swahili Sanifu (SS) mainly promoted in Tanzania and in Kenya. Dialogue between a Congolese and a Tanzanian or a Kenyan often leads to a deaf-and-dumb dialogue. Such a situation proves to be unfavourable to the regional integration and development. Based on field data collected in Lubumbashi, an extending urban society facing cross sociolinguistic challanges, the paper aims at pointing out linguistic diversity as one among brakes to the regional integration and development. The paper is divided into three main parts. The first one is a contrastive sketch of the LS aiming at providing a small idea of what this dialect ressembles actually as to oppose it to the SS at phonological, morpho-syntactic, lexical and prosodic levels. The second part is devoted to sociolinguistic and

political factors that cause the Kiswahili language split into opaque dialects tending toward different languages. The third part provides practical solutions intended to promote the future of the Swahili language then help the regional integration and development be boosted.

Key words : Lubumbashi Swahili, Swahili Sanifu, contrastive sketch, sociolinguistic and political factors, language split, deaf-and-dumb dialogue, regional integration and development, future of the Swahili language.

Dhima ya Vyombo vya Habari katika Kukikuza Kiswahili

Ken Walibora
Mtafiti wa Kujitegemea
kwwalibora@gmail.com

Katika karne ya 21 wanadamu wamepiga hatua kubwa sana katika maendeleo ya teknohama, maendeleo yanayotamanisha sawia na kuzuzua. Vyombo vya habari vilivyozoeleka kwa miaka na mikaka, kama vile magazeti, majarida, redio na runinga vinachuana na mtandao wa intaneti, na majukwaa ya kijamii kama vile *Facebook, Twitter, Netflix, Youtube,* na *Instangram* katika kinyang'anyiro kikali cha kuwania hadhira. Kwa watu wengi kinyang'anyiro hiki kilizuka ghafula bin vuu kama nyangumi katika ardhi kavu--bila kutarajiwa wala kutabiriwa kabla ya kujiri kwa nyenzo hizi mpya za kurushia na kusambazia habari, burudani na maarifa. Vyombo hivi sasa vimelazimika kujumuisha mitandao hii katika kuwasilisha habari, burudani na maarifa. Ilmuradi siku hizi unaweza kutazama kipindi cha machale cha Churchill Live cha runinga ya Kenya iitwayo NTV popote duniani wakati wowote kupitia kwa tarakilishi, kipakatalishi au simu ya kiganjani. Aidha Unaweza kusikiliza Idhaa ya Kiswahili ya BBC au idhaa ya Kiswahili ya Radio Deutsche Welle (DW) kwenye tarakalishi, kipakatalishi, au simu ya kiganjani katika mseto wa njia za mawasiliano ulioletwa na mapindukizi katika teknohama ukiwa popote duniani wakati wowote. Hata hivyo, tunapaswa kujisaili: Je, nini hasa hali na nafasi ya Kiswahili katika maendeleo haya au tuseme mtafuruku huu wa kiteknohama? Je, Vyombo vya habari vina dhima gani katika kukiendeleza, kukikuza na 'kukifagilia' Kiswahili katika enzi hii? Je, ni vizingiti vipi vinavyovikabili vyombo vya habari katika utekelezaji wa dhima hizi? Je, vizingiti hivi vinaweza kukiukwaje? Makala hii inajaribu kuyajibu maswali haya na mengine kama haya kwa kuchanganua utendaji wa vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili kama wenzo wa kujielezea, si hoja kama vina makao yake makuu maeneo ya ndani au nje ya mipaka ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu: Kiswahili na Uwajibikaji wa Asasi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kimani Njogu
Twaweza Communications, Nairobi
Kimani.njogu@gmail.com

Malengo ya Maendeleo Endelevu (MAMAE) yaliidhinishwa na Umoja wa Mataifa ili kupunguza totauti kubwa za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kimazingira na kiteknolojia duniani. Utekelezaji wa Malengo hayo kumi na saba yatajitaji ushikirishaji wa serikali na wananchi wa mataifa yote. Starkey (2002) amedai kuwa jumuiya zenye wingi-lugha yanapaswa kuunda na kutekeleza sera za

lugha zinazotilia maanani miktadha ya mataifa wanachama. Kwa sababu Jumuiya ya Afrika Mashariki imesheheni wingi-lugha itakuwa haina budi kuzingatia fursa na changamoto zitakazotokana na hali hii. Ili 'sauti' ya kila serikali na mwananchi isikike, itakuwa muhimu kuwa na mawasiliano madhubuti katika viwango mbalimbali kupitia lugha na mitambo inayofaa kwa walengwa. Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) imetambua Kiswahili kuwa lugha ya matumizi mapana katika ukanda huu. Kwa hivyo, lugha hii ni uti wa mgongo katika ufikiaji wa maendeleo endelevu. Makala hii inajikita katika utekelezaji wa lengo la 16 la MAMAE katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na nafasi ya Kiswahili. Tunajadili namna Kiswahili kitakavyochangia katika ujenzi wa asasi madhubuti. Ili kuleta amani, kuimarisha ushiriki wa umma katika harakati za maendeleo na kujenga jamii zinaongozwa na sheria na haki.

Tathmini ya Lugha ya Kiswahili katika Kutimiza Lengo la Maendeleo Endelevu la Elimu Bora Miongoni mwa Nchi Teule za Afrika Mashariki

Leonard Chacha Mwita na Anjejo Mark Odawo
Chuo Kikuu cha Kenyatta na Chuo Kikuu cha Rongo
chachamwita8@yahoo.com na odawomark14@gmail.com

Baada ya nchi za Afrika Mashariki kupata uhuru kutoka kwa wakoloni, lugha za wakoloni hao ziliendelea kutumika kama lugha rasmi katika nchi hizo. Lugha hizi zimechukuliwa kuwa ni lugha za kimataifa kwa sababu ya upana wa matumizi yake. Lugha ya Kiswahili inatumiwa, japo kwa viwangi vinavyotofautiana, katika nchi zote za Afrika Mashariki. Mbali na lugha hizo za kikoloni na ile ya Kiswahili, pia kuna lugha nyingine za wenyeji wa Afrika Mashariki zinazotumiwa na makundi ya jamii mbalimbali katika nchi hizi. Suala la maendeleo endelevu, hususan katika kitengo cha elimu, linarejelea lugha zinazotumiwa katika mafunzo shuleni na hivyo na linaingiliana na lile la haki za kiisimu ambazo zinalindwa na mikataba ya kimataifa. Makala hii inaangazia mashindano yaliyopo kati ya makundi matatu hayo ya lugha kuhusu lugha inayopaswa kutumiwa katika mafunzo shuleni na lugha ambayo kwa kweli hutumiwa. Ni lugha ipi inayo nafasi bora ya kuwainua watu wa Afrika Mashariki kielimu ikiwa itatumiwa kufunzia masomo yote shuleni? Nadharia itakayotumiwa kuelekeza utafiti huu ni ile ya ubeberu wa kiisimu. Kimsingi, nadharia hii inazungumzia hali ambapo wazungumzaji wa lugha wanalazimishiwa matumizi ya lugha nyingine isiyo 'yao'. Mifano itakayotumiwa katika makala hii itatolewa katika nchi za Kenya na Tanzania (na Zanzibar).

Kiswahili na Utangamano wa Afrika Mashariki

Levis Dotto Niyonkuru
Chuo kikuu cha Burundi

Makala yangu itaanisha mchango wa Lugha pendwa ya Kiswahili katika kuleta umoja na utangamano wa Afrika Mashariki. Ni ukweli usiopingika kuwa lugha yoyote ile ni kiungo muhimu hasa katika swala zima la mawasiliano. Lugha ya Kiswahili kama lingua franka ina mchango mkubwa katika kuleta utangamano wa wana Afrika Mashariki. Sambamba na hayo Kiswahili kimeendelea kutuunganisha wana Afrika kupitia utanzu wa fasihi simulizi

na andishi . tanzu ibuka ya muziki hasa wa kizazi kipya imekuwa mnato wa aina yake miongoni mwa vijana mwa vijana hapa Afrika Mashariki. Muziki kutoka Tanzania, Uganda hutolewa katika nchi zote za ukanda huu na bila kusahau zile za Burundi na Rwanda ambazo zimekuwa chachu inayo akisi mazingira mazuri ya Afrika yetu. Kama wahenga walivyosema, mwenye macho haambiwi tazama, ni ukweli usiopingika kuwa Kiswahili kinaendelea kuwaunganisha wana jamii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika nyanja mbalimbali kama vile uchumi, mawasiliano na hata katika shughuli nyingine nyingi. Hivyo mada hii itatathimini mchango wa Kiswahili katika umoja na utangamano wa Afrika Mashariki.

Mapendekezo katika kukuza na kuendeleza Lugha ya Kiswahili Nchini Burundi kufuatana na mpango maalum wa Akadema ya Lugha za Kiafrika

Lothaïre Niyonkuro
Chuo Kikuu cha Burundi
lothniyonk@yahoo.fr/lothniyonk2@gmail.com

Madhumuni ya kwanza ya makala hii ni kufafanua mazingira ya kisiasa, kijamii na kiutamaduni ambamo juhudi zakttkuza na kuendelezalugha ya Kiswahili zinafanyika nchini Burundi. Baada ya kueleza mpango maalum wa kuendeleza lugba za Kiafrika uliobuniwa na Akademia ya Lugha zaKiafrika (ACALAN), tunakumbusha misimamo ya kisiasa ya.Burundi kuhusu matumizi rasmi ya lugha za Kiafrika, yaani Kirundi na Kiswahili, kufuatana na mikataba ya kimataifa (Umoja wa Afrika) na ya kikanda (Jumuiya ya Afrika Mashariki), pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Burundi. Tunatoa pia maoni na mapendekezo katika kukuza na kuendeleza Kiswahili. Mapendekezo hayo yanalenga taasisi husika kwa ngazi mbalimbali, ama za kitaifa, za kikanda, au za kimataifa.

Mchango wa Kiswahili katika kuendeleza Biashara na Kazi Nchini Uganda

Lubuuka Yunusu
Chuo kikuu cha Kyambogo
lubuukayunusu@gmail.com

Uganda ni nchi inayopatikana Magharibi mwa eneo la Afrika Mashariki. Inazungukwa na nchi zifuatazo; Kenya upande wa Mashariki, Tanzania, Rwanda na Burundi upande wa Kusini, DRC upande wa magharibi na Sudan kusini upande wa kaskazini. Uganda ina watu milioni 40, makabila na lugha zaidi ya 50. Uganda ni nchi iliyo na utegemezi wa kimlishano na nchi jirani za Afrika Mashariki ambazo zinatuzunguka. Nchi hizi zinatumia Kiswahili kama lugha ya Kuwasiliana. Shughuli za kibiashara na kazi ni nguzo muhimu ya kuimarisha muungano wa Afrika Mashariki na kuhakikisha maendeleo ya watu chini ya muungano. Makala hii itabainisha mchango wa matumizi ya Kiswahili katika kuendeleza biashara na kazi nchini Uganda na Afrika mashariki kwa jumla. Malengo mahsusi ni kuchunguza jinsi matumizi ya Kiswahili nchini Uganda yameathiri biashara na kazi; Kuchunguza mitazamo ya Wanauganda kuhusu matumizi ya Kiswahili katika shughuli za kibiashara, Kuchunguza nafasi ya Kiswahili katika kuendeleza shughuli za kibiashara na kazi nchini Uganda na kupendekeza mikakati ya kuimarisha matumizi ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano nchini Uganda. Swala hili ni muhimu kwa sababu kulingana na Itifaki ya muungano wa Afrika Mashariki kifungu 137 Kiswahili ni lugha inayofaa kukuzwa, kuendelezwa na kutumiwa kama lugha ya eneo la Afrika Mashariki. Katiba ya nchi ya Uganda ya 1995 kama ilivyorekebishwa 2005 kifungu 6(2), lugha ya Kiswahili inatambulika kama lugha rasmi ya pili nchini Uganda. Uganda kama moja wapo wa nchi sita zinazounda muungano wa Afrika Mashariki

kisera inafaa kuendeleza lugha ya Kiswahili katika nyanja zote yaani kijamii, kiuchumi na kisiasa. Huu utakuwa utafiti wa maktaba ambao umechochewa na hali na hadhi ya Kiswahili nchini Uganda.

Fasihi ya Kiswahili na Uwajibikaji wa Vijana Barani Afrika

Magdaline Wafula
Chuo Kikuu cha Moi
mnwafula@gmail.com

Imesekana kuwa vijana ndio viongozi wa kesho na kwamba asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Misemo hii inashadidia ukweli kuwa kizazi kizee kina wajibu wa kukielimisha na kukiadilisha kizazi kichanga ili kukipokeza majukumu ya kukuza na kuendeleza jamii. Japo vijana wakilinganishwa na wazee au watu 'waliokomaa' huenda wasiwe na uwezo na tajriba ya kutosha kushika hatamu za uongozi katika nyanja mbalimbali katika jamii, kizazi kichanga hakina budi kuwajibika na kuwa katika mustari wa mbele kuendesha asasi za kijamii. Hali sivyo ilivyo katika nchi nyingi barani Afrika. Kizazi kizee licha ya kuwa kinakonga, kimeendelea kung'ang'ania uongozi badala ya kuwapisha vijana ili wapate fursa ya kukuza vipawa vyao.Vijana wanasatahili kuwezeshwa mapema iwezekanavyo ndipo wapate kutoa mchango wao kuleta maendeleo endelevu barani Afrika. Njia mojawapo ya kukiwezesha kizazi kichanga ni kukihami na elimu na mafunzo mwafaka ndipo kichukue hatamu za uongozi kingali na nguvu na kutoa huduma faafu na kulinyanyua bara la Afrika kimaendeleo. Makala haya yanadai kuwa fasihi ya Kiswahili kama mojawapo ya somo linalofunzwa shuleni na vyuoni lina nafasi kubwa ya kuleta mabadiliko miongoni mwa umma. Hii ni kwa sababu mojawapo ya dhima ya fasihi ni kuieleimisha jamii. Fasihi ni miongoni mwa nyenzo kuu za kukiwajibisha kizazi kichanga kuwa viongozi wa sasa na wa kesho. Kwa vile mazoezi huvyaza mazoea, ni kwa vipi kizazi kizee barani Afrika kinawazoesha vijana kumudu kunga za uongozi kama zinavyomulikwa katika fasihi ya Kiswahili? Kwa kuangazia kazi teule zinazofundishwa na kutahiniwa katika shule za Sekondari nchini Kenya, makala haya yanatathmini namna kizazi kizee kama mama mlezi kinatekeleza wajibu wake wa kukihami kizazi kichanga na maarifa pamoja na ujuzi ili kipate kuwajibika na kudumisha maendeleo endelevu katika Afrika Mashariki.

Kiswahili katika Vyombo vya Habari

Marcel KALUNGA MWELA UBI
Université de Lubumbashi/ DRC
markalunga@yahoo.com

Miongoni mwa vyombo vya habari kuna: Majarida, Magazeti, Redio, Televisheni na hata Simu za mkononi. Redio zinaweza kutofautishwa kutokana na maeneo yanayolengwa : Redio za Kitaifa zinawalenga watumizi wa Kiswahili katika nchi zinamopatikana. Walengwa wa Redio za kimataifa ni watu wote ulimwenguni ambako lugha hii hueleweka. Mada yetu inahusika na Kiswahili katika Redio za kimataifa. Siku hizi, matumizi ya Kiswahili kwenye redio hizi yanazidi kupanuka. Hakika matangazo ya Kiswahili hupeperushwa kutoka mabara manne: Marekani(Sauti ya Amerika), Ulaya (BBC, RFI, Sauti ya Ujerumani , Redio Vatican) Afrika (Channel Africa, Redio Cairo) Asia (Redio Teheran, Redio Cairo, Redio Beijing, Redio Pakistan). Mtazamo wangu

kuhusu matumizi ya Kiswahili katika redio za kimataifa una pande mbili: wa kwanza ni wa kuridhisha , na wa pili unazusha matatizo kadhaa.

I.Wa kuridhisha

Kutokana na uwezo wake maalum wa kutangaza moja kwa moja na bila kuchelewa matukio mbalimbali yanayoufikia ulimwengu huu, Kiswahili kinajipatia nafasi ya heshima miongoni mwa lugha nyingine zote za kimataifa.

Ni hivi, kwa mtu anayeelewa vema Kiswahili , hakuna tena haja ya kungoja matangazo ya Kifaransa au ya Kiingereza ili kujulishwa ni habari kubwa za kimataifa

II.Je kinatatiza ?

Kuna katika Kiswahili cha redio za kimataifa maneno na miundo kadhaa yasiyoeleweka vizuri na watumiaji wa kawaida wa kiswahili. Ni hivi, baadhi yao wanajiona kama wametiwa kando na matangazo hayo . Ingawa sifa zake ,Kiswahili hiki kinabidi ujuzi maalumu kwa kueleweka barabara .

Lakini matumizi yake katika vyombo vya habari vya kimataifa yanabaisha ukubwa wa lugha hii ambayo kila mara inajitahidi kuenda na wakati. Basi, ni kwetu sisi wasikilizi na wapendwa wa kiswahili kijikaza kufuata hatua zake.

Kiswahili, Siasa na Demokrasia: **Mintarafu ya Uganda**

Masereka Levi Kahaika
Chuo Kikuu cha Makerere
maserekalevi@yahoo.com

Suala mojawapo linalohitaji kushughulikiwa nchini Uganda linahusu suala la siasa na Demokrasia. Wananchi wa nchi yoyote ile Uganda ikiwemo, inapofikia masuala ya siasa, wanafaa kushiriki katika shughuli za uamuzi kuhusu masuala yanayoikumba nchi yao. Ili raia waweze kutumia uhuru wao wa uamuzi, wanahitajika kupewa nafasi za kutoa maoni yao kimajadiliano kwa kutumia lugha inayoeleweka kwa wote. Kidemokrasia, kila raia anafaa apewa uhuru wa kushirika katika kuamua juu ya mfumo unaonuia kuendesha serikali iliyochaguliwa kwa manufaa ya watu. Matumizi ya Kiswahili nchini Tanzania na Kenya imewapa raia wa nchi hizo uwezo wa kuelewa masuala ya kisiasa na kidmokrasia. Mbali na kuwa Uganda ni nchi mojawapo ya nchi zilizomo katika jumuiya ya Afrika mashariki ambako Kiswahili ndiyo lugha ya mawasiliano, matumizi ya lugha ya Kiswahili kisiasa na kidomokrasia kama ilivyo katika nchi ya Kenya na Tanzania ni finyu mno. Shughuli nyingi za kisiasa na kidemokrasia nchini Uganda huendelezwa kwa Kiingereza au hata lugha nyingine za kikabila. Pamoja na wingi wa lugha za kikabila na kutoelewana kimawasiliano kwa sababu ya tofauti za lugha, kumekuwepo vita vya ubaguzi na vya kisiasa ambavyo hutishia uhuru demokrasia na usalama wa nchi. Inajulikana kote kuwa Uganda hutuma wabunge katika bunge la jumuiya ya Afrika mashariki ambako Kiswahili kinafaa kutumiwa. Makala hii inanuia kujibu na kutoa suluhisho katika maswali kama; je hali hii itaendelea hivyo mpaka lini, ni kipi kinachofaa kufanyika ili Kiswahili kitumiwe katika masuala ya kisiasa na kidemokrasia nchini Uganda? Ni shughuli ipi itakayofanywa ili kila mwanauganda na viongozi watumie Kiswahili katika masuala ya kisiasa na kidemokrasia?. Ni watu gani wanaofaa kushirikishwa katika kutatua

shida hii na je ukamilifu wa shughuli hii utasaidiaje kuweka wazi umuhimu wa Kiswahili kisiasa na kidemokrasia mintarafu ya Uganda?

Ulinganishi wa Mtindo wa Lugha ya Kifasihi baina ya mwandishi Katama Mkangi wa Kenya na Mohamed Suleiman wa Zanzibar: Mintarafu kipengele cha Usambamba

Masoud Nassor Mohamedd
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar

almanamo@yahoo.com

Makala hii inanuia kuangazia kipengele cha usambamba ambacho ni kimoja kati ya vipengele vilivyopuuzwa na kusahauliwa katika ulimwengu wa fani ya fasihi ya Kiswahili, hususan nathari. Hata hivyo, kipengele hiki kitaangaliwa kwa njia ya ulinganishi baina ya waandishi wawili; mmoja wa Kenya (Katama Mkangi) na mwengine wa Tanzania Zanzibar (Mohammed Suleman) Riwaya nne zitatumika kiulinganishi katika uchunguzi huu ambazo ni Mafuta (1984) na Ukiwa (1975) za Katama Mkangi na Kiu (1972) na Nyota ya Rehema (1976) za Mohamed Suleiman. Makala itaanza kuieleza dhana ya usambamba kwa mujibu wa watalamu mbalimbali pamoja na mifano kadhaa, baadaye, makala hii itawatambulisha na kuwaeleza kwa ufupi waandishi teule ambao riwaya zao zimetumika katika uandishi wa makala hii. Na mwisho kabla ya hitimisho makala itabainisha kufanana na kutafautiana kwa waandishi hawa katika kipengele cha usambamba ambacho kinaonesha ufundi mkubwa wa lugha kwa waandishi. Ni matumini yangu kuwa, makala hii itasaidia sana kuonesha ustawi wa lugha ya Kiswahili katika eneo hili la fasihi miongoni mwa waandishi wa eneo pana la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar na Kenya ikiwa ni sehemu za Jumuiya ya Afrika Mashariki zenye historia kubwa ya uandishi wa riwaya za Kiswahili. Aidha inaweza kuwa ni chanzo kizuri cha kuwaunganisha waandishi wa kazi za fasihi katika eneo la Afrika mashariki pamoja na kusababisha mabadiliko chanya ya uandishi bora wa riwaya.

Uwezekano wa kutumia Lugha za Kiafrika katika nyanja za Elimu

Mbwarali Kame
Chuo Kikuu cha Moi
dkttabuyaasir@gmail.com

Kila anayeishi kwenye ulimwengu huienzi lugha yake na kuipa kipawa mbele katika mambo mengi ya kimaisha na hata swala la elimu. Lugha za Kiafrika zimekuwa za dharauliwa na kuwekwa kwenye kiwango kutoweza kutumiwa katika ufundishaji au kwenye nyanja za elimu. Kuna dharura kubwa kufanywa utafiti wakuhusishwa lugha za Kiafrika hasa lugha ya Kiswahili na uwezo wake katika elemu na ufundishaji jamii mambo muhimu yanayo wahusu. Kwa sasa, karibu lugha 200 za Kiafrika hutumiwa katika shule barani Afrika, kwa kiasi kikubwa katika madarasa ya awali ya shule za msingi. Lugha chache za Kiafrika hufundishwa pia katika shule za sekondari na vyuo vikuu. Ingawa mifano hii inaonyesha kwamba lugha za Kiafrika zinaweza kutumiwa kama lugha nyingine yoyote katika mfumo rasmi wa elimu katika ngazi zote, bado kuna mashaka kama kweli zinafaa kwa elimu ya mfumo rasmi. Makala hii itaangazia umuhimu wa nchi za Afrika kutambua na kuzienzi lugha za Kiafrika na njia gani zafaakutumiwa kufikia viwango vyakutambulika lugha hizo, kanuni gani zatakiwa zifuatwe ili kuziendeleza lugha, njia gani zafaa kutumiwa kustawisha lugha za Kiafrika kufikia maarifa ya kisayansi.

Kiswahili: Chombo adhimu cha kuleta mabadiliko katika biashara na kazi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Miriam Mwita

bagenim@gmail.com

Kiswahili ni lugha ya kimataifa kufuatia hatua ilizopiga pamoja na majukumu ambayo imetukwa tangu karne ya 18 hadi leo. Mathalani, tangu enzi hizo za kale, Kiswahili ilikuwa lugha ya biashara miongoni mwa Waswahili wenyewe na baadaye ikatumika kufanya biashara kati yao na wageni waliokuja katika pwani ya Afrika Mashariki. Leo hii, Kiswahili ni lugha rasmi na lugha ya taifa nchini Tanzania. Nchini Kenya, ni lugha ya taifa huku baadhi ya watu wakiitaja kuwa lugha rasmi kulingana na katiba mpya. Nchini Rwanda hivi majuzi, Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha rasmi na kuwekwa kwenye daraja moja na Kifaransa, Kiingereza, na Kinyarwanda. Zaidi ya hayo, Kiswahili kimekubaliwa kwa kauli moja kuwa kiwe lugha ya Umoja wa Afrika (AU). Isitoshe, Kiswahili kimepewa hadhi ya kuwekwa nafasi ya sita katika orodha ya lugha za kimataifa kikitanguliwa na Kiingrereza, Kifaransa, Kihispania, Kiarabu na Kireno. Pamoja na haya, Kiswahili kinakadiriwa kuwa na wazungumzaji zaidi ya milioni 160 duniani. Aidha, Kiswahili kinafundishwa katika vyuo mashuhuri vya dunia na aidha kinatangazwa katika vituo anuwai vya redio na runingandani na nje ya Afrika. Kutokana na habari hizi, ni bayana kuwa Kiswahili uwezo usiokuwa wa kawaida. Kufuatia mantiki hii, makala yetu inadhamiria kuchungua na kusadikisha uwezo wa Kiswahili katika kustawisha maisha kwa jumla na hivyo kuleta mabadiliko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, makala hii, itapendekeza baadhi ya mambo yatakayopelekea kuwepo ustawi wa biashara na kazi endapo matumizi ya Kiswahili yatahimizwa na kupewa kipaumbele na viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuwa lugha hutambulisha jamii, ni azma yetu kupendekeza kuwa jamii ya Afrika Masharik haina budi kutumia Kiswahili kujijenga kiuchumi, kielimu, kisiasa na kijamii.

Athari ya tafsiri isiyokuwa faafu katika sekta ya afya Nchini Kenya

Miriam Osore
Chuo Kikuu cha Kenyatta
kenyanimo@gmail.com

Tafsiri ni shughuli isiyoweza kutenganishwa na matumizi ya lugha katika mazingira ya wingi lugha. Tafsiri inahusu kuhamisha ujumbe wa makala kutoka lugha moja hadi nyingine. Watu wengi wanaohitaji huduma ya afya nchini Kenya wana kiwango cha chini cha uelewa wa lugha ya Kiingereza na hivyo basi wanahitaji tafsiri au ukalimani ili waweze kupata huduma kutoka vituo vya afya na hospitali. Mara nyingi wahudumu wa afya kama madaktari na wauguzi hujaribu kuwapashia taarifa kwa kutafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili au lugha za kwanza. Katika hali kama hizi inachukuliwa kwamba wahudumu hawa wana uwezo wa kutekeleza jukumu hili kwa sababu wanaweza kuzungumza lugha hizi. Kinyume na matarajio haya, tafsiri na ukalimani ni taaluma zinazomhitaji mtu kupata mafunzo maalumu na uwezo wa kuzungumza lugha sicho kigezo pekee cha kumwezesha mtu kutafsiri. Vivyo hivyo, taaluma ya tiba inahitaji utaaluma wa hali ya juu. Kimsingi, kuhamisha ujumbe kwa aina yoyote kutoka kwa lugha moja hadi nyingine kwa kuzingatia umilisi wa lugha pekee ni jambo la kupotosha na kuhatarisha maisha ya wagonjwa. Kwa hivyo, ujuzi wa taaluma ya tibu pamoja na umilisi wa lugha ni mambo muhimu ya kuzingatia

katika tafsiri ya sekta ya afya. Nchini Kenya hapana watafsiri au wakalimani waliohitimu ambao wameajiriwa na serikali katika sekta ya tiba ili kusaidia wahudumu wa afya kutekeleza majukumu yao. Makala haya yanalenga kuchanganua na kutathmini jinsi ambavyo tafsiri inavyoendelezwa katika vituo vya afya. Makala yatadondoa baadhi ya msamiati wa Kiswahili unaotumiwa kati ya wahundumu na wagonjwa nchini Kenya. Kiwango cha mawasiliano na uhakika kitachunguzwa ili kudhihirisha athari ya tafsiri hizi kwa wagonjwa.

Fasihi Simulizi na Umajumui wa Afrika Mashariki: Mfano wa Tendi Simulizi za Ukanda wa Maziwa Makuu

Mlinzi Mulokozi

tamulokozi50@yahoo.com

Maingiliano na mashirikiano miongoni mwa watu wa Afrika Mashariki hayakuanza katika karne ya ishirini, bali yalianza zamani zaidi kabla ya ukoloni. Katika eneo la Maziwa Makuu mashirikiano na maingiliano miongoni mwa watu, himaya na falme yalikuwa mkubwa sana, kama si mkubwa zaidi, kabla ya ukoloni kuliko ilivyo sasa. Palikuwa na maingiliano kwenye ngazi ya kijamii (koo), kabila, utawala (nasaba za kifalme, himaya kama za Buganda, Buha, Buhaya, Bukerebe, Bunyoro Kitara, Burundi na Rwanda), utamaduni (zikiwamo imani za dini ya asili, visasili na miviga yake, sanaa na fasihi simulizi). Maingiliano haya yamezungumziwa kidogo na wanahistoria na wanaisimu, lakini hayajapata kushughulikiwa kwa undani na wanafasihi. Makala yetu inayotokana na utafiti wa uwandani wa tendi za nanga za mkoa wa Kagera itachunguza uakisi na usawiri wa maingiliano ya watu wa eneo la Maziwa Makuu katika tendi simulizi za nanga. Tendi tatu za nanga zilizorekodiwa na M.M. Mulokozi na watafiti wengine kati ya 1950 na 1985 zitatumika katika mjadala huu; tendi hizo ni *Mugasha*, *Mugangala* na *Nyarubamba*. Lengo ni kuonesha kuwa wananchi wa Afrika Mashariki, kabla ya ukoloni, walikuwa na maingiliano makubwa na walijua kuwa wao ni wamoja na wanahitaji kushirikiana ili kujinusuru. Utambuzi wa jambo hili huweza kuwa msingi mzuri wa kiitikadi wa kuunda ushirikiano mpya na hatimaye Shirikisho la Afrika Mashariki.

Dhima ya Mashirika ya Utangazaji ya Serikali kwa kueneza Kiswahili hasa Uganda Broadcasting Corporation nchini Uganda

Monday Akol Amazima
mwalimakol@gmail.com

Mashirika ya utangazaji yanayomilikiwa na serikali katika nchi wanachama wa Afrika Mashariki, yanajukumu kubwa la kuelimisha, kuhamasisha na kuburudisha wana-Afrika Mashariki ili Kiswahili kienziwe kama lugha ya mawasiliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini kwa sababu moja au nyingine baadhi ya mashirika hayo kama Uganda Broadcasting Corporation (UBC) la Uganda hayajatoa mchango kama inavyokusudiwa kwa kueneza Kiswahili nchini Uganda. Kwa hivyo makala haya yatalenga kueleza kwa undani nafasi na changamoto kwa mashirika ya utangazaji ya serikali kama UBC katika harakati za kukikuza Kiswahili. Pia makala haya yatajaribu kutoa iwezekanavyo historia ya matangazo ya Kiswahili nchini Uganda na kutoa ufafanuzi juu ya mashirika mengine ya utangazaji ambayo yamejaribu kutoa huduma zao kwa

Kiswahili. Mwishowe makala haya yatatoa mapendekezo kwa mashirika ya serikali kama UBC yatakayosaidia kubadili mfumo na usimamizi wa vipindi vya Kiswahili. Mapendekezo haya yatatumia mifano kutoka mashirika ya utangazaji yanayotumia Kiswahili ndani na nje ya Afrika Mashariki. Mada hii niliyoiteua inazingatia mada kuu ya kongamano ambayo ni; kuleta mabadiliko katika jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kiswahili. Zaidi mada hii itatosheleza baadhi ya mahitaji ya mada ndogo namba tisa ambayo ni; Kiswahili, Vyombo vya Habari na mawasiliano kwa umma.

Nafasi ya Kiswahili katika Sekta ya Elimu Nchini Tanzania

Mussa. M. Hans
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
mussahans30@gmail.com

Lugha ni kitu muhimu sana katika mawasiliano ya sekta mbalimbali kama vile elimu, afya na siasa. Mara baada ya nchi ya Tanzania (wakati huo Tanganyika) kupata uhuru, lugha ya Kiswahili iliendelea kutumika katika sekta mbalimbali ingawa kwa viwango tofauti tofauti. Mathalani, katika sekta ya elimu, Kiswahili kilitumika na bado kinaendelea kutumika kama njia ya mawasiliano katika ufundishaji wa masomo ya shule za msingi na vyuo vya ualimu kwa masomo ya ngazi ya cheti. Aidha, Kiswahili ni somo la lazima kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Kwa upande wa elimu ya sekondari hadi vyuo vikuu, lugha ya mawasiliano ni Kiingereza na Kiswahili kinafundishwa kama somo. Ili kuhakikisha kwamba matumizi ya Kiingereza yanaimarishwa na kwamba wanafunzi wanakielewa vizuri Kiingereza hususani katika ngazi ya sekondari kumekuwa na jitihahada mbalimbali ambazo zimekuwa na bado zinaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 1980 kumekuwa na tafiti na ripoti mbalimbali zikifuatiwa na matamko kadhaa ya viongozi waandamizi wa serikali yakionesha umuhimu wa kutumika kwa lugha ya Kiswahili katika mawasiliano mapana ikiwa ni pamoja na sekta ya elimu nchini Tanzania. Aidha, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2014 inakitambua Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha za kufundishia kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vikuu. Lengo la makala haya ni kutathmini nafasi ya Kiswahili katika sekta ya elimu nchini Tanzania huku yakitilia maanani matamko ya viongozi waandamizi wa serikali, sera ya elimu na hali halisi ya matumizi ya Kiswahili katika ngazi mbalimbali za elimu nchini Tanzania.

Mwegemo wa Lugha ya Kiswahili Nchini Uganda

Muthahinga Moses
na
Kulava Y. S.
mozemb@yahoo.com

Ingawa lugha ya Kiswahili imefanywa lugha jumuishi kwa nchi za Afrika Mashariki; ukubalifu wake kwa wanafunzi wa shule za upili ungali ni wa mwendo pole. Kwa utafiti uliofanywa katika shule za upili wilayani Kasese; ilibainika kwamba wanafunzi wa shule za upili wana mielekeo hasi kuhusu kukukubali Kiswahili kiwe somo la lazima kwa shule za upili nchini Uganda. Makala haya – utafiti wake umeongozwa kwa nadharia ya uakili kwa mwegemo wa hojaji LIKATI; kwa madhumuni ya: kupambanua mielekeo ya wanafunzi waswahili wanaojifunza Kiswahili katika

shule za upili na kubainisha mambo ambayo yanawapelekea wanafunzi waswahili wa shule za upili kuwa na mitazamo tofauti katika kujifunza Kiswahili.
Maneno Muhimu: Mielekeo ya wanafunzi kuhusu Kiswahili

Makosa ya uandishi katika insha za wanafunzi wa skuli za msingi za mjini Unguja

Mwanahija Ali Juma
na
Amour Salim Said
mwanahijajuma1@gmail.com

MAKALA hii inachunguza insha za wanafunzi na kubainisha makosa yanayojitokeza katika uandishi wa insha hizo kwa wanafunzi wa darasa la nne katika skuli saba za mkoa wa Mjini Magharibi Unguja Tanzania. Mada iliyozingatiwa ni Kiswahili na Uandikaji. Katika makala hii tutafafafanua kwa uwazi makosa ya kimofolojia na kisintaksia katika insha hizo. Makala hii ni muhimu kwa watunga mitaala na vitabu vya kufundishia kujifunza kuandika Kiswahili. Pia itakuwa marejeo kwa watafiti wa mada kadhaa za sarufi na isimu ya Kiswahili.

Navigating towards Kiswahili, the East African Community and Sustainable Development

Mwanakombo Mohamed
Moi University
mwanakombonoordin@yahoo.com

The protocol on the establishment of the East African Kiswahili Commission declared," The East African Kiswahili Commission formed in 2007 has the vision of being the leader in the promotion and coordination of the development and usage of Kiswahili for regional unity and sustainable socio- economic development in partner states". The study seeks to critically analyze the role of Kiswahili as the language of solving development challenges facing the EAC. The research questions are: How will Kiswahili enable sustainable socio- economic development in partner states? How can language promote regional unity? The aim of this study is to evaluate the discussion on sustainable and inclusive development in the East African Community from the point of view of Kiswahili as the medium of communication. The debate will introduce current analyses of the sustainable development goal 4. The research is focused on SDG 4 as it forms the foundation of the realization of all the other SDGs. Education here is seen as the key driver of the successful implementation of all the other sustainable development goals in the East African region. The paper shall elucidate the East African Community as a regional organization, its objectives and the current situation. The role of Kiswahili as the language of the East African Community and the challenges it encounters will be discussed. This study is significant as it will define and guide our perceptions of the role of the East African Kiswahili Commission in fulfilling its mandate. Secondly, it will highlight how the use of Kiswahili constitutes the peoples view of the world they live in. Kiswahili in East Africa is a reflection of the social, cultural and physical environment of the people. KEY Words: sustainable development, integration, world view.

Kiswahili kama Injini ya Mageuzi katika Afrika Mashariki

Mwenda Mbatiah

Chuo Kikuu cha Nairobi

anmbatiah08@yahoo.com

Katika makala hii, tunatumia neno “mageuzi” kwa maana ya mabadiliko makubwa ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia ambayo yanalinyanyua taifa kutoka kiwango cha chini cha maendeleo hadi kiwango cha juu. Hatuna shaka kwamba mataifa ya Afrika Mashariki yanajitahidi kubuni mikakati ya kufikia mageuzi kama hayo, kwa muda mfupi iwezekanavyo, kwa manufaa ya watu wake. Huu ndio mkondo wa ulimwengu mzima ambapo kila dola hujaribu kuhalalisha kuwepo kwake kwa kuboresha maisha ya wananchi. Katika makala hii, tunajadili kwamba Kiswahili kinaweza na kinafaa kutumiwa katika mradi huu. Hata hivyo, kuna kazi kubwa inayohitaji kufanywa ili kukiandaa kwa dhima hiyo. Tunachunguza hatua zifaazo kuchukuliwa kukiwezesha Kiswahili kuwa injini madhubuti ya kufanikisha mageuzi katika Afrika Mashariki. Katika kufanya hivyo, tunaangazia wajibu wa asasi kama vile serikali, mashirika mbalimbali, wasomi na wadau wote kwa jumla.

Utungaji wa Kamusi za Istilahi za Kiswahili: Mikakati, Changamoto na Mustakabali wake

Mwenda Mukuthuria, James Omari Ontieri
Chuo Kikuu cha Maasai Mara, Kenya

na

Stanley Adika Kevogo
Chuo Kikuu cha Mount Kenya
surayangu@gmail.com

Maendendeleo katika sanaa na ufundi wa leksikografia yamepelekea kuwepo kwa idadi kubwa ya kamusi za istilahi za Kiswahili katika fani na taaluma mbalimbali. Hata hivyo, licha ya maendeleo hayo, hakuna kamusi kamilifu isiyo na dosari. Kwa kutumia mbinu za utafiti wa maktabani, makala hii inachunguza na kuchanganua mikakati na mbinu ambazo zimekuwa zikitumika katika utungaji wa kamusi za kiistilahi za Kiswahili. Azma yetu ni kubainisha mbinu zinazofaa zaidi katika utungaji kamusi za istilahi za Kiswahili zitakazokidhi mahitaji ya sasa ya lugha hiyo. Hoja kuu ya makala hii ni kwamba kuegemea zaidi kwenye mbinu za tafsiri na zile kileksikografia badala ya zile za kiteminografia katika utungaji wa kamusi za istilahi za Kiswahili kumetinga ufanisi katika sayansi na sanaa hiyo.

Istilahi Muhimu: Istilahi, Teminografia, Leksikografia, tafsiri

Kiswahili, Mshikamano wa Kikanda na Maendeleo

Nancy Kahaviza Ayodi
Maasai Mara University
nancyayodi@gmail.com

Wasilisho hili liinadhamiria kubainisha majukumu ya Kiswahili katika kukuza mshikamano na maendeleo katika Jumuiyia ya Afrika Mashariki. Kiswahili ni lingua franca inayokubalika na kutumiwa na watu zaidi ya milioni 100 ulimwenguni. Hali hii inaashiria uwezo wa lugha hii kukuza na kuzidisha umoja na mshikamano miongoni mwa watu wenye misingi tofauti ya kiisimu,

kijamii au kisiasa. Azimio la Muungano wa Afrika (OAU) mwaka wa 1986 kuwa lugha ya Kiswahili itumike katika vikao vya Muungano ilichochewa na uwezo huu wa Kiswahili. Hata hivyo, hali ya Wingi Lugha barani Afrika imepelekea kuwepo changamoto kubwa za mawasiliano katika elimu na sekta nyinginezo. Matokeo ni kuwa nchi nyingi barani kwa sababu za kisiasa na/ au za kiuchumi zimehiari kutumia lugha za kikoloni kama lugha rasmi na wakati mwingine pamoja na lugha moja au zaidi za Kiafrika; mfano mzuri ni matumizi ya Kiswahili Afrika Mashariki pamoja na Kiingereza, Kifaransa au Kiarabu.Mapendekezo yanayotolewa katika makala ni kuwa lugha ya Kiswahili ina uwezo sawa na lugha za kikoloni mradi iwezeshwe na mataifa husika.

Popular Culture and Swahili Slang

Nancy Jumwa Ngowa
&
Deo Ngonyani

This is a study of Swahili slang as used in Dar es Salaam and Mombasa. Slang is widely recognized as distinctive patterns of speech that mark in-groups and constitute a cultural style, especially of youth. It is an essential component of popular subversive youth culture. Slang is often ignored by prescriptively inclined grammarians and linguists even though it is prevalent in all languages. In this study we highlight slang whose origins are easily traced to common metaphors and metonymy. The study draws its inspiration from the cognitive approach to metaphors and metonymy. Since the publication of Lakoff and Johnson's (1980) *Metaphors We Live By*, metaphors have been recognized as a major vehicle of everyday thought. They are characterized as expressions with two domains: (a) the target domain or the phenomenon talked about, and (b) the source domain or the phenomenon whose terms are used to express the target phenomenon. Metonymy, on the other hand, is recognized as exhibiting a relationship between items in one domain, but one is made more prominent in order to represent the other (Kövecses & Benczes, 2010). For example, *pamba* 'cotton' is playfully transformed to represent sharp outfit by the youth in Dar es Salaam. We demonstrate how metonymy leads to creative use of existing everyday vocabulary in Swahili and how new words are coined. One important agent of this creative process is music. We present examples of slang from popular music in the two cities.

Athari ya Mwingiliano wa Utamaduni kwa Wageni wanaojifunza Kiswahili

Nasra Habibu Ally
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
nasrahabibu@yahoo.com

Kuna uhusiano mkubwa baina ya lugha na utamaduni. Mjifunzaji wa lugha ya kigeni hanabudi kuufahamu utamaduni wa lugha anayojifunza ili kuweza kuwasiliana. Wageni wanaojifunza Kiswahili vilevile hujifunza utamaduni wa Waswahili. Wageni hao hufika katika mikoa mbalimbali ya Tanzania na huko hujifunza Kiswahili. Katika mikoa hiyo, wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili huwa wana tamaduni mbalimbali zinazotokana na lugha zao za Kikabila katika maeneo yao. Tamaduni hizo hazitenganishwi na utamaduni wa mswahili na hivyo mjifunza lugha kuweza kuzichukua. Kwa hivyo, lengo la makala haya ni kubainisha athari za mwingiliano wa utamaduni wa wazungumzaji wa Kiswahili kwa wageni wanaojifunza Kiswahili katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania.

Mambo muhimu: *Mswahili, utamaduni, mwingiliano wa utamaduni na ujifunzaji wa lugha ya Kigeni.*

Matumizi ya Kiswahili na wanafunzi katika siasa na uongozi wa vyuo vikuu nchini Kenya kwa ajili ya maendeleo na mfungamano wa Afrika Mashariki

Nathan Oyori Ogechi
Chuo Kikuu cha Moi, Kenya
ogechinathan@yahoo.com

Makala hii itajaribu kudhihirisha na kuchambua ongezeko la matumizi ya Kiswahili miongoni mwa vijana nchini Kenya wanapokuwa wanaendesha siasa zao na kushiriki katika vikao vya uongozi na usimamiaji wa vyuo vikuu; na kwa kufanya hivyo, kubainisha mada za Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa zinazojadiliwa kwa Kiswahili kama vile amani, virusi vya ukimwi na kujenga ushirikiano. Mjadala utakadiria na kutabiri jinsi ambavyo vijana, wakitumia Kiswahili, wataharakisha malengo endelevu ya maendeleo na kuleta mwunganiko wa Afrika Mashariki. Itaonyeshwa kwamba katika mwongo mmoja uliopita, vijana wengi wamejisajili katika vyuo vikuu vya umma na vya kibinafsi. Isitoshe, tangu 1985 Kiswahili ni somo la lazima linalotahiniwa katika mitihani ya mwisho ya kitaifa ya darasa la nane na kidato cha nne, na pia matokeo ya mtihani, ama ya Kiswahili au Kiingereza, huzingatiwa ili kumwezesha mwanafunzi kuingia katika taaluma mbalimabali chuoni. Kutokana na hilo, ni kawaida kuwashuhudia wanafunzi wakiongea na hata kutuma jumbe fupi kwa simu kwa Kiswahili ambacho ni lugha rasmi na ya taifa kikatiba nchini Kenya na lugha ya kazi katika mwungano wa Afrika Mashariki. Vijana wa vyuo vikuu hutangamana sio tu vyuoni mwao bali pia na wenzao wa vyuo vingine nchini na hata nchi jirani. Kwa kujikita katika muktadha huu, makala itajaribu kuangazia matumizi ya Kiswahili katika shughuli za wanafunzi kama vile vyama vya serikali za wanafunzi vyuoni, vyama vingine chuoni na mwingiliano wao na maafisa wa vyuo vikuu ili kutathmini matumizi ya Kiswahili katika maingiliano yao. Mjadala huu utachanganua aina za "Viswahili" vinavyotumika na kujadili mustakabali wa ongezeko hilo la matumizi ya Kiswahili miongoni mwa vijana katika mfungamano na maendeleo ya Afrika Mashariki.

Kiswahili vyombo vya habari na mawasiliano kwa uma

Niyokindi Valère
Chuo kikuu cha Mwanga cha Bujumbura

niyokindivalere@gmail.com

Ikisiri ya Mada : Kiswahili kama lugha zingine uma wanaitumia katika nchi mbalimbali tofauyi pia jumuia ya Afrika mashariki .Kwani,humo nchini hizo za Afrika mashariki, lugha kawaida ya kuongea katika majadiliano ndio kiswahili .Kwa kimaukuzaji,tunaona umuhimu wa kiswahili kwa vyombo vya habari na kwa uma kupitia mawasiliano yao.Vyombo vya habari ni jinsi muhimu sana inayosaidia watu kufuatilia habari kitaifa au kimataifa zinazoeleza sekta mbalimbali za maisha. Na hapo,malengo yavyo ni usambazaji au utangazaji wa taarifa ili zifikie watu wengi wanaowezekana .Inapotumika lugha kama kifaransa na kirundi tu kwa kupuuza kiswahili,ina maana kuna kipande cha uma ambao hawatasikiliza redio au hawatafuata vipindi kupitia

runinga.Ili vyomvo vya habari vishike malengo yavyo vinalazimishwa kutumia lugha zote wanazoongea nchini ambapo vinatangazia ,miongoni mwazo kuna Kiswahili. Kiswahili ni muhimu kwa uma, Inawawezesha uma kupata habari ya mambo yanayoendelea nchini mwao na pia ulimwenguni pote kujuwa kwamba kuna nchi zinazotumia kiswahili kama lugha mama, Kwa mfano, Hapo kupitia kiswahili,na vyombo vya habari, mrundi anaweza kufuata yanayofanyika Tanzania. Kiswahili, ni lugha inayohitajika sana.kutokana kwanza na kuwa ni lugha inayotumiwa katika kanda la maziwa makuu na Africa mashariki.Vyombo vya habari vina mchango mkubwa sana katika sekta mbalimbali: Kwa ufanyabiashara; Kwa ukulima; Kwa ufugaji; Elimu na mafunzo; Kwa kudumisha amani; Kwa maendeleo;na kadharika. Kwa kimaukuzaji,nitajaribu kuchambua sekta moja moja mwa hizo hapo juu.

Ujifunzaji na Umaizi wa Kiswahili na Kiingereza: Tathmini ya Ufaulu wa Masomo Nchini Tanzania

Nkinde Mwangoka
Chuo Kikuu cha Jordan, Morogoro, Tanzania

ruthwynn6@gmail.com

Kulingana na sera ya lugha nchini Tanzania, Kiswahili kinatumika kama lugha ya mawasiliano na ya kufundishia katika shule za msingi kwa masomo yote isipokua somo la Kiingereza. Kwa ngazi za elimu ya sekondari na vyuo vya elimu ya juu, lugha ya kufundishia ni kiingereza. Kiswahili kinafundishwa kama programu katika vyuo au somo tu katika sekondari. Mpango huu wa kisera kuhusu lugha unakinzana na mikabala ya ujifunzaji na umaizi wa lugha na matokeo yake ni ufaulu duni katika masomo. Moja kati ya hatua za awali za makuzi na mabadiliko ya mtoto ni ujifunzaji wa Lugha. Cherry (2014:) anasema watafiti mbalimbali wametoa mapendekezo ya nadharia mbalimbali zinazoeleza jinsi na sababu za ujifunzaji lugha. Cherry anasema kuwa Skinner anapendekeza mbinu ya ujifunzaji lugha unaotokana na uigaji na uhamasishaji wakati Chomsky anadai kuwa lugha ni uwezo wa asili wa mwanadamu. Chomsky anasisitiza hili kwa kusema kuwa mtoto anazaliwa na uwezo unaomwezesha kujifunza na kutoa lugha mara baada ya kujifunza msamiati wa msingi wa lugha husika. Aidha, Chomsky anaongezea kwa kusema kuwa, watafiti wamegundua kuwa ujifunzaji wa lugha unaanza kabla mtoto hajazaliwa na wanadai kuwa mtoto akiwa mchanga anaweza kutambua maneno na mpangilio wa sauti ya anazotamka mama yake. Katika umri wa miezi minne mtoto anakuwa na uwezo wa kutofautisha sauti na kusoma kile ambacho midomo ya mama yake inazungumza. Pia watafiti hao wamegundua kuwa watoto wachanga wana uwezo wa kutofautisha sauti za maneno za lugha zote. Katika umri wa miezi kumi baada ya kuzaliwa wanaanza kutambua sauti za maneno ya lugha zinazozungumzwa nyumbani tu. Akifikisha umri wa miaka mitatu anakuwa na msamiati usiopungua maneno elfu tatu. Uwezo wa ujifunzaji lugha moja (ya kwanza) na baadae lugha zaidi ya moja (ya pili) unakuwa mkubwa zaidi katika hatua za mwanzo za makuzi na mabadiliko ya umaizi wa mtoto. Uwezo huo unapungua kadri umri unavyoongezeka. Makala hii inajaribu kubainisha ni kwa kiasi gani (sera ya lugha kuhusu elimu) utaratibu wa lugha ya kufundishia unachangia katika ufaulu duni wa wanafunzi hususani kwa ngazi ya sekondari na vyuo. Makala hii itazingatia, mbali na vigezo vingine, kigezo cha mabadiliko na makuzi, na umaizi katika ujifunzaji wa lugha katika hatua za mwanzo za makuzi ya mtoto na vikwazo anavyokumbana navyo katika ujifunzaji wa masomo. Aidha, makala hii

itajaribu kutathmini dai la Omary, I. M. (2011) anayesema kuwa ujifunzaji duni wa lugha na ufaulu wa masomo hauendani bali tatizo ni kigezi cha tatu ambacho ni ufundishaji duni.

Tafakuri mpya kuhusu mwanguko wa maadili katika mashairi ya nyimbo za Taarab ya Sasa

Omar Salum Mohamed

Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar - Suza

Makala hii inakusudia kuweka bayana mwanguko wa maadili uliyomo katika mashairi ya 'Taarab ya Sasa', pamoja na kubainisha sababu za mwanguko wenyewe. Sina shaka yeyote kwamba wazoefu na magwiji wa muziki wa taarab wanayatambua maadili yaliyoongoza muziki huu katika utungaji na katika uimbaji wa mashairi ya nyimbo zake. Maadili haya yaliheshimiwa na kutafsiriwa kama ndiyo dira msingi ipasayo kuongoza mfumo kamili wa muziki wa taarab. Licha ya kuwepo vikundi na klabu mbalimbali za muziki wa taarab katika nchi za mwambao wa Afrika ya Mashariki, hakuna kikundi au klabu yeyote iliyothubutu kuikengeuka dira msingi yenye kuongoza maadili haya. Ule muwala na urari katika mashairi ulitiririsha mashairi ya klabu na vikundi mbalimbali kufuata mfumo uliyo sawa mmoja. Kiasi ambacho mashairi ya vikundi hivi hayakuwa rahisi kutambuliwa tafauti za maumbo yao kabla ya kuyaimba. Katika utafiti wa hivi karibuni uliofanyika Bara na Visiwani Zanzibar, umebainisha wazi mwanguko wa maadili katika mashairi ya nyimbo za 'Taarab ya Sasa'. Na kwamba kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa dira msingi si katika utungaji wa mashairi tu, na katika kuyaimba. Madhara ya ukiukwaji huu lau yaachiliwa yaendelee kama ilivyo hivi sasa, miaka michache ijayo muziki wa taarab utaangamia na kuyoyoma mfano wa moshi upoteavyo angani. Ilivyo hasa mashairi ya taarab ndiyo roho ya viungo mbalimbali vya muziki wa taarab kama vile uimbaji, uitikiaji, upigaji ala za muziki, uchezaji, utuzaji na pia uvaaji. Hivyo, kukengeuka maadili yatengezayo shairi la wimbo kuwa wimbo huathiri viungo vikamilishavyo muziki wa taarab kuwa taarab. Mashairi ya taarab yalikuwa na mjengeko maalumu yaliyotumia lugha maalumu na kwa sababu maalumu. Kukosekana kwa mambo haya katika mashairi ya 'Taarab ya Sasa' ndiyo sababu hasa ipelekeayo mwanguko wa maadili wa mashairi haya. Kasi iliyopo ya ukiukwaji wa dira msingi ambayo yazidi kupata nguvu kwenye jamii ni utabiri usiyo shaka juu ya uzikwaji wa 'Taarab Asilia' uliyokusudiwa na kama ulivyokusudiwa. Shaka iliyopo kwamba kadiri mwendelezo huu upigapo hatua, ndivyo ile dhana ya muziki wa taarab inapopotea. Na hatimaye kuwa historia ya utamaduni wa pwani katika kipindi fulani. Katika kulitambua hili ndipo fikra za uandishi wa makala hii zilipoibuliwa ili iwe fundisho na tahadhari katika jamii iliyopo na ile ijayo. Wahenga walisema, 'Usipoziba ufa utajenga ukuta', na pia 'Mdharau mwiba humchoma'. Lakini pia tusisahau hekima iadilishayo isemayo, 'Kinga ni bora kuliko tiba'. Majuto yajayo baada ya ukumbusho huzidisha kejeli iumizayo moyo kila ufikiripo.

Nafasi ya Kiswahili katika utandawazi na ukuzaji wa Ushirikiano katika Kanda ya Afrika Mashariki

Ondara Kiyondi Reuben

Chuo Kikuu Cha Kisii
ondarakiyondi@yahoo.com/ondarakiyondi@gmail.com

Lugha ni mojawapo ya 'washenga' wakuu watano wa utandawazi, wengine wakiwa fasihi, vyombo vya habari, muziki na tafsiri (Kezilahabi, 2006). Washenga hawa ndio nguzo kuu ya utandawazi kwa kuwa ndio waenezaji na wakuzaji wakuu wake. Utandawazi unahusisha kuzungumzia maisha ya kila siku ya watu na lugha wanayoitumia katika mawasiliano, elimu na sekta zote za kijamii. Aidha, hunuia kujenga uhusiano wa kiulimwengu katika nyanja za biashara, uchumi, siasa, utamaduni na jamii kwa kuifanya dunia kuwa kama kijiji kimoja, kilicho na hali sawa ya maisha. Mahusiano haya ni mojawapo ya Malengo Endelevu ya Maendeleo, yanayonuiwa kuafikiwa kufikia mwaka 2030 na jamii ya kimataifa. Kiswahili ndiyo lugha ya kipekee katika kanda ya Afrika Mashariki iliyo na sifa na uwezo wa kuunganisha watu wa mataifa haya na kukuza ushirikiano wa kimaendeleo utakaohakikisha kuafikiwa kwa haya malengo endelevu ya maendeleo katika eneo hili. Makala haya yananuia kuweka wazi mchango na nafasi ya Kiswahili katika utandawazi pamoja na kukuza ushirikiano huu wa kimaendeleo katika eneo hili kwa mujibu wa malengo endelevu ya maendeleo yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa.

Kiswahili, Trade and Business: The case of Rwanda's Northern Corridor

Pacifique Malonga

becos1@yahoo.com

Africa's development move is not only a big deal but also a question of choice and direction. It is not the energy one uses to move but the strategy he/she adopts. The best methodological implementation of Africa's plans should focus on people's gain not leader's decisions. Communication between both parties should be really based on expeditious actions involving people in their daily activities. Kiswahili is in East Africa what English is in the commonwealth countries, an identity and a unifying factor for faster integration and sustainable development. If Kiswahili is not given its real value in the EAC, other plans and projects will be like flowers blossoming and fading few days after. While the EAC moves well in some directions, it needs serious considerations in others giving time, means and ways to its people to truly communicate effectively and efficiently. In the popularly known as Rwanda's northern corridor including, Rwanda, Uganda & Kenya trade and Business seems to be moving, well with petty traders moving from Kigali to Nairobi through Kampala and Vice versa. However, the real business still needs Kiswahili use and development to make this corridor from temptation to redemption of the common man. A practical solution resides in the collective efforts to set up a solid foundation for Kiswahili to steadily grow strongly among the EAC nations and beyond with Rwanda, Uganda and Kenya "Northern Corridor" paving the way and showing direction, hence shaping the integration people want.

Posters, Fliers and Programs: Which Way Kiswahili?

Pamela Anyango Oloo
Maseno University

aoloo2001@yahoo.com

Communication is a key ingredient of all aspects of human interaction and is carried out to pass information, exchange ideas or simply to establish a sense of oneness or commonness between two or more interactants. This paper seeks to examine the place of Kiswahili in dominant health discourse, particularly that on HIV and AIDS. The concern here lies in the fact that the bulk of communication in the medical arena presupposes literacy on the part of their target audience, yet this is hardly the case. The media of choice remain posters and fliers while radio programs now focus on the local languages, conferences and meetings held on critical health issues use mainly English and sometimes French as the official conference language. This situation obtains even in Kenya where Kiswahili is recognized as an official language alongside English. Effective communication, reaching a wide audience, remains a crucial means of containing the spread of disease and managing infections. Examination of communication strategies, including the choice of language of communication is therefore key. It is therefore necessary to critically interrogate the place of Kiswahili in the face of the foregoing.

Kuleta mabadiliko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kiswahili: Fasihi ya Watoto kama Kichochezi cha kujua Kusoma na Kuandika

Pamela Muhadia Ngugi
Chuo Kikuu cha Kenyatta
muhadia@yahoo.com/ngugi.pamela@ku.ac.ku

Utafiti uliofanywa na shirika la Uwezo- Kenya kuanzia mwaka wa 2014 hadi 2016 kuhusu "*Are our Children Reading?"* umethibitisha kuwa watoto wengi hasa katika shule za msingi hawajui kusoma na kuandika kwa mujibu wa viwango vya madarasa waliyomo. Kwa sababu hiyo, shirika hili limependekeza mabadiliko katika mikabala ya ufundishaji na kupendekeza kutumika kwa mkabala jumuishi wa elimu iwapo sekta ya elimu inatarajia kupata maendeleo thabiti. Mkabala jumuishi huhimiza wanafunzi kushiriki katika ujifunzaji wao na hivyo basi, kusaidia katika ukuzaji wa maarifa ya kufikiria kwa kiwango kikubwa. Katika kufanya hivi, ujifunzaji huwa wa maana kwa mwanafunzi na huchangia katika kujenga stadi nne za lugha ambazo ni, kusoma, kuandika, kusikiliza na kuongea kwa kiwango cha juu. Lengo la makala hii ni kujadili na kubainisha namna ambavyo fasihi ya watoto inaweza kutumika kama kichochezi cha kujua kusoma na kuandika, hasa pale ambapo wanafunzi wanapewa nafasi ya kujenga maana kutokana na usomaji wao. Fasihi ya watoto inaweza kuchangia katika kuinua maarifa, stadi na milelekeo chanya miongoni mwa wanafunzi kuhusiana na masuala ya kusoma na kuandika hali ambayo itachangia katika kufikia malengo endelevu ya maendeleo katika sekta ya elimu katika jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kiswahili, kujua Kusoma na Kuandika na Afya

Patience Mbonabuca
Kikuu cha Taifa la Burundi

mbonapati.pipi@gmail.com

*"*Kipendacho moyo ni dawa*"*. Kitabu kizuri ni dawa ya moyo wa bua. Kitabu kibaya huiangamiza nafsi. Kujua kusoma na kuandika Kiswahili ni njia bora ya kuimudu lugha na maudhui yake huifanya afya ama kuwa njema au kuwa mbaya. Kujua kuandika na kusoma ni lishe bora kiisimu

na kiafya. Maneno mazuri ni mafuta ya mifupa. Kiswahili chako afya yako. Kuandika kwako afya kwa jamii. Kusoma kwako malezi kwa nafsi yako na jamii. Afya yako makuzi ya Kiswahili. Kusoma na kuandika huzipanua akili na mali, akili na mali huijenga afya na huondoa umasikini. Je kusoma na kuandika Kiswahili na afya hutegemeana? Asili ya lugha ya Kiswahili bado ni mjadala mrefu. Wataalamu hudai kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni : huko Kongo (D.R.C), ni ki-pijini au ki-krioli, ni Lugha ya Jamii ya Vizalia au kilitokana na visiwa vya Lamu, Kilamu/Kiamu. Kiswahili hujizalisha na kujieneza sawa sawa na afya inavyokuza hali. Kujua kusoma na kuandika Kiswahili hubadili mawazo. Makala ni malezi na makuzi ya lugha. Kiswahili huzaliwa, hulelewa, huugua na hutibiwa na hufariki sawa sawa na binadamu. Zaidi ya makuzi ya watoto, hutegemea malezi kutoka kwa wazazi; Jumuiya ya Afrika mashariki Makao Makuu ya Kiswahili imekilea Kiswahili hakika, Afrika na Dunia nzima hunawiri. Mfano halisi ukimbizi nchini Tanzania. Malezi bora ni afya njema. Sina shaka Kiswahili hakitapotea kamwe. Kusoma na kuandika ni afya njema na huboresha maisha. Kusoma na kuandika hutegemea afya. Kusoma na kuandika si kipaji cha kuzaliwa nacho bali hufunzwa. Afya njema hutegemea lishe bora. Umasikini hupofusha kusoma na kuandika. Elimu duni ni kuhusishwa na matokeo kadhaa mabaya ya afya. utafiti wa siku zijazo, kwa kutumia njia ya ukali zaidi, itakuwa bora kufafanua uhusiano wa Kiswahili,kujua kusoma na kuandika na afya.

Kiswahili Rasilimali kwa Jumuia ya Afrika ya Mashariki: Mfano wa Nchi ya Rwanda

Patrice Ntawigira

ntapa2000@yahoo.com

Kadiri nchi ya Rwanda inavyoendelea kuona umuhimu mkubwa wa kujiunga na mataifa mengine katika eneo la kanda ya maziwa makubwa, zikiwemo nchi za Afrika ya Mashariki zinazotumia Kiswahili kama Lugha-unganishi; ndivyo Rwanda inalenga kukuza na kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii na nchi hizo. Ushirikiano huo unawafanya Wanyarwanda kuwa na haja kubwa ya kujua, kukuza na kuendeleza Kiswahili katika jamii ya Kinyarwanda ili waweze bila kipingamizi chochote kunufaika na ushirikiano huo. Kiswahili ni daraja kubwa tena imara la kudumu katika kuwaunganisha wanyarwanda na ndugu zetu za Jumuia ya Afrika ya Mashariki pamoja na mataifa mengine yote yanayotumia Kiswahili. Lugha hii ni bomba kubwa la kubasafirisha ujuzi, utaalamu, maarifa ya mambo mazuri yanayopatikana katika nchi zilizotutangualia kutumia lugha hiyo. Kiswahili ni mtaji mkubwa kwa wanyarwanda utakaotuwezesha kuwa na kupanua umoja na ushirikiano wa kudumu na mataifa mengine ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki. Ni Rasilimali inayoweza kutimika kwa kukuza maendeleo ya nchi yetu ya kiuchumi, kielimu, kiafya, kisiasa kijamii nk. Katika kipindi hiki kizuri cha kuboresha ushirikiano na mataifa hayo, kipindi cha kuwakaribisha ndugu zetu waliotutangulia kutumia lugha ya Kiswahili, kuna umuhimu mkubwa wa kuzingatia na kuweka hadharani umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika maendeleo ya mataifa yote ya jumuia ya Afrika ya Masharika, hasahasa Taifa la Rwanda. Miongoni mwa rasilimali za Rwanda, Kiswahili kimeongezeka kama rasilmali mpya ya kuwezesha wanyarwanda kuingia kwenye zile semehemu za ndani mwa Afrika ya Mashariki, pale ambapo Kiingereza hakiwezi kutufikisha! Kiswahili kina uwezo mkubwa wa kuchangia katika maendeleo ya taifa letu katika maendeleo ya jamii hiyo, yakiwa ya kiuchumi, kijamii kisiasa na

kielumu. Kukuza, kuratibu na kueneza lugha ya Kiswahili katika sekta mbalimbali za nchi yetu ni mojawapo ya njia muhimu za kutufikisha kwa maendeleo ya kudumu.

Kiswahili, Linguistic Theory, Language Practices, and Development Revisited

Peter Mose

pmose61@yahoo.com

Kiswahili, in spite of actual and perceived challenges, bears the potential to be the language of socio-cultural and economic development in not only East Africa but also in Eastern Africa. Post 2015 and sociolinguistic trends indicate that Kiswahili may cease to be grouped as among the ordinary multiple African languages that characterize the African population. The purpose of this article is to explore linguistic theory, language practices and how these two project Kiswahili as the language of future Eastern Africa education systems. Data for this article are from literature review and observations of language trends i.e. classrooms, public offices, and other extra-formal contexts. The article suggests that theoretically, Kiswahili satisfies conditions of being a premier language of all aspects of development in East Africa. Secondly, evidence suggests that language patterns in various contexts in this region point to growing potential of the language. This further indicates that Kiswahili will, inevitably, for instance take a central position in future language-in-education planning and policies-acquisition planning provides a platform of language growth. With its inroads to such countries as Democratic Republic of Congo, Malawi, Southern Sudan, etc, there is a further possibility that Kiswahili may become not only one of the key African lingua francae but also a language with more sociolinguistic possibilities.

Key words: Kiswahili, theory, practices, education.

Sanaa kama kazi na biashara kueneza Kiswahili

Phibbian Nancy Muthama
Multimedia University of Kenya
muthamaphibbian@gmail.com/mphibby@gmail.com

Sanaa ni utanzu katika fasihi ambao ndio kipengele pekee kinachoeneza kiswahili kwa kazi mno.Sanaa(ushairi)ndio iliofanya kiswahili kitambulike,waswahili na mila zao,itikadi,desturi,na dini kufahamika.sasa lugha yetu ya Afrika inatambulika ulimwengini kwa sababu ya Sanaa.na sasa nimekuwa kazi na biashara kama zile zingine Kueneza lugha yetu ya Afrika. Tutasema zaidi katika jopo namna gani Sanaa inakuwa kazi na biashara na has a kuendeleza na kueneza Kiswahili.

Nafasi ya Kiswahili katika mabadiliko ya kanda

Prisca Jerono
Chuo Kikuu cha Nairobi

Prisca1jerono2@gmail.com

Jumuiya ya Afrika Mashariki iliundwa ili kuleta na kuimarisha umoja wa kiuchumi, kisiasa na kijamii baina ya nchi wanachama.Lengo hili lilitazamiwa kufikiwa kupitia kwa mikakati mbalimbali. Moja wapo ya mikakati ni mawasiliano. Ili kuwezesha mawasiliano ya pamoja jumuiya ya Afrika Mashariki iliteua Kiswahili kama lugha mawasiliano baina ya nchi wanachama. Kuteuliwa kwa Kiswahili kulihitaji mikakati ya kuimarisha matumizi ya yake. Ni kwa sababu hii ndipo Tume ya Lugha ya Kiswahili iliundwa ili kutekeleza ajenda hii kupitia kwa utafiti, elimu, ufundishaji na uendelezaji wa lugha. Tume hii imepiga hatua katika maendeleo ya Kiswahili kwa kupendekeza Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Jumuiya ambapo pendekezo na sheria ya kuidhinishwa kwake bado linasubiri uidhinishwaji rasmi wa viongozi wa mataifa haya. Hata hivyo, imeonekana kuwa tendo la kuidhinishwa kwa lugha kuwa rasmi katika hali nyingine hakuchochei mabadiliko katika matumizi ya lugha. Hali hii kwa mfano inaonekana nchini Kenya ambapo kwa kiwango kikubwa shughuli zote za kiserikali na kibiashara bado zinaendeshwa katika Kiingereza licha ya Kiswahili kuidhinishwa kama lugha rasmi kikatiba. Ni kwa sababu hii ndipo makala hii inajaribu kuangazia nafasi ya Kiswahili katika Jumuiya na katika vyombo vya habari na changamoto zinazokabili matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na lugha mawasiliano na jinsi changamoto hizo zinavyoweza kukabiliwa ili kuendeleza matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kuleta mabadiliko katika kanda hii.

Kiswahili na Upatikanaji wa Rasilimali

Privat Nibaruta
Wizara ya Elimu , Elimu ya Juu
Na utafiti wa Sayansi nchini Burundi
Ofisi ya Utungaji na Uchunguzi wa
Mitalaa.
privatnibaruta@gmail.com

Ushahidi wa kihistoria unathibitisha kuwa lugha ya Kiswahili ilizungumzwa katika upwa wa Afrika Mashariki hata kabla ya ujio wa wageni kama vile warabu na wazungu. Baada ya kuwa lugha husikika na kutumiwa katika nchi ni dhahiri kwamba ongezeko la watu wanaotumia lugha yenyewe linakomaa kiasi cha kuvuka mipaka ya awali . Kiswahili kilichangia pia kinachangia kwa kiasi kikuu kupatishia rasilimali watumiaji wa lugha hiyo. Wafanyabiashara wakiarabu walianza kuimarisha biashara ya masafa marefu ya pembe za ndovu na watumwa katika maeneo ya bara wakitumia kiswahili kama chombo cha mawasiliano. Kwa muda huu , lugha ya Kiswahili inatumika kama lugha ya mawasiliano katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki au katika bara .Kutokana na raia wengi kusisitiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli za biashara, rasilimali huongezeka kwa kiwango cha kutosha. Rasilimali si biashara tu, Kiswahili kinatumika kwa kuelimisha jamii au kueneza dini kama walivyofanya Warabu na Wazungu bila kusahau utekelezaji wa utawala wa demokrasia.

Ujasiriamali wa Kike: Mifano kutoka Riwaya za Kiswahili

Rachel Maina
Chuo Kikuu cha Kenyatta

Rachelmaina374@gmail.com

Lugha ya Kiswahili ni lingua franka ya Afrika Mashariki na Kati. Imetumika katika mawasiliano katika nyanja za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Inatumika katika biashara kote katika eneo la Afrika Mashariki; eneo ambamo wanawake wamejifunga kibwebwe wakishirikiana na wenzao wanaume kukabiliana na changamoto anuwai za kiuchumi zinazoikumba jamii. Wajasiriamali wa kike wamethibitisha kuwa wanamudu biashara ndogo na hata kubwa. Uwezo wao wa kijasiriamali unadhihirika katika kuthubutu na kuvumbua ambako huchangia juhudi za mataifa yao mbalimbali kushiriki katika soko la ulimwengu. Jitihada za wajasiriamali hawa hazikuwapita waandishi wa kazi za kiubunifu za Kiswahili. Ujasiriamali wa wanawake umeangaziwa katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Makala haya yataangazia namna ujasiriamali wa wanawake umesawiriwa katika riwaya ya Kiswahili; changamoto wanazokumbana nazo na namna wanazikabili na kuibuka washindi. Kazi zitakazotumika ni mbili; NYUSO ZA MWANAMKE ambayo ni riwaya ya S. A. Mohamed na KALA TUFAHA ya Omar Babu. Mohamed ni Mtanzania ilhali Babu ni Mkenya. Ni matumaini yetu kuwa matokeo ya utafiti yataonyesha uhodari wa wajasiriamali wa kike na uwezo wa waandishi katika kuchora jamii kama ilivyo; katika uhalisia wake.

Uchambuzi wa Mashairi ya kisiasa ya Lamu

Rayya Timammy
rayyat@yahoo.com

Kote ulimwenguni wakati wa kipindi cha uchaguzi na hasa uchaguzi mkuu, wanasiasa hutumia ushairi na nyimbo kuvuta akili au fahamu na hisia za wapiga kura. Hivyo kwa miaka mingi, mashairi yametumiwa kama njia ya kuwasilisha jumbe za kisiasa ambazo zinaweza zikawa ni nzuri au mbaya kwa makundi tofauti ya kisiasa. Mashairi hayo yamekuwa njia ya kupitisha jumbe za kisiasa ambazo zisingewasilishwa katika lugha ya kawaida ya kisiasa au hotuba. Mbali na kuwa na ujumi au mitindo inayovutia, mashairi haya ni kifaa muhimu ambacho kinatumika kuchanganulia maswali ya kisiasa na kijamii yanavyojitokeza na jinsi yanavyoeleweka na jamii. Kuelewa maana halisi au hasa iliyokusudiwa kunahitaji ufasiri wa sawasawa na wa kimantiki wa lugha pamoja na muktadha ili kuuelewa ujumbe wake vilivyo. Hii leo kuwepo kwa mitandao ya kijamii kumeyafanya mashairi haya ya kisiasa kuenea kwa haraka na kuifikia hadhira pana. Lengo la makala haya ni kuyachunguza mashairi haya ya kisiasa yanayopitishwa kwa njia ya mitandao ya kijamii na kuyachambua kwa upande wa lugha, muktadha wayo na kuonyesha umuhimu wa vipengele hivi viwili katika kupitisha ujumbe wa mashairi yenyewe. Tutajifunga zaidi na mashairi yanayotungwa kuhusu siasa za kaunti ya Lamu.

Sayansi bunilizi kama msingi wa kuimarisha mielekeo ya Sayansi na Teknolojia katika Kiswahili

Richard Makhanu Wafula
Chuo Kikuu cha Kenyatta

rnamwinguli@gmail.com

Makala hii inanuia kufafanua jinsi sayansi bunilizi ya Kiswahili inavyoweza kuwa msingi wa kuimarisha mitazamo na mielekeo ya kisayansi na kiteknolojia katika lugha ya Kiswahili. Pamoja

kuwa kisima cha ujenzi wa msamiati wa kisayansi na teknolojia, sayansi bunilizi inaweza kupeana motisha kuhusu majaribio yatakayoleta uvumbuzi mpya. Kwa kutumia machapisho kama Kusadikika (shaaban Robert), Babu Alipofufuka (S.A. Mohamed), Walenisi (Katama Mkangi) na Bin-Adamu! (Wamitila), makala itaonyesha namna ambavyo inaweza kuhamasisha uvumbuzi na utendakazi wa uvumbuzi huo katika lugha ya Kiswahili.

Mchango wa vyombo vya habari na wanahabari wa Kiswahili Burundi kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili na Muungano wa Jumuia ya Afrika

Riziki Jacob

jacobriziki@yahoo.com

Kiswahili kama lugha ilianza kabisa kutambulika Burundi miaka ya 1880 enzi za utawala wa mfalme wa Burundi Mwami Mwezi Gisabo baada ya waarabu kujitokeza mwambao wa ziwa Tanganyika na bonde la Rusizi. Kwa upande wa vyombo vya habari lugha ya kiswahili ilianza kutumiwa kwa mara ya kwanza kabisa mwaka 1954 katika redio ya taifa (RTNB). Kipindi hicho kilikuwa ni kipindi cha harakati za uhuru na Kiswahili kilitumika kama lugha ya kiafrika kwa lengo la kujikomboa. Kipindi hiki redio ya taifa ilianza kupeperusha nyimbo za kiswahili ambazo zilikuwa na ujumbe wa kuamsha Waafrika kujikomboa na kufukuza wazungu. Baada ya uhuru Burundi ilianza kujitegemea kiuchumi kisiasa na kiutamaduni. Kwa kuzingatia Jiografia, Burundi ililazimika kujiunga na jumuia za kikanda na kufungua milango pia kwa lugha za kikanda. Sambaba na vipindi vya Kiswahili redio ya taifa iliendelea kupeperusha miziki ya kiswahili yenye midundo ya kiafrika. Miziki ya Zaire, Tanzania na Kenya diyo ilinyakua soko Kiswahili Burundi. Miaka ya 1990 zilipoingia harakati za utawala wa kidemokrasia, redio na runinga binafsi zilifungulia na zilipeperusha matangazo ya Kiswahili. Kwa kuzingatia michakato yote ya maisha ya wananchi na taifa, wanahabari wa Kiswahili Burundi wamekuwa ni nyenzo rahisi na mashine tata za kusukuma gurudumu la umoja wa warundi na miungano ya kikanda katika Afrika mashariki, kati na pembe ya Afrika.

Kiswahili, Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi

Rocha Chimerah
Chuo Kikuu cha Pwani
rocha.chimerah@yahoo.com

Inadaiwa kuwa Kiswahili ni baina ya lugha saba na kumi na tano kubwa zaidi ulimwenguni. Ukubwa wake umo katika usambazi wake kwa kasi sana katika maeneo yake ya jadi; yaani Afrika ya Mashariki na Kati, na sasa takriban ulimwengu mzima. Inasemekana Kiswahili katika hii karne ya 21 kina wasemaji zaidi ya milioni mia moja hamsini, na bado tu kinazidi kupanuka. Kwa hili, imedaiwa kuwa ndiyo lugha ya pili baina ya lugha zote ulimwenguni kusambaa kwa haraka zaidi; nyuma tu ya Kihispanyola. Tatizo kubwa dhidi ya mapanuzi haya ni jinsi ulimwengu ulivyobadilishwa na unavyoendelea kubadilishwa na mavumbuzi mapya kila uchao katika Nyanja za sayansi, teknolojia na vitumeme. Mavumbuzi haya huwa yanaandamana na istihali mpya mpya ambazo aghalabu huwa ni za lugha ya wavumbuzi ambayo, katika enzi hizi, ni lugha ya Kiingereza au lugha nyinginezo zenye chimbuko moja nayo. Hapo ndipo Kiswahili kinapojikuta katika udhaifu wake mkubwa. Udhaifu huu unaweza kurekebishwa na wanaisimu kutohoa maneno hayo yote na kuyatia katika matamshi na umbo la Kiswahili, au kubuni istilahi mpya kwa takriban kila

dhana mpya moja kwa moja kutoka lugha ya Kiswahili na kuziingiza katika lugha yenyewe ilimradi kikinawirisha, kukikwasisha na kukirasmisha kama lugha ya kimataifa yenye kustahiki sifa hiyo. Ikiteuliwa mbinu ya utohozi, haitachukua muda Kiswahili kitafanana na lugha ya kizungu kuliko lugha yo yote ya Kiafrika. Mbinu ya pili ina nafasi kubwa ya kukinusurisha kutokana na janga hili, ambalo tayari lishaikumba lugha hii awali kilipokutana na Kiarabu, mkutano ambao ulikujafanya idaiwe kuwa Kiswahili ni lahaja mojawapo katika lahaja za Kiarabu, au ni mchanganyiko wa Kibantu na Kiarabu; yaani ni pijini. Ni wazi basi kuwa, ili kukiepushia madai ya aina hii na kuwafanya wasemaji wake wadharauliwe au wapuuzwe, hakuna budi ila kuipanua lugha yetu adhimu kutokana na misingi ya uthabiti wa mizizi yake. Hii tayari ishafanyika pale istilahi kama vile runinga, barua pepe, mangala (Nabhany) na tarakilishi, tovuti, wavuti, taarasha (Chimerah), baina ya nyinginezo zilipobuniwa. Hii ndiyo mbinu inayofaa kuendelezwa na kuboreshwa.

Fikra ya Mapenzi Maudhi: Mifano kutoka katika Riwaya ya *Nyota ya Rehema*

Salma Omar Hamad
Chuo kikuu Huria cha Tanzania
mamamaya@yahoo.com/salma.hama

Mapenzi na maudhi ni kama watoto pacha waliogand@out.ac.tzana. Hakuna uwezekano wowote wa kumpata pacha mmoja na kumkosa mwenzake. Ingawa kila mmoja katika ulimwengu anadai kupenda na/au kupendwa, bado mapenzi hayajatupiwa jicho la ndani zaidi na la kiudadisi. Watu wengi huyaangalia mapenzi kijuujuu na kuyahusisha na starehe, furaha, maliwazo, burudani na hata mafanikio. Makala hii inakusudia kuchunguza fikra ya ‘mapenzi ni maudhi’ kama inavyojitokeza katika riwaya ya ***Nyota ya Rehema*** ya Mohamed Suleiman. Uhalisia unaonesha kwamba kila dhana ya mapenzi inapojitokeza haiachi kuambatana na dhana ya maudhi. Maudhi yatokanayo na mapenzi humfika mwenye kupenda, mwenye kupendwa, jamii inayowazunguka wanaopendana na hata Mungu.

Nafasi ya Kiswahili katika Uhamasishaji na Ushirikishaji wa Umma kwa Ujenzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Sangai Mohochi
Chuo Kikuu cha Rongo

mohochis@ruc.ac.ke

Malengo ya mipango na mikakati yoyote ya maendeleo ni kuleta mabadiliko yanayoboresha hali ya maisha katika jamii. Kwa maana hiyo, fanaka ya mipango na mikakati hiyo hupimwa, hatimaye, kutokana na kiwango cha athari yake katika maisha ya binadamu waliolengwa. Hii ndiyo sababu maamuzi kuhusu maswala haya hutarajiwa kufanywa kwa makini, na kwa kuzingatia yaliyotokea katika sehemu nyingine za dunia awali. Ni wazi basi kuwa ni vyema kuwahusisha walengwa katika hatua za maandalizi na za utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali inayoamuliwa. Isitoshe, kushirikishwa kwa wahusika mbalimbali kunatoa mchango mkubwa katika hatua zote

zinazochukuliwa ili kufikia lengo kuu. Aghalabu maamuzi yanapofanywa na viongozi na kutekelezwa na wafanyakazi waliopewa jukumu hilo na viongozi, bila kuhusisha wahusika wakuu, matokeo hayawi mazuri. Makala hii, imelenga kuchunguza haya katika muktadha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Je, ni kwa kiwango gani mipango na mikakati mbalimbali ya ujenzi wa Jumuiya hii imewahusisha wananchi wa nchi wanachama? Wananchi wa kawaida wamehamasishwa na kushirikishwa vipi ili kuiona Jumuiya kama milki yao na hivyo kujitolea kushiriki katika ujenzi wake? Lugha ya Kiswahili imetekeleza jukumu gani katika hali hii? Na labda muhimu zaidi ni kuwa makala hii itajaribu kupendekeza jinsi Kiswahili kinaweza kuchangia zaidi katika kuhakikisha kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki si ya viongozi katika makongamano na maofisi bali ni ya wananchi.

Nafasi ya kuimarika na kutanuka kwa Lugha ya Kiswahili kama kitakuwa Lugha ya kufundishia katika Afrika Mashariki.

Sarah Ndanu Mwangangi Ngesu
Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya

sarahngesu@gmail.com

Lengo la makala haya ni kujadili nafasi ya kuimarika na kutanuka kwa lugha ya Kiswahili kikiteuliwa kuwa lugha ya kufundishia katika Afrika Mashariki. Lugha ya taifa inapotumiwa katika elimu, teknolojia na utawala huwa ni fahari kuu kwa taifa husika. Katika nchi zilizo “huru”, lugha inayozungumzwa na wananchi wengi ndiyo hutumiwa katika elimu(kufundishia) ambayo huwawezesha wanafunzi kuwa wabunifu, wagunduzi na huzungumza na mioyo yao pamoja na akili zao.Kila jamiilugha hupendelea kuona lugha yake ikikua na kuenea kutoka hatua moja hadi nyingine (kitaifa hadi kimataifa). Kuna ukuruba mkubwa kati ya lugha, elimu, saikolojia na sosiolojia. Kielimu mwanafunzi hujifunza haraka kupitia lugha anayoielewa vyema kuliko lugha ngeni.Kisaikolojia lugha za asili ni mfumo wa alama zenye maana ambazo katika akili ya mwanafunzi hufanya kazi haraka katika kujieleza na kuelewa. Kisosiolojia lugha ya asili ya mtu ni njia ya kujinasibisha na jamii yake. Kiswahili ni lugha rasmi ya Umojawa Afrika (AU) na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miongoni mwa lughaza kimataifa, Kiswahili kina hadhi ya nafasi ya sita. Aidha, Katika Afrika Mashariki Kiswahili huzungumzwa na takribani watu milioni 100. Kwa hivyo Kiswahili ni lugha ya asili ya wananchi wa Afrika Mashariki. Uteuzi wa lugha ya Kiswahili kufundishia katika viwango vyote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutaipa lugha hii jukumu na mfumo wake wa kiisimu utapanuka ili kukidhi haja za mawasiliano ya kilataaluma.

Utumizi wa kongoo katika ufundishaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili

Seleman S Sewangi
BAKITA
sewangi@hotmail.com

Utumiaji kongoo katika kusaidia ufundishaji lugha na fasihi ya Kiswahili ni jambo geni kabisa kwa waalimu wengi, kama sio wote. Bado ufundishaji wa taaluma hizi ni wa kimapokeo ambapo mwanafunzi humtamzama mwalimu kama chanzo kikuu cha data na maarifa huku mwanafunzi akichukuliwa kuwa mpokeaji wa wa mbambo hayo kutoka kwa kwa mwalimu wake. Mkabala huu wa ufundishaji lugha na fasihi yake unabadilika kwa kasi katika nchi zilizoingiza matumizi ya

kongoo ya kikompyuta katika ufundishaji wa taaluma hizi. Ufundishaji wa aina hii, tofauti na ule wa kimapokeo humpa mwanafunzi nafasi ya kujifunza kwa kudadisi na kugundua mambo mbalimbali kutokana na data halisi ya lugha inayopatikana kwenye kongoo. Ugeni wa makabala huu wa ufundishaji katika Kiswahili unatokana na sababu anuai, mojawapo ikiwa ni ukosefu wa ulewa wa namna ufundishaji huu unavyofanywa. Lengo la makala haya ni kujaribu kutoa mwanga kuhusu mahitaji na mbinu za kutumia mkabala wa kongoo katika kufundishia lugha na fasihi ya Kiswahili.

Kiswahili katika Muziki wa Hip Hop na Bongo Fleva na Mchango wake katika Kuleta Mabadiliko kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Shani Omari
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
shaniom@yahoo.com

Lengo la makala hii ni kujadili mchango wa muziki wa Hip hop na Bongofleva kutoka nchini Tanzania katika kuendeleza Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuleta mabadiliko faafu katika nchi hizo. Muziki huu, ingawa asili yake ni Afrika, uliingia nchini Tanzania miaka ya 1980 kutokea Marekani. Muziki huu hapo mwanzoni ulipoingia nchini ulianza kuimbwa kwa Kiingereza na baada ya miaka kadhaa ukaanza kuimbwa kwa Kiswahili. Kwa hivi sasa Kiswahili ndio kimetamalaki katika uimbaji wa nyimbo hizo ingawa Kiingereza pia kinatumika kwa kiasi kidogo. Umaarufu wa muziki huo unapatikana ndani na nje ya Tanzania. Makala hii basi inachunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nyimbo za muziki huo yanavyoweza kuchangia katika kuleta mabadiliko na maendeleo katika nchi wanachama za Afrika Mashariki kiutamaduni, kiuchumi, na kisiasa. Data za makala hii zimekusanywa kwa kusikiliza mashairi ya muziki huo, kutazama video zake, kusoma kazi mbalimbali tangulizi na kufanya mahojiano na wadau mbalimbali wa muziki huu nchini Tanzania. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba, mbali na changamoto mbalimbali za muziki huu, muziki huu una dhima kubwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutokana na matumizi yake ya lugha ya Kiswahili.

Nafasi ya Kiswahili katika kuimarisha uelewa wa Masuala ya Kiafya kwa minajili ya kukuza taifa lenye siha bora

Sheila Pamela Wandera-Simwa
Chuo Kikuu cha Laikipia
sheiwande@gmail.com

Mojawapo wa Malengo endelevu ya maendeleo yaliyopitishwa na umoja wa mataifa katika mwaka wa 2015 ni uimarishaji wa afya kupitia kujua kusoma na kuandika ambako kunahusisha masuala ya lugha tumizi. Siha njema ni adhimu kwa maendeleo ya taifa lolote lile. Ili taifa liwe na siha toshelevu, sharti wananchi wake wawe na uelewa mwafaka wa masuala ya kiafya ili waweze kuyakuza miongoni mwao. Lugha basi inakuwa kiungo muhimu cha kutekeleza hitaji hili la siha bora. Kiswahili kama Lingua Franka ya jumuiya ya Afrika Mashariki haina budi kuchukua jukumu hili kwani ndiyo lugha tu inayounganisha nchi hizi, na basi ndiyo inayoweza kuleta utangamano miongoni mwa wananchi wake, hasa wakati huu ambapo nchi hizi zinazingatia ubadilishanaji wa wataalamu katika nyanja mbalimbali za maisha ili kuthibiti mahitaji ya kikanda yanayoendana na mabadiliko ya maisha kwa jumla. Katika nyanja ya afya, lugha mwafaka inayotarajiwa

kuwawezesha madaktari na wahudumu wote wa taasisi za afya kuweza kuhudumu katika nchi yoyote manachama, bila vikwazo vingi ni Kiswahili. Vivyo hivyo, inatarajiwa kuwa wagonjwa kutoka nchi hizi wanaweza kupata matibabu yao kutoka hospitali zozote katika nchi wanachama kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Makala hii itahakiki nafasi ya Kiswahili katika masuala haya ya kiafya; hali ilivyo sasa; vikwazo vilivyoko; na kujaribu kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na hali hii, ili katika kuleta utangamano wa kikanda, pia Kiswahili kiweze kufanikisha lengo la afya la maendeleo endelevu. Data ya makala hiii itakusanywa kutoka hospitali kuu ya mkoa iliyoko Nakuru mjini, nchini Kenya.

Nadharia ya Lugha Mbadala Amilifu na Mchango wake katika Uamiliaji wa Lugha ya Pili.

Silas Odhiambo Owala
Chuo Kikuu cha Maasai Mara
oowala2000@yahoo.com au owala@mmarau.ac.ke

Katika nchi nyingi hali ya lugha ni wingi lugha mbapo watu huzungumza lugha tatu au zaidi. Hata hivyo, uchunguzi umeonyesha kwamba licha ya uwepo wa lugha hizo nyingi, kuna namna ambavyo watu huamua kuzingatia lugha fulani na kupuuza zingine au hata wakijifunza hawaonyeshi nia ya kuzimilisi namna wanavyo milisi zingine. Katika miaka iliyopita watafiti wengi wamefikia uamuzi kwamba sababu inayochangia hili ni swala la mwelekeo. Ingawa mwelekeo huweza kusababisha hali hiyo, makala haya yanahoji dhana hii na kujadili haja ya kufikiria jambo hili kwa njia mpya kabisa. Kwamba huenda kutooonyesha nia ya kumilisi lugha hizo hutokana na uwepo wa lugha mbadala amilifu. Dhana ya mbadala amilifu ni dhana katika uwanja wa biashara. Dhana hiyo hueleza hali ambayo iwapo kuna bidhaa mbadala katika soko basi wananunuzi hawana haja ya kutafuta bidhaa mahususi na kwa hiyo thamani ya bidhaa hiyo kupungua. Naona kwamba nadharia inaweza kuibuliwa kutokana na dhana hii ili kueleza sababu za watu kuamili lugha zingine kwa urahisi na kupuuza zingine. Napendekeza kuwaalika wataalamu kujadili nadharia mpya iitwayo **Nadharia ya lugha mbadala amilifu** (Functional alternative language theory) kama kigezo muhimu cha kueleza uamiliaji wa lugha ya pili miongoni mwa jamii zenye wingi lugha

Teaching Extended Piano Techniques with Turkish Piano Repertoire

Şirin Akbulut Demirci
Department of Music Education, Faculty of Education, Uludag University Bursa, Turkey.
akbulut.sirin@gmail.com/sakbulut@uludag.edu.tr

This study was searched Turkish piano repertoire and detected the compositions, was composed by using extended piano techniques. All techniques were organized by tabulating. The research questions are which compositions for solo piano were composed using extended piano techniques in Turkey? How can the repertoire tabulate according extended piano techniques? How can be this material used in piano education?. For first two research questions descriptive study was made and for the last research questions teacher piano performers were interviewed with semi-structured questions and results were analyzed with N-Vivo 11 Qualitative research program. It was thought

and purposed that extended piano repertoire should be used more widespread by the results of this study and take place in piano curriculum.

Key words: Piano education, extended piano repertoire, Turkey, Turkish piano literature

Kiswahili, Biashara na Kazi

Sophie Okwena
Chuo Kikuu cha Kenyatta
sophiejoyedwin@gmail.com

Makala hii itaangazia mchango wa Kiswahili katika nyanja za biashara na kazi katika jumuiya ya Afrika Mashariki. Kiswahili ni chombo muhimu cha mawasiliano na maingiliano ya watu wenye tamaduni tofauti katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Dhana ya kuwa na lugha moja sawa miongoni mwa jamii katika jumuiya ni wazo ambalo linafaa kupewa kapaumbele ikichukuliwa kwamba, dunia imekuwa kama kijiji kidogo. Kiswahili ni lugha ambayo huzungumzwa na makabila mengi ambayo huishi sehemu ya Afrika Masharika na hata Kusini kama vile; Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Msumbiji. Aidha, Kiswahili ni lugha ya taifa au rasmi katika nchi hizo na ni lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia, Kiswahili ni lugha shawishi kisiasa, kiuchumi na hata kijamii na ufahamu wayo utarahisisha uhusiano wa kibiashara na kazi. Lugha ya Kiswahili imejulikana kama lugha ya utambulisho katika jumuiya ikiwa mojawapo ya lugha chache za Kiafrika ambazo huzumgumzwa ulimwenguni kote. Aidha, ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi mno. Lugha ya Kiswahili ikiwa lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, inafaa kutumika katika shughuli za kibiashara na kazi ili kuwezesha mchakato wa kuiunganisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kiswahili ni lugha-mawasilano (lingua franca) katika Afrika Mashariki. Lugha hii kwa sasa imevuka mipaka ya jamii yake ya Waswahili na sasa inatumika na watu wote wa Tanzania, asilimia kubwa ya Wakenya na kiwanga cha kuridhisha nchini Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kufuatia kuanzishwa kwa sera ya masoko huria, kuna mwamko wa wananchi wa jumuiya kujitokeza katika kufanya shughuli za kibiashara. Kwa sasa kuna haja ya kuwafikia, kuwahamasisha na kuwaunganisha watu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili waone haja ya kukuza na kuendeleza Kiswahili katika shughuli za biashara na kazi. Kunafaa kuwe na ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika ili kuwezesha kufungua milango mingi ya ushirikiano katika nyanja za biashara na kazi. Kadhalika, kuwe na azma ya kuwa na mipaka huru baina ya nchi husika, sarafu moja, soko la pamoja la bidhaa n.k. Mazingira kama hayo yatafanya maingiliano baina ya watu wa jumuiya kuwa makubwa zaidi hasa kwenye nyanja za biashara na kazi. Waaidha, mazingira kama hayo yataafikiwa zaidi kama Kiswahili kitatiliwa maanani katika nchi hizi. Serikali kutoka nchi husika pia zinafaa kuwekeza zaidi katika kupanua matumizi, ukuaji na uelewa wa Kiswahili katika jumuiya yetu.

Sauti ya Wamakunduchi

Suleiman Haji
na
Yassin Salim Mussa
Chuo Kikuu Cha Kiislamu Uganda

Nyimbo ni chombo muhimu ambacho hutumiwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Katika tamaduni za Watanzania sherehe mbalimbali huhusisha nyimbo za kitamaduni. Visiwani Zanzibar nyimbo za ***Mwaka Kogwa*** za Wamakunduchi si tu kuwa zimekuwa zikilitangaza taifa Tanzania nje ya mipaka yake, lakini pia ni kibebeo cha kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kila uchao. Jimboni Makunduchi, sherehe za ***Mwaka Kogwa*** huadhimishwa kitaifa. Kwa ushawishi uliomo katika nyimbo za ***Mwaka Kogwa,*** wageni wengi humiminika minaajili ya kujifunza lahaja hiyo ilivyosheheni mila za Wamakunduchi na misamiati endelevu ya lugha ya Kiswahili. Ni kwa mwegemo huo ambapo makala haya yamechanganua nyimbo za ***Mwaka Kogwa;*** ambapo kwa ufahima wa watafiti ni kwamba nyimbo hizo hazijawahi kutafitiwa hususani kuhusu ushawishi uliomo. Kwayo, watafiti wamejikita katika kubainisha maudhui na mitindo mahususi inayowapelekea wenyeji na wageni kushawishika kuhusu nyimbo hizo za ***Mwaka Kogwa*** kila uchao; hata ikapelekea serikali kuziona ni tunu ya lugha ya Kiswahili na kwa hivyo kuadhimishwa kitaifa. Makala haya yameongozwa na nadharia ya uamilifu ambapo nadharia tete zake ni: (a) Nyimbo za ***Mwaka Kogwa*** zina maudhui gani mahususi? (b) Nyimbo za Mwaka Kogwa zina mitindo gani iliyopelekea kushawishi hadhira? (c) Nyimbo za ***Mwaka Kogwa*** zina athari gani mahususi kwa hadhira? Fauka ya hivyo, data ya utafiti ilikusanywa kwa mbinu ya upekuzi na mahojiano; na kuchanganuliwa kithamano na kiwingiidadi.

Maneno muhimu: *Nyimbo za Mwaka Kogwa, Kiswahili*

Kiswahili kama Lugha-Chombo, Lugha-Jamii na Lingua Franka katika Afrika Mashariki

Susan C. Choge
Chuo Kikuu Cha Masinde Muliro cha Sayanasi na Technolojia
schoge@mmust.ac.ke/susanchoge@gmail.com

Kiswahili ni lugha ambayo imepewa nafasi kubwa katika maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ndani na nje ya Afrika Mashariki. Tangu enzi za wafanyi biashara na wainjilistic mwambao mwa pwan mwa Afrika Mahsariki na baadae wakati wa ukoloni na baada ya uhuru, Kiswahili imetekeleza majukumu mengi kama lugha-chombo, Lugha-jamii na lingua franka. Makala hii inalenga kuchunguza nafasi ya Kiswahili katika utatu huu tangu katika Afrika mashariki tangu miaka ya 1960 wakati nchi za Afrika Mashariki zilipopata uhuru. Makala hii itatekemea data ya kimaktaba na kuongozwa na nadharia ya mifumo changamano.

Research and Innovation Management in Burundi in the context of EAC Integration Process: An Overview

Tatien Masharabu
University of Burundi
tatien.masharabu@ub.edu.bi

In the aim of boosting the sector of Research, Science, Technology and Innovation (STI), Burundi has put in place laws and institutions. This paper documented the enabling environment, related programmes under way and challenges. The enabling Environment includes among others Policy Framework and ICT Infrastructure being put in place. The Fibre-optic project is currently running to provide ICT infrastructure across the country alongside development of the Burundi Backbone System (BBS). In the area of research and STI, the country developed and adopted a National

Policy on Scientific Research and Technological innovation (STI Policy) document in June 2011. The policy outlines various actions that the Government of Burundi intends to undertake in order to ensure that R&D and innovation activities are adequately funded. Its implementation framework 2014-2018 was launched in August 2014. As STI are universally recognized as powerful drivers for socio-economic development, Burundi is in the process of setting up a National Commission for STI with the goal of developing and valuing the national potential. In terms of communication tool, most of all these policy documents are drafted in French. Their translation in Kiswahili (and in English as well as in Kirundi) should therefore be undertaken in order to facilitate, on one hand, their exploitation at national and regional level, and on another hand, implementation at national level. Collaborations at different levels should address issues related to the above priorities as the country lacks a dedicated mechanism for funding R&D and innovation.

Dhima ya Kiswahili katika Uendelezaji wa Biashara ya Kisasa

Timothy Kinoti M'Ngaruthi
University of Embu, Kenya
kinoti67@gmail.com/mngaruthi.timothy@embuni.ac.ke

Maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kiasi kikubwa hutegemea maendeleo katika sekta ya biashara. Kwa upande mwingine, sekta ya biashara huitegemea sekta ya mawasiliano ili kufikia malengo yake. Hii ni kwa sababu biashara hushirikisha wahusika wawili wakuu, yaani mfanyibiashara na mteja wake. Kufanikiwa kwa biashara yoyote hutegemea maafikiano kati ya wahusika hawa kuhusiana na bidhaa au huduma zinazotolewa. Hata hivyo, maafikiano haya yatakwama iwapo lugha inayotumiwa haitaeleweka na wahusika wote. Makala haya yananuia kubainisha nafasi ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa katika uendelezaji wa biashara ya kisasa kote ulimwenguni hasa kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mtazamo kadirifu wa kifeministi na nafasi yake katika Mfungamano na Maendeleo ya kijamii

Titus Kaui

kauititus@gmail.com

Fasihi andishi ya Kiswahili imepiga hatua kubwa za kimaendeleo tangu kufikishwa kwake Afrika Mashariki na wanasanaa wa Kizungu. Baadhi ya maendeleo yaliyopigwa ni pamoja kuhulutishwa kwa mitazamo ya kinadharia ya kigeni na ile asilia katika utungaji na uhakiki wake. Miongoni mwa mitazamo ya kinadharia maarufu katika utungaji wa tungo za fasihi ya Kiswahili ni ufeministi. Ufeministi umetumika sana na watungaji kwa madhumuni ya kushambulia asasi za kijamii za Kiafrika ambazo zimekuwa zikiendeleza udhalilishaji wa wanawake. Maoni ya watungaji wengi wanaoshikilia mtazamo wa kifeministi ni kuwa asasi zinazoendeleza unyanyasaji wa jinsia ya kike zimechakaa na kupoteza umuhimu wake katika jamii. Hii ndio maana baadhi yao wanahimiza wanawake waasi ndoa na kupinga mafundisho ya dini yanayomdunisha mwanamke. Licha ya kwamba jamii ya sasa imepitia mabadiliko mengi hasa katika mahusiano ya kijinsia, baadhi ya waandishi wa fasihi ya Kiswahili wangali wanaendeleza mitazamo ya kale ya kifeministi ambayo inashindwa kutambua maendeleo yanayoafikiwa kila uchao katika harakati za kifeministi.

Mtazamo halisia wa kifeministi unapaswa kwenda na wakati na kuangazia mafanikio na changamoto zilizopo. Kuna haja ya kuhakiki mitazamo ya watunzi wa kike na wale wa kiume wanaotunga kwa misingi ya kifeministi ili kubainisha udhaifu uliopo na kupendekeza mtazamo kadirifu. Fasihi ina dhima muhimu ya kuelekeza jamii kwa masuala mbalimbali, na kuwapo kwa mitazamo mikali ndani yake kunaweza kusababisha vurugu za kijamii na hivyo kusambaratisha ufungamano na maendeleo ya kijamii. Makala hii inachunguza nafasi ya mtazamo kadirifu wa kifeministi katika uendelezaji wa mfungamano wa kijamii na maendeleo.

Lugha Mwiko, Tasfida na Athari zake katika Mtandao wa Facebook

Toboso Mahero Bernard na Mosol Kandagor

Chuo Kikuu cha Moi

markkandagor@yahoo.com

Tamaduni nyingi za ulimwengu zijajulikana kwa sifa ya kudhibiti matumizi ya baadhi ya maneno hadharani. Tamaduni za Kiafrika hasa zimewekea vikwazo matumizi ya maneno yanayochukuliwa kuwa machafu. Matumizi ya hadharani ya maneno yanayotaja tendo la mapenzi, sehemu za siri za mwili, tendo la kwenda haja, kifo, matusi, maradhi, hatari na majina ya Mungu yamepigwa marufuku. Badala ya kutumia maneno haya, tasfida hutumiwa. Hata hivyo, kuasisiwa kwa teknolojia mpya ya habari na mawasiliano na mitandao ya kijamii iliyofuatia kumesababisha kukiukwa kwa miiko hii. Mitandao ambayo imeathirika zaidi ni Facebook na Twita. Ni muhimu kukumbuka kwamba mawasiliano katika mitandao ya kijamii ni ya hadhara. Hii ina maana kwamba mawasiliano ya mitandao kama Facebook hufikia na kusomwa na watu wengi hata wale ambao hawakulengwa na mwasilianaji. Hali hii imefanya ujumbe wa mitandao kama Facebook kutoweza kuchukuliwa kama ujumbe wa siri. Makala haya basi yanajadili lugha mwiko katika Facebook na tasfida zinazotumiwa katika Facebook pamoja na athari zake.

Maneno muhimu*:* Lugha mwiko, Facebook, mawasiliano, mitandao

Kiswahili kuwa Lugha Mama, Daraja la Umoja katika Muungano wa Afrika Mashariki

Turizeye J.Claude
Wizara ya Muungano wa Afrika Mashariki
Idara ya Mambo ya Ushirikiano
Bujumbura-Burundi
tumaiclo1@gmail.com

Ulimwenguni kote lugha ndiyo chombo cha wanadamu cha kuwasiliana. Watu huongea katika lugha tofauti ila kuna nchi zinazofananisha lugha na zinatumia lugha moja, na kuna zingine zinatofautiana sana. Kutoongea lugha isiyo yako kiasili haimaanishi kwamba huezi kujifunza lugha hiyo bali ukiijua itakuwa daraja la kuingia katika mataifa mengine yanayoiongea lugha hiyo. Katika Afrika nzima lugha za kibantu huwa zinafanana, au kuna nchi zinazoongea lugha moja na ukweli unakuja katika muungano wetu wa jumuiya ya afrika mashariki ambapo tuna lugha za kiasili ila lugha ya Kiswahili inatumiwa na watu wengi katika nchi hizo. Ni ukweli Tanzania na Kenya zinakuja mbele ila na zingine zinafuata kama Burundi, Rwanda na uganada bila kuisahau

sudani ya kusini. Kama Kiswahili kinatumiwa na watu wa Jumuiya, bora tuifanye Lugha Mama ili kuwa nguzo ya umoja wetu, pia, kupewa kipao mbele ya kuikuza na kuifundisha wananchi wote ili iwe daraja letu la kuleta mabadiliko katika Nyanja mbalimbali za Jumuiya.

Fasihi Elektroniki: Matokeo ya Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Wallace Mlaga
Chuo Kikuu cha Rwanda
wmlagha@ur.ac.rw

Makala haya yenye anwani "Fasihi Elektroniki: Matokeo ya Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia" yamechochewa na mada ndogo ya kongamano yenye anwani "Kiswahili, Sayansi, Teknolojia, na Uvumbuzi." Mada hii ndogo imetupatia fursa ya kujadili utanzu mpya wa fasihi ambao tunauita "fasihi elektroniki." Utanzu huu ni matokeo ya maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyoikumba dunia. Hii ni sawa na kuangalia namna ambavyo ulimwengu hapo awali ulikuwa na utanzu mmoja tu wa fasihi kabla ya uvumbuzi wa maandishi. Hivyo utanzu uliokuwepo ni fasihi simulizi tu. Wataalamu mbalimbali kama vile Mulokozi (1996) na Wamitila (2003) wamefanya uanishaji wa fasihi ya Kiswahili na kubainisha mgawanyo tanzu kuu mbili: fasihi simulizi na fasihi andishi. Ijapokuwa wataalamu wote hawa wanakiri kuwa fasihi ni moja tu bila kujali kuwa ni andishi au simulizi. Wataalamu hawa wawili tunapoaangalia hawatoi nafasi ya kuangalia tanzu mbalimbali mpya zilizoibuka kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kutokana na kutozingatia uvumbuzi uliotokana na sayansi na teknolojia, wataalamu hawa wanajikuta hawabainishi tanzu za fasihi simulizi kama vile filamu, maigizo ya runinga, vibonzo jongefu, futuhi au komedi, nyimbo za bongofleva, michezo ya redioni kama tanzu au vipera vinavyojitegemea. Wanashindwa kufanya hivi kwa kuwa wanashindwa kuamua kama tanzu husika zinaangukia katika fasihi simulizi au fasihi andishi. Kwa hakika uanishaji wa fasihi simulizi ukiishia tu kuangalia matawi mawili ya fasihi ya Kiswahili kuwa ni fasihi andishi na fasihi simulizi kuna tanzu ambazo zitakosa kwa kuwekwa liha ya kujadiliwa kama fasihi.Wapo wataalamu walioangalia athari za sayansi na teknolojia katika fasihi simulizi (Mutembei, 2007; Mrikaria, 2006). Wataalamu hawa wote hawapigi hatua ya kubainisha tanzu na vipera vipya vinavyoibuka ambavyo haviingii katika fasihi simulizi wala fasihi andishi. Hivyo makala haya yatajikita kubainisha ni kwa nini tunapaswa kuwa na tawi jipya la fasihi nje ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

Media Advocacy Communication Campaigns to Enhance Kiswahili Language Culture for Climate Change Adaptation Information Service in East Africa

Wilson Okaka
and
Irene Judith Nagasha
Kyambogo University – Uganda
judith.nagasha@gmail.com

This paper uses the East African Community climate change policy review to state a case for the social responsibility of the media in promoting Kiswahili culture for national and regional integration for climate change adaptation information service in the sub-region for SDG 13 progress by 2030. The objectives are to: explain the opportunities and challenges of developing a

common climate information services; discuss the effectiveness of media advocacy communication campaigns for regional and national climate change policy information access; assess the key stakeholders or actors in adaptation communication strategies; and explain the role of gender equality and women in achieving SDGs 13. The paper elaborates on the adverse consequences of climate change, the current efforts taken by the sub-region and the key information, knowledge, and policy gaps identified. The negative impact of climate change adaptation and mitigation policy or research gaps have disastrous social, environmental, economic, and political loss and damage. Hence, very urgent need to plan national and regional collaboration for climate change mitigation and develop comprehensive plans in response to the current and projected climate-related public communication. East Africa could face a more catastrophic social, economic, political, and ecological impact due to climate change damage and loss. A national-regional harmony of the climate change advocacy campaign strategy is an imperative for the timely attainment of the 2030 SDGs in the east Africa sub-region. Kiswahili language binds African unity to realise Africa's dream for global leadership, competitiveness, peaceful, and united in diversity.
Keywords: East Africa, language, media advocacy, climate change, Kiswahili, SDGs

Mchango wa Graffiti katika kuibua Fasihi Mpya

Willy Migodela
SAUT
migodela@hotmail.com

Makala haya yanahusu mchango wa *graffiti* (maandishi yaliyopo katika sehemu za umma) katika kuibua fasihi mpya. Makala haya yanaonesha maandishi yaandikwayo vyooni yalivyojaa ubunifu. Katika makala haya tumetathimini ubunifu unaojitokeza katika maandishi hayo. Vilevile makala haya yamebainisha na kupambanua upekee wa dhima ya ubunifu unaojitokeza. Ubunifu huo unajitokeza katika fani na katika maudhui hususani katika dhamira. Halikadhalika, makala haya yanaonesha usawiri wa hali mbalimbali katika jamii kama vile mtazamo kuhusu umuhimu wa elimu, dini, maadili na utamaduni. Mwisho, inahitimisha kwa kuonesha upya utokanao na graffiti katika fasihi.

Kilio cha Mwalimu J. K. Nyerere

Yasin S. Musa
Chuo Kikuu Cha Kiislamu Uganda
yasinimusa@yahoo.com

Hotuba ni usemi unaotolewa kwa hadhira kwa njia ya mazungumzo au maandishi kwa uzingatifu wa jambo mahsusi. Miongoni mwa maraisi wa nchi huwa mna waliojaaliwa vipaji vya kiuneni kiasi cha kuwafanya raia wa nchi zao kuyaamini yale wayasemayo na kuyaingiza katika utendaji wa maisha ya kila siku; mintaarafu ni Mwalimu Nyerere; hotuba zake zimegubika lugha makbuli ya Kiswahili. Mwalimu Nyerere alipendelea Kiswahili kitumike katika siasa za kiafrika badala ya lugha nyingine yeyote ya Ulaya kwa uoni kwamba kuendeleza lugha zao si tu kwamba ni kuukumbatia utumwa lakini kuuza utu wa Mwafrika – Bloommaert, 1990. Hotuba zake daima zimekuwa ni mshawasha kwa wasomaji na wasikilizaji kila uchao; hasa kwa jinsi zilivyo tagaza ufahima hususani katika kila nyanja ya maisha ya mwanadamu. Leo yake Mwalimu Nyerere

hatunaye tena. Kwa ushawishi wa hotuba zake, Watanzania wengi wanaamini lau kama angerudi duniani mafisadi, walarushwa na wasiopenda amani – ingekuwa patashika. Makala haya yameongozwa kwa nadharia ya Balagha (Rhetoric Theory); na madhumuni yake makuu ni kubainisha mbinu za kifani alizozitumia Mwalimu Nyerere kuendeleza maudhui yake kupitia hotuba zake hata ikawa ni abakie katika vinywa vya watu wengi, wakimlilia hadi hivi leo.

Usawiri wa mwanamke katika *Utenzi wa Vitimbi vya Wanawake*

Zaharia Mohamed Alawy

zamuafi@yahoo.com

Makala haya yana madhumuni ya kueleza usawiri wa mwanamke, kupitia "Utenzi wa Vitimbi vya Wanawake". Mwanamke amechorwa ni mtu asiyeaminika, asiyejitambua, asiyejielewa wala kueleweka. Anayeongozwa na utashi wa nafsi yake na mbaya kuliko yote ni ile ya *"samaki akioza mmoja kuambiwa wameoza wote*". Kosa la mmoja kuchukuliwa ni kosa la wote. Tatizo lililojitokeza ni mbinu iliyotumika kumkomboa mwanamke,kutokana na mfumo wa ubabedume. Ikitarajiwa ukombozi wake kupitia mazungumzo (siasa). Matokeo yake mwanamke amedhalilika zaidi. Mbinu zilizotumika katika makala haya ni ya maktabani. Kupitia matini husika na kuiona jinsi ilivyomsawiri mwanamke.Na kutambua ana nafasi gani katika jamii anayoishi. Makala haya imeelezea historia ya mwandishi kwa ufupi, dhana ya usawiri. Nadharia iliyotumika katika makala haya ni nadharia ya mtazamo kike. Kwa lengo la kuonesha mwanamke anahitaji kujikomboa, dhidi ya ukandamizwaji wa mwanamme. Kwa umuhimu wa uchambuzi wa makala haya; Imeelezwa kuwa mwanamke ni mtu wa kuenziwa na kuthaminiwa. Sio kudhalilishwa na kubandikiziwa kashfa juu ya kashfa, ni hasara iliyoje. Kwani kila mwanaadamu awe mwanamke au mwanamme ana uhusiano wa namna moja au nyengine na mwanamke. Hivyo kumdhalilisha au kumgandamiza mwanamke ni sawa na mtu kujidhalilisha mwenyewe.

Ushikamano wa Kisarufi katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Riwaya ya *Utengano*

Ziada Haji Ali
Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)
harthabai@gmail.com

Ushikamano ni dhana ya kisemantiki, ambayo hurejelea tabia au sifa za vipashio vikubwa zaidi ya mofimu, vinavyoambatanishwa pamoja katika sentensi ili kuunda matini. Dhana hii kwa muda mrefu imeonekana kama kuwa haiwezi kuangaliwa katika matini za fasihi, badala yake huangaliwa katika matini nyengine tu ambazo si za fasihi. Lengo la makala hii ni kuchunguza ushikamano wa kisarufi katika riwaya ya Kiswahili, ikitolewa mifano kutoka katika riwaya ya ***Utengano***, iliyoandikwa na Said Ahmed Mohammed mwaka 1980. Data za makala hii zimepatikana kwa njia ya kudurusu riwaya hiyo, na makala mbalimbali zilizosaidia kupatikana kwa data sahihi. Makala hii imebaini kuwa mwandishi wa riwaya ya ***Utengano*** ametumia vijenzi vya ushikamano vya aina nne katika kazi yake. Vijenzi hivyo ni urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na viunganishi. Makala hii itasaidia kutoa mwangaza kwa watafiti kuchambua kazi za fasihi kwa kutumia vipengele

mbalimbali vya kiisimu. Vilevile itasaidia kuwakumbusha waandishi kuwa isimu na fasihi ni taaluma zenye uhusiano wa karibu hivyo katika uandishi wao waangalie taaluma zote mbili wasiegemee upande mmoja tu.

Mchango wa lahaja katika kukuza Kiswahili Sanifu: Mifano kutoka Istilahi za Tiba na Uuguzi

Zuhura Ali Moh'd

zuhura.mohd@yahoo.com

Lengo la makala haya ni kuonesha namna lahaja zinavyoweza kuchangia katika kukuza Kiswahili sanifu msisitizo ukiwa katika tasnia ya tiba na uuguzi.Wataalamu mbalimbali na vyombo vinavyojishughulisha na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili vimewahi kupendekeza misingi ya kufuata katika uundaji wa msamiati na istilahi za Kiswahili. Mathalani, BAKITA mwaka 1982, lilipendekeza kuwa msamiati na istilahi za Kiswahili ziundwe kwa kufuata misingi ifuatayo: Kwanza, kuchunguza lahaja mbalimbali za Kiswahili, Pili, kuangalia lugha za Kibantu, Tatu, kuchunguza lugha za Kiafrika, na kama imeshindikana kuangalia lugha nyingine nje ya Afrika. Licha ya mapendekezo hayo ni dhahiri kwamba misingi hiyo haijazingatiwa ipasavyo kwani kwa sasa msamiati na istilahi nyingi huingizwa katika Kiswahili sanifu kwa kutumia njia ya utohozi na istilahi fafanuzi. Data ya uchunguzi huu imekusanywa kutoka uwandani na maktabani. Uchambuzi na uchanganuzi wa data hiyo umeongozwa na nadharia ya teminografia. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa lahaja zinaweza kutumiwa kuongeza na kukuza msamiati na istilahi za Kiswahili sanifu hususani katika tasnia ya tiba na uuguzi. Hali hii inaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya utohozi kama mbinu za uundaji na ukuzaji wa msamiati na istilahi katika Kiswahili sanifu. Kutokana na data yetu tunashauri kuwa wataalamu wasikimbilie kutohoa badala yake wafanye uchunguzi katika lahaja mbalimbali za Kiswahili.